NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 19 Mei, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMARI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Nimwite sasa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa ajili ya maswali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya asanteni sana, ninayo orodha ya Wabunge ambao walijiorodhesha kwa ajili ya maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tutaanza na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sera ya nchi yetu kuhakikisha kwamba bandari zetu zinapanuliwa na kuboreshwa na ili ziweze kuwavutia wafanyabiashara wa nchi jirani kutumia bandari zetu, na hii tumefanikiwa sana kwa Bandari ya Dar es Salaam.

Swali langu je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuhakikisha wafanyabiashara wa Sudan Kusini na Uganda wanaitumia Bandari ya Tanga na wafanyabiashara wa Congo, Malawi na Zambia wanaitumia Bandari ya Mtwara? Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** *Bismillah*.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chikota, Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu kupitia Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imetenge fedha kwa ajili ya maboresho ya bandari zetu zote nchini, zile zilizoko Ukanda wa Bahari Kuu pia kwenye Maziwa Makuu ya kuimarisha miundombinu na huduma mbalimbali. Mkakati wa Serikali ambao Mheshimiwa Mbunge anataka kujua wa namna ya kuvutia matumizi ya bandari hizi kwa nchi jirani ipo na inasimamiwa pia na Wizara yetu ya Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, moja tunaongeza vifaa vinavyoweza kupakua na kupakia mizigo kwa muda mfupi ili kuwahakikishia wale wateja wetu kuwa matumizi ya bandari yanatumika kwa muda mfupi zaidi, lakini mbili, tumefanya mapitio ya tozo hasa kwa Bandari ya Tanga na kule Mtwara tumetoa fursa ya kupunguza tozo ili kuvutia kulinganisha na mahitaji ya Dar es Salaam kwa sababu Dar es Salaam wingi wa meli ni mkubwa sana kuliko Bandari ya Tanga na Dar es Salaam ambako pia hata msimu uliopita tumekuwa tukilishughulikia hili na hatimaye tukafikia hatua ya kupunguza tozo ya asilimia 30 ya meli yoyote inayokwenda Tanga kwa ajili ya kuwezesha nchi kama Somalia na Sudan ili kuweza kutumia Bandari ya Tanga na kule Mtwara kwa nchi kama Malawi, Zambia na hiyo Congo ambako pia ni rahisi kufika ili wale wateja wanaoleta mizigo kwenye Bandari hizi za Mtwara na Tanga waweze kuvutiwa zaidi..

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili tunaamini sasa tunaweza tukawavutia wengi kwasababu wakija Dar es Salaam tozo ni kubwa na pale Mtwara na Tanga tozo ni ndogo. Lakini bado tunaangalia pia kwenye eneo la ushushaji wa mafuta nako tumeimarisha vituo na zile mita za kushushia mafuta. Kwa hiyo, tunakaribisha pia na meli zinazoshusha mafuta kwenye bandari zetu za Mtwara na Tanga; na tumejenga pia na matenki ya kutosha. Kwa hiyo urahisishaji wa kazi kwenye bandari hizo ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini Mamlaka ya Bandari tumeona ikifanya jitihada mbalimbali kupitia Balozi zetu zilizoko kwenye nchi hizo kuhamasisha wafanyabiashara wa nchi hizo kutumia bandari zetu. Hili linaendelea na tumefungua pia hata ofisi za Mamlaka ya Bandari kama vile Congo na tumefungua ofisi Malawi, Zambia ili wateja wote wanaohitaji kupata huduma kupitia bandari yetu na bandari zetu zote watapata mawasiliano kwenye nchi zao bila ya kuwataka wao kuja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na jitihada nyingine nyingi ambazo tunazifanya ikiwemo na elimu ya kuelimisha wafanyabiashara mbalimbali kutumia bandari zetu za Tanzania. Lakini wote mnajua kwamba Serikali ya Awamu ya Sita nayo inaendelea kusimamia ukamilishaji wa reli ya kati ambayo itakuwa inabeba mizigo; ukamilishaji wa barabara ambako pia magari makubwa yatapita yakiwa yamebeba mizigo haya yote tunaamini wanaelewa.

Mheshimiwa Spika, na nitoe wito kwa wafanyabiashara wa ndani ya nchi na nje ya nchi kutumia vyema bandari zetu zote zilizoko ukanda wa Pwani pia kwenye maziwa yetu tuweze kuruhusu kuongeza uchumi zaidi kwenye nchi yetu na kwa mataifa ya nje tuwahakikishie usalama. Tanzania ni nchi salama na tumeendelea kuimarisha usalama ndani ya nchi. Kwa hiyo tunawahakikishia usalama wa mizigo yao. Wao wenyewe wanapoingia lakini pia wanapopeleka mizigo kwenda kwenye nchi zao. Haya yote tunaamini wafanyabiashara kupitia *forum* pia za mikutano ya wafanyabiashara wa Tanzania na nchi hizo

itaendelea pia kutoa elimu kwa nchi hizo kuleta mizigo na kutumia bandari yetu kuchukulia mizigo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana nchi yetu ilikumbwa na tatizo kubwa la soko la mahindi, hali iliyopelekea kwa Mikoa ya Kusini ikiwemo Ruvuma, Rukwa, Mbeya na Iringa kuuza zao hilo kwa shilingi 15,000 kwa gunia; na hii ilitokana na baadhi ya wakulima na wafanyabiashara kudhani kwamba zao hili kuna zuio la kuuza nje ya nchi.

Swali langu, nini kauli ya Serikali kuhusu zao hili kwa msimu huu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Mbinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchi yetu kupitia Mikoa ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini wanazalisha sana mahindi na mimi nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wakulima wa maeneo haya. Kwa sababu leo hii nchi yetu tunaposema tuna uhakika wa usalama wa chakula kwa maana ya kuwa na kiwango kikubwa cha chakula kinatokana na jitihada zinazofanywa na wakulima nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zao la mahindi ni kweli mwaka jana tulipata tatizo kidogo kwa sababu bei ilishuka na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema wakulima wengi walidhani kwamba tumeweka zuio la kupeleka mahindi nje katika kutafuta soko. Tumekuwa na mikutano mingi na

Waheshimiwa Wabunge wa mikoa hiyo kuwahakikishia kwamba Serikali haina zuio hilo. Pia tuliwahi kutoa tangazo hapa mbele ya Bunge lako tukufu ili kuwahakikishia wakulima.

Mheshimiwa Spika, nini tunachokifanya kwenye eneo hili, kwanza lazima tujiridhishe na usalama wa chakula au kiwango cha chakula ndani ya nchi kwamba tuna chakula cha kutosha pia tunakuwa na ziada. Ile ziada ndio ambayo tunaruhusu kuuzwa nje ili ndani ya nchi tusiwe na shida ya chakula. Kwa hiyo, pia hata msimu huu uzalishaji wa chakula msimu huu pindi Wizara ya Kilimo ambayo imekamilisha bajeti yake jana ikishafanya tathmini zake na kujua kiwango cha chakula tulichonacho na kuitambua ile ziada; ile ziada tunatoa kibali cha kuuza nje ili wakulima waweze kupata masoko ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu tunaoutumia hapa hatupeleki tu nje holela, bali yule mkulima ambaye anataka kupeleka nje kwa mfano Mikoa ya Rukwa, kupeleka Zambia, Congo na maeneo mengine omba kibali tu kwa Mkuu wa Wilaya ili Mkuu wa Wilaya ajue leo tunatoa tani ngapi nje na sisi itatusaidia pia kujua tumeingiza shilingi ngapi fedha za kigeni kupitia zao la mahindi.

Kwa hiyo, utaratibu ni huo mkulima yeyote anayetaka kuuza nje atakwenda kwa Mkuu wa Wilaya kuomba kibali cha kupeleka nje na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ina Afisa wetu wa Kilimo ambaye pia anaangalia kiwango cha chakula na uzalishaji wake ziada. Kwa hiyo, na yeye pia anajua leo imeombwa kibali cha tani 10, kesho tani 20 akijumlisha anajua kwamba tunafikia kile kiwango cha ziada ambacho tunacho.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufatilia eneo hili Serikali inaendelea kufatilia mwendeno wa masoko ya nje ili kuwaruhusu wakulima waliozalisha hapa ndani waweze kupata masoko pia nje huo ndio utaratibu ambao tunautumia wa Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na malalamiko makubwa sana hapa nchini kwa ndugu zetu, Watanzania wenzetu waliokuwa watumishi Serikalini walioondolewa kwa kigezo cha kutokuwa na cheti cha *form four.*

Sasa ni lini watalipwa stahiki zao halali za kiutumishi ambazo wanadai ili waweze kupeleka watoto wao shule na wengine waweze kujitibisha? Nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ulipata taarifa wiki moja iliyopita agizo ambalo lilitolewa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan juu ya msamaha alioutoa kwa wale wote waliokuwa wameondolewa kwenye utumishi, waliokuwa wametambulika kama wameghushi vyeti vya kidato cha nne na wametumikia katika nchi hii kwamba sasa tufanye mapitio tuwatambue. Pia alitoa fursa la kuunda timu kutoka Wizara ya Utumishi na Utawala Bora kwa pamoja na TAMISEMI ili kuwatambua wale wote waliotumikia kwenye nchi hii na kutoa agizo kwamba walipwe asilimia tano ya *pension* walikuwa na mchango kwenye *pension* waliokuwa wanaichangia ili waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Tume ile itakapokamilisha kazi tutayatambua haya yote, idadi yao, halafu pia wangapi, wale wote ambao wanastahili kupata hiyo asilimia tano ya mchango waliokuwa wanauchangia, lakini pia kuona makundi mengine na maelekezo yanayotolewa.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameunda Tume naomba nisitoe majibu juu ya hilo tuiache Tume ifanye kazi yake, halafu tutapata majibu sahihi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2014 tulitunga Sheria ya Tozo ya Ujuzi na Maendeleo ambapo mwajiri wa sekta binafsi wenye wafanyakazi zaidi ya kumi walitakiwa kuchangia asilimia nne kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha *VETA*. Lakini asilimia mbili zilielekezwa kwenda kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Kwa kuwa sasa Serikali imejenga *VETA* nyingi nchini; na kwa kuwa ofisi yako sasa hivi imetoa fursa kwa vijana wengi kuweza kujiunga na mafunzo haya ya muda mfupi ili waweze kujiajiri na kuajiriwa.

Ni kwa nini sasa Serikali isione ni muda muafaka wa kurejesha ile asilimia mbili ile iliyopelekwa kwenye bodi ya mikopo iweze kurudi *VETA* ili waweze kutumia kukopesha wanafunzi hawa vifaa ambavyo watajifunzia na baadaye waweze kuondoka navyo kwenda navyo mtaani vya kuanzia kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulitunga sheria inayotengeneza mgao wa fedha ambazo pia tungependa tuzione zikitumika kwenye vyuo vyetu vya elimu hasa kwenye ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua mpango wa Serikali utakaowezesha vijana wanaohitimu *VETA* baada ya kuwa tumejenga *VETA* nyingi

nchini namna ya kuwasaidia wanaohitimu ili waweze kuanza vizuri.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Serikali imeanza kuimarisha sekta hii ya ujuzi kwa utaratibu, mwanzo tumeanza kujenga *VETA* na tulianza kujenga *VETA* kila mkoa, kazi ambayo tumekamilisha siku chache zilizopita; na mimi nimepata nafasi ya kupita mikoa mingi kuona maendeleo ya ujenzi; lakini pili tumeanza na programu ya ujenzi wa *VETA* kila wilaya zoezi ambalo sasa linaendelea. *(Makofi)*

Msimu uliopita tulipata fedha, Waheshimiwa Wabunge mlipitisha bajeti ya kujenga *VETA* 28 kazi ambayo inaenda mwishoni ili pia tuweze kujenga *VETA* nyingine.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tunaenda kwa awamu, tumeanza na ujenzi wa miundombinu, lakini mbili tunatoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, halafu tuje tuone sasa tuna idadi gani ya wanafunzi wanaohitimu, tuweze kutenga fecha pamoja na hiyo tozo ambayo pia tunatoza na ile asilimia tunayoitenga tuiingize kwenye mpango huo ili kutoa vifaa vitakavyowezesha kijana huyu anayehitimu kuanza mafunzo yake na stadi yake mara tu anapohitimu. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kulifanyia kazi jambo hili ili kuona hawa vijana wetu wanaoingia kwenye vyuo hivi kwa ajili ya kupata ufundi stadi anapomaliza anaanza kazi moja kwa moja.

Kwa hiyo kadri tunavyoendelea Wizara ya Elimu ambayo ndiyo inashughulikia elimu ya ufundi kupitia *VETA* itaendelea kuratibu na kuomba fedha zaidi na tunashukuru mmetupitishia bajeti ya Wizara ya Elimu katika sekta mbalimbali ikiwemo kwenye eneo la ujuzi, ili tuweze kuhakikisha kwamba vijana wa Kitanzania wanakuwa na ujuzi katika fani mbalimbali ambazo wao wanazihitaji ziwasaidie pia kwenye kujitafutia ajira au pia wao wenyewe kuwaajiri wengine, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwakuwa baadhi ya maeneo yenye migogoro na hifadhi za Taifa hayajajumuishwa kwenye ile Kamati ya Wizara nane na hata mengine yaliyojumuishwa nayo uamuzi bado haujatolewa na Serikali.

Je, ni lini sasa zoezi hili litaanza rasmi na kumalizika ili wananchi waendelee na shughuli zao bila wasiwasi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu nikupe uhuru wa kujibu hilo swali, kama unayo majibu, kama huna linapaswa kujibiwa na Waziri mwenye sekta.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtega, Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru umenipa nafasi ya kulijibu swali hili kwa sababu timu ya Mawaziri wanane kutoka Wizara zile shiriki imeendelea kufanya kazi ya kutambua maeneo yote yenye mgogoro na kazi hii tulianza mwaka 2019. Tayari tumeshaainisha maeneo yote na tulileta taarifa hapa Bungeni ya vijiji vilivyofikiwa vilivyokuwa na migogoro lakini katika kutatua migogoro hii iliyopo kati ya wakulima na wafugaji, wakulima na wananchi na hifadhi, lakini pia hata maeneo ya ulinzi tumeweza kuratibu vizuri na ile timu pia hata wiki iliyopita ilikuwa imesafiri kwenda kukamilisha hiyo kazi na kazi bado inaendelea.

Mheshimiwa Spika, migogoro hii ina ngazi mbalimbali na sisi Serikali tumeweka utaratibu; kwanza migogoro yote ya ardhi inaratibiwa na ngazi za vijiji kwanza kwenye maeneo yenye migogoro, na zile kamati zinao uwezo wa kumaliza migogoro hii kwa kukutanisha wenye migogoro, lakini pia ngazi ya Kata, ngazi wa Wilaya na Mkoa. Leo tunazungumzia Wizara nane matatizo yanayoshughulikiwa na Wizara hizi

nane ni yale makubwa tu, ambayo yanahitaji pia kukutanisha wataalam wa ngazi za Wizara na ndio kwa sababu Wizara nane zote zinazunguka na kupitia migogoro ile mikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilitaka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na kazi ya kuondoa migogoro inayojitokeza kwenye maeneo yetu na tunafanikiwa kwa kiasi kikubwa na tunaendelea kubainisha maeneo yenye migogoro yenye tija na yasiyokuwa na tija, lengo hapa ni kuwataka Watanzania kila mmoja afanye kazi yake, wale wakulima waendelee kufanya kazi zao, wanaoshughulikia mifugo, uvuvi na maeneo mengine, lakini pia hata hifadhi zetu nazo zifanye kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwenye hifadhi wote mnatambua Serikali hii pia ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, imeridhia maeneo yale ya hifadhi ambayo kwa sasa yanaonekana hayana tija tunayaruhusu wananchi wafanye shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utaratibu huu unaendele kuratibiwa na pindi watakapokamilisha tutakuja kutoa taarifa kwenye Bunge lako tukufu ili Waheshimiwa Wabunge mnaotoka kwenye maeneo hayo muwe na taarifa hiyo. Kwa hiyo tutakamilisha wakati wowote tu kwa haraka zaidi ili na nyie mpate taarifa na migogoro iishe kwenye maeneo yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ninatambua changamoto kubwa iliyopo ya ajira kwa vijana wetu, changamoto ambayo ni ya kidunia, lakini nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa juhudi kubwa ambazo imeendelea kuzichukua

kuhakikisha kwamba vijana hawa wanaweza kujiajiri ama kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali sasa inaonaje inapokuwa inatoa kibali cha ajira na kuzitangaza ajira ikawepo asilimia fulani ambayo itakuwa ni maalum kwa ajili ya vijana wenye ulemavu wenye sifa zinazotakiwa. Tofauti na ilivyo sasa hivi ambapo vijana hawa wamejikuta wanaomba ajira na kukosa na hivyo kuendelea kupelekea ugumu wa maisha kwao na hasa ikizingatiwa kwamba ulemavu na gharama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ikupa, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu kwenye mfumo wetu wa ajira, utaratibu ambao pia unawatambua wenzetu wenye mahitaji maalum ambao pia wanaomba ajira kwenye eneo husika, tumeunda Tume, Tume inaitwa Tume ya Ajira ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais Utumishi, na tumejiwekea kanuni ambayo pia Tume ya Ajira inasimamia kanuni hii na pia tumetoa maelekezo kwenye sekta zote za ajira kwamba kila panapokuwa na nafasi ya ajira lazima tutenge asilimia tatu kati ya wajiriwa 20 iwe ni kwa ajili ya walemavu. Kwa utaratibu huu ambao tunaendelea nao sasa umewezesha wenzetu wengi wenye ulemavu kupata ajira kwenye sekta mbalimbali, muhimu ni kuwa na zile sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna maeneo ambayo pia hata kama hana sifa, lakini ana uwezo na anaweza akafanya kazi hiyo, basi Tume huwa inatoa fursa ya kuweza kuingia kwenye ajira na maelekezo ambayo tumeyatoa kwenye eneo hili ndugu zetu wenye ulemavu wanapata nafasi ya awali hata kwenye *interview* (kwenye mahojiano) wao wanaanza kwanza wanakamilisha alafu wengine wanafuata. Hii yote nikutambua wenzetu ili na wao pia waweze kuingia kwenye mfumo wa ajira.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Ikupa kwamba Serikali kupitia utaratibu huu inaendelea kuwahakikishia wale wenzetu wote wenye mahitaji maalum au wenye ulemavu kwamba pindi tunapotoa nafasi za ajira na wao pia watapata fursa ya kuwa sehemu ya watakaoajiriwa na wote mnaona kwenye sekta mbalimbali mnaona waajiriwa wapo, hata kwenye teuzi za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu ametambua hili amefanya uteuzi kwenye ngazi mbalimbali Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Maafisa mbalimbali kwenye sekta zote, hii maana yake ni nini; kuonesha kwamba Serikali inatambua uwepo wa ndugu zetu wenye ulemavu ambao pia wanao uwezo mkubwa wa kufanya kazi kuliko hata sisi ambao tuko imara kwenye viungo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niwahakikishie wale wote ambao wangetamani kuomba nafasi za ajira Serikalini ambao ni walemavu wajitokeze kila wanaposikia ajira kwa sababu fursa ipo na inatekelezwa kupitia taasisi zote zinazoajiri, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Edwin Malleko Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kumuuliza Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mikoa takribani 15 ya Tanzania ikiwemo Kilimanjaro, Kagera, Tanga, Ruvuma na mingineyo uchumi wake unategemea sana zao la kahawa, lakini zao hili halina ruzuku.

Ni nini msimamo wa Serikali kuhakikisha zao hili linapata ruzuku kama ilivyo kwa mazao mengine ya kimkakati? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Malleko, Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kahawa ni miongoni mwa mazao yanayotegemea kupandisha uchumi kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye mikoa ambayo Mheshimiwa ameitaja; na mimi juzi nilikuwa Mkoani Kagera kushughulikia zao hilo hilo, lakini pia jana tumekamilisha bajeti ya Wizara ya Kilimo na limechangiwa sana na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa juu ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo mkakati wa Serikali kutoa ruzuku kwenye mazao mbalimbali ikiwemo kahawa na ruzuku inategemea sana kwenye zao hilo mahitaji yake makubwa kwa sababu kila zao lina mahitaji yake, lakini tunajua tuna suala la mbegu au miche wakati mwingine, lakini pia tuna madawa kwa maana ya pembejeo madawa, mbolea lakini pia namna bora ya kulisimamia zao hili hata maghala nayo pia tunaweza kuweka ruzuku kama alivyosema Waziri wa Kilimo jana. Zao la kahawa linalolimwa Kagera na kule Kilimanjaro kila eneo linategemea na mahitaji yao na hayo mahitaji ndio tunayoyafanyia ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano juzi nilipokuwa Kagera Vyama Vikuu vya Ushirika vilikuwa vinazungumzia wakulima wao kwamba kuna umuhimu wa kuongeza ruzuku kupata miche, lakini pia kuna tatizo la upungufu maghala na wanahitaji ruzuku kwa ajili ya maghala. Kwa hiyo unaweza ukaenda Mbinga nilishakwenda Mbinga wakati tunasimamia zao hili kule sehemu kubwa ilikuwa ni kupata ruzuku ya kupata mbolea kwa sababu Mbinga bila mbolea huwezi kukuza zao hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ruzuku inategemea na mahitaji ya zao na eneo hilo kwa hiyo Serikali imeweka utaratibu wa kutoa ruzuku na kwenye kahawa kama kule Kagera tumetoa ruzuku kwenye miche kupitia taasisi ya utafiti ya *TACRI*. Lakini pia tumeshakubaliana na Waziri na Waziri ameshaahidi kule Kagera kujenga maghala ambako pia

tunaanza na mfumo wa masoko kupitia stakabadhi ghalani ambayo inahitaji kuwa na maghala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ruzuku huko Mkoani Kilimanjaro na maeneo mengine tutakapokuja tutajua mahitaji ni nini na tutaona uwezo wa Serikali na mpango ambao tumeweka ruzuku basi tutatoa ruzuku kutegemea na eneo hilo na mahitaji ya zao hilo; huo ndio utaratibu ambao tunautumia kwenye mazao yetu karibu yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna upimaji wa ardhi na maeneo mbalimbali yenye migogoro ya ardhi ikiongozwa na Wizara nane, sehemu nyingine ambazo zinapimwa ni maeneo ambayo yapo mbali na vyanzo vya maji nchini, imeleta taharuki kubwa kwa wananchi katika upimaji huu kiasi ambacho wananchi wanajua wanabomolewa nyumba zao nchini katika taharuki hii ya upimaji katika maeneo ya maji ya upimaji wa ardhi.

Je, Serikali ina kauli gani kwa wananchi kuondoa taharuki hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, swali linarudi tena kwa sura nyingine la migogoro kwenye maeneo, lakini natambua mara kadhaa nimekuwa nikipita Morogoro na Mheshimiwa Mbunge mara kadhaa amekuja na wananchi wanaotoka kwenye eneo lake hasa kule Mindu wakizungumzia ile amri ya ujenzi wa makazi umbali wa mita 60 na zaidi ya 60 na kule ilikuwa mita 500 kulikuwa na mgogoro wa aina hii.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza awali kwamba ile timu ya Mawaziri ambayo inaratibu migogoro ya kitaifa na kwamba Serikali imeweka utaratibu wa kutatua migogoro kulingana na ukubwa wa migogoro na ngazi ambazo tumezipanga kutoka ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na hatimaye Taifa kupitia timu yetu ya Mawaziri. Mgogoro ambao Mheshimiwa Abood mara kadhaa amekuwa akiusimamia na kuwasemea wananchi wake wa kule Mindu, bado kazi tunaendelea kuifanya na tunashirikiana na Ofisi ya Mkoa ili kuhakikisha mgogoro wa aina hii popote unapotokea ikiwepo na hapo Mindu tunaisimamia kwa karibu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakapoona sasa kuna umuhimu wa kuleta timu ya Mawaziri wanane tutawaleta Mheshimiwa Abood pale Mindu ili kukaa na wananchi, kuwaelimisha na kuona namna nzuri ya kuwawezesha kufanya shughuli zao za kijamii ikiwemo na kilimo na hasa eneo lile.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Abood swali lake hili ambalo amelizungumza kwa ujumla jumla lakini kwakuwa na mimi nimeshashughulikia tatizo la Mindu pale Morogoro niendelee kumhakikishia kwamba tunashughulikia na tutatatua tatizo lile kwa haraka sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, muda wako wa kujibu maswali umekwisha, ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na maswali ya kawaida tutaanza na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 224

**Upatikanaji wa Umeme wa *REA* kwenye Vijiji vyote vya Songwe**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango wa kuhakikisha vijiji vyote vya Mkoa wa Songwe vinapata umeme wa *REA?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Songwe una jumla ya vijiji 307; vijiji 180 vina umeme na vijiji 127 havijafikiwa na miundombinu ya umeme. Vijiji hivyo 127 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme vinanufaika kupitia mradi wa *REA III* mzunguko wa pili unaoendelea. Utekelezaji wa mradi unaendelea na Mkandarasi *Derm Electrics* ndiye anayetekeleza mradi kwa kipindi cha miezi kumi na nane kwa gharama ya shilingi bilioni 11.23. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niwe na swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara imekuwa na utaratibu wa kufikisha huduma katika makao makuu ya vijiji na kusababisha watu wa vitongoji kukosa huduma.

Je, ni lini Wizara hii itaanza kufikisha huduma hii kwenye vitongoji ili wananchi wengi waweze kufikiwa na huduma hii ya Umeme? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hatua ya kupeleka miundombinu ya umeme kwenye maeneo yote ya vijiji imekuwa ikienda awamu kwa awamu, ni kwamba tulianza na vijiji kidogo kulingana na uwezo wa Serikali uliokuwepo, lakini baadaye Serikali ikajihimu na kuhakikisha vijiji vyote vinafikishiwa miundombinu ya umeme angalau kwa kuanza na makao makuu ya vijiji. Lakini ipo mipango ya Serikali madhubuti kabisa ya kuhakikisha kwamba kila eneo linafikiwa na umeme na njia hizo ni kwa kuanza na miradi yetu ya ujazilizi inayoitwa *densification* ambapo tuna ya kwanza, ya pili na ya tatu zinaendelea, na zitaendelea kufanyika kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali imeona ni vema kutafuta fedha nyingi kwa wakati mmoja na kumaliza vitongoji vyote ambavyo havijafikiwa na umeme na kama ambavyo tumeshasema mara kadhaa hapa Bungeni tumeona kwamba tunahitaji takribani shilingi trilioni sita na bilioni kama mita tano ili kumaliza maeneo yote ya vitongoji na Serikali ipo katika harakati za kuhakikisha kwamba inapata fedha hii kufikisha umeme katika maeneo hayo, lakini katika kipindi hiki cha kuanzia fedha inapopatikana Serikali inazidi kusogeza miundombinu ya umeme katika vitongoji kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mbulu Vijijini kuna vitongoji 400 na vijiji 76; ulifika Mheshimiwa Waziri ukatoa ahadi vijiji vyote vitapata umeme.

Je, ni lini ahadi yako inatekelezwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay kama nilivyojibu swali la msingi kwamba kadri Serikali inavyoendelea kupata fedha itajitahidi kuhakikisha kwamba vitongoji vyote vinapatiwa umeme katika muda mfupi ujao.

**SPIKA:** Mheshimwia Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; Mkoa wa Mara ni kati ya Mikoa iliyokaa kimkakati ukizingatia ni Mkoa uliomtoa Muasisi Mwalimu Julias Kambarage Nyerere.

Je, ni lini Serikali itapeleka Umeme wa *REA* katika vijiji vyote vya Mkoa wa Mara ukizingatia wakati wakiomba kura Mama yetu Samia Suluhu Hassan na Hayati Magufuli waliahidi kwamba vijiji vyote vilivyobaki vitapata umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Marwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyozungumza mradi kabambe wa kupeleka umeme kwenye vijiji unaoitwa *REA III Round Two* unaendelea katika vijiji vyote nchini, na Mkoa wa Mara ni mmojawapo kati ya maeneo hayo. Na ninakumbuka mkandarasi anayepeleka umeme katika maeneo haya anaitwa *Giza Cables***,** anapeleka umeme katika Mikoa ya Manyara na Mara, na tunatarajia kufikia Desemba mwaka huu vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya

umeme vitakuwa vimefikiwa na umeme kwa mkataba tuliokuwa nao na tunasimamia kwa karibu kabisa kwa sababu pesa tunayo na kazi inaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, katika vijiji ambavyo vilipatwa na changamoto ya umeme kutokukamilika ni vijiji takribani vyote vya kata kama tatu hivi katika Jimbo la Lulindi; Kata ya Mchauru kulikuwa na hiyo; Kata ya Sindano, Kata ya Luatala.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha vijiji hivi vilivyokosa umeme mpaka sasa hivi katika kata hizo na maeneo mengine ya Lulindi vinapata umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nikwamba ifikapo Desemba, 2022 Serikali imeji-*commit* kuhakikisha inafikisha miundombinu ya umeme katika vijiji vyote Tanzania Bara ambavyo havijafikiwa na umeme na kazi zinaendelea katika maeneo mbalimbali, wakandarasi wako *site* wanaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa katika Jimbo la Vwawa kuna vijiji 31 ambavyo bado havina umeme, na kwa kuwa mkandarasi sasa hivi karibu mwaka mmoja umekatika hakuna kijiji hata kimoja ambacho kimepata umeme. Je, Serikali inatuhakikishiaje kwamba kufikia Desemba vijiji vyote hivyo vitakuwa vimewashwa umeme?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, taratibu za kupeleka umeme wa *REA* na miradi mingine mikubwa uko katika awamu tofauti tofauti na kwa harakaharaka tunayo awamu ya kumpata mkandarasi na tukishasaini mkataba anakwenda *site* kufanya *physical verification,* anakwenda kukagua maeneo na kuona uhalisia wake, lakini tunarudi mezani yeye pamoja na *TANESCO* na *REA* kuangalia na kukubaliana *scope* ya kazi yenyewe ambayo inatakiwa ifanyike halafu anakwenda kwenye hatua ya tatu ya kuagiza vifaa na hatua ya nne ni ya kwenda *site* na kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwa Mheshimiwa Japhet Hasunga mojawapo au mbili au tatu ya hatua hizo zinaendelea, na tunatarajia ifikapo Desemba muda wa kufanya kazi kwa miezi hii sita, saba iliyobakia tutakabana na wakandarasi kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma hii ya umeme kwenye maeneo yote kwa sababu tayari vifaa vimeshanunuliwa na *surveys* zilishafanyika na sasa wako *site* wanaendelea kufanya kazi, kwa hiyo kazi zitakamilika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kule kwenye Jimbo la Tarime Vijijini eneo la Nyamungo na Nyamwaga wananchi wangu wamekwenda kulipia nguzo za umeme wa *REA* badala ya kulipia shilingi 27,000 wamedaiwa shilingi 515,000 kwa nguzo moja.

Naomba nipate kauli ya Serikali kwamba bei imebaki shilingi 27,000 ile ambayo tulikubaliana kwa wananchi wetu au kuna mabadiliko mengine sasa ya gharama ya umeme wa *REA? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi kidogo, sikusikia vizuri, nitashindwa kutoa majibu mazuri. Naomba kwa ridhaa yako arudie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama mmetoa bei mpya kwa sababu wananchi wake badala ya kudaiwa shilingi 27,000 wanadaiwa shilingi 500,000.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Waitara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, bei za umeme za maeneo ya vijijini ni shilingi 27,000 bila kujali habari ya nguzo au *transfoma* au nini; kwa vijijini ni shilingi 27,000. Maeneo ya mijini ndiyo yamerudia kwenye zile bei ambazo tayari Serikali inaweka ruzuku ili ziweze kuwa za chini kidogo ili wananchi waweze kuzikimu, lakini kwa vijijini ni shilingi 27,000.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Bakorongo kilikamilika na kufunguliwa na Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mwaka 2007, tangu hapo maelekezo yamekuwa yakitolewa kiwekewe umeme na hakijawekewa.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua nini kauli ya Serikali kuhusu kuweka umeme katika kituo hicho cha afya? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunayo maeneo mengi ya taasisi za umma ambayo hayajafikiwa na umeme, kwenye vituo vya afya, vyanzo vya maji, shule na taasisi za dini. Baada ya kuona mahitaji makubwa wenzetu wa *REA* wamekuja na mkakati na mradi maalum ambao tutapeleka umeme katika vyanzo vya maji, vituo vya afya na migodi ili kuharakisha na kurahisisha ufikaji wa miundombinu ya umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya kutoka hapa basi nizungumze na Mheshimiwa Mbunge ili tuone kama liko *captured* kwenye huo mradi wetu ambao tunatarajia unaweza ukaanza mwishoni mwa mwaka huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Tarafa nzima ya Mungaa katika Jimbo la Singida Mashariki nilishasema hapa haina umeme hata kijiji kimoja. Lakini juhudi zilifanyika, kata nne zimeshawekewa nguzo leo ni mwezi wa nne unakwenda wa tano.

Ni lini sasa mkandarasi atarudi kuja kuweka nyaya na transfoma ili wananchi wale waanze kupata umeme wakati wengine wanasubiria kumalizia nguzo zilizobaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtaturu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kulitokea changamoto ya ongezeko la bei, hasa kwenye bidhaa za vyuma, *copper* na *aluminium* ambazo zinatumika kutengeneza *transfoma,* nyaya na *accessories* nyingine katika uunganishaji wa umeme.

Katika kujadili tatizo hili na kulitatua imetuchukua kidogo muda, lakini tunakaribia kumaliza jambo hili na tunaamini mwishoni mwa mwezi huu basi habari ya kuvuta waya, kufunga *transfoma* na mengine yataendelea kwenye maeneo ambayo tayari nguzo zilishasimamishwa. Na ninaelekeza kwa wakandarasi yale maeneo ambayo bado nguzo hazijasimama basi kazi zisizohusika na ongezeko la bei ziendelee kufanyika wakati mambo mengine haya yakiendelea kukamilika, kuhakikisha kwamba umeme unafika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Geita Mjini kata nane hazijafikiwa na umeme mpaka leo. Serikali iliahidi kwamba kutakuwa na mradi wa *peri urban* ambao ungeanza mwezi Aprili, lakini leo ni mwezi Mei mradi huo haujaanza. Ni lini mradi huo utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Constantine Kanyasu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo yako mijini lakini yana muonekano wa kuwa vijijini, ukiachana na kwake Geita, hata Jimbo ninalotoka mimi la Bukoba Mjini lina hali hiyo hiyo; na ni kweli Serikali iko katika harakati za mwisho za kukamilisha Mradi wa *peri urban* ambao tunatarajia utaanza kufikia mwezi Julai ili kupeleka umeme katika maeneo ya mijini, lakini yenye muonekano wa vijiji.

Nimuombe Mheshimiwa Mbunge awaambie wananchi wavumilie kidogo, Serikali ya Awamu ya Sita itatimiza ahadi yake na mimi nimo humohumo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kata tatu za Kilolo yaani Ukwega, Nyanzwa na Udekwa, hazina umeme, na mkandarasi alikuja akachomeka nguzo, sasa ni miezi sita haonekani.

Je, Serikali iko tayari kumuita na kumtafuta huko aliko ili aende akamalizie ile kazi kule? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyamoga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo moja na eneo lingine hatua za utekelezaji zinatofautiana kulingana na mkandarasi alianza lini na amepata vifaa wapi na mambo kama hayo na kama nilivyoelekeza wakandarasi wote waendelee na kazi zisizohusiana na mazungumzo tunayoyafanya kuhusiana na bei.

Mheshimiwa Spika, naomba nikitoka hapa niwasiliane na Mheshimiwa Nyamoga ili nione hasa kwake kuna changamoto gani mahususi ili kama ni kuitatua mara moja tuitatue, kama ni ile ambayo inaendelea kwenye taratibu nyingine basi namhakikishia kwamba kazi itaendelea na itakamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitangaza mabadiliko ya bei za umeme kwa wananchi wanaoishi mjini. Wananchi wanaoishi pembezoni mwa mji mfano Kishiri, Sangabuye, Buhongwa na Kayenze na tayari walishalipia umeme wa shilingi 27,000.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawekea umeme? Walishalipa kabla ya tangazo la Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa majibu kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba kusema maneno machache yenye uhalisia na ukweli; wale wote waliokuwa wamelipa shilingi 27,000 kabla ya mabadiliko ya bei wataunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, agizo hili liko kwa Mameneja wote wa Mikoa na wa Wilaya na wanajua, na tulikubaliana kuwa wale wenzetu waliokuwa wametangulia kulipa wapewe kipaumbele kwa kufanya *first in first out.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wale ambao bado hawajaunganishiwa na walishalipa shilingi 27,000 wasiwe na wasiwasi gharama italipwa na wale ambao wanaona wamechukua muda mrefu naomba tuwasiliane ili tuweze kuona tatizo na changamoto iko wapi ili tuweze kuondokana na tatizo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 225

**Barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Mkiwa – Itigi hadi Rungwa inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Singida utaanza kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Makongolosi – Rungwa – Mkiwa kwa awamu. Taratibu za manunuzi ya mkandarasi wa kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Noranga – Itigi eneo la Mlongoji yenye urefu wa kilometa 25 zipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba.

Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kujenga sehemu ya kilometa 31.9 kati ya Itigi Kitongoji cha Mlongoji na Mgandu kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu iliyobaki Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yana dhamira njema ya kuunganisha Mikoa ya Singida na Mbeya kwa barabara ya kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa maelezo yake Mheshimiwa Naibu Waziri; ni lini sasa huyu mkandarasi atafika Itigi ili wananchi nao waanze kufurahia matunda mazuri ya nchi yao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mkoa wa Singida unaunganishwa na Mkoa wa Simiyu kwa barabara ya vumbi kupitia Daraja la Sibiti. Je, ni lini sasa na barabara hii nayo itaweza kuanza ujenzi wa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inapokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge kwa kuanza ujenzi wa barabara hii. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati nakuja hapa Bungeni tayari mkandarasi wako wanasainiana mkataba na mara baada ya kufanya kazi hii naamini mkandarasi ataanza kukusanya vifaa ili kuweza kwenda kuanza hii kazi. Kwa sababu baada ya kusaini mkataba kazi inayofuata ni *mobilization* na kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili la kuunganisha Mkoa wa Singida na Simiyu; barabara hii aliyoitaja ambayo inapita Daraja la Sibiti tayari imeshakamilishwa kwa kufanyiwa usanifu wa kina. Daraja limeshajengwa; nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia kwamba katika mwaka huu wa fedha tumeongeza kilometa za kujenga barabara za lami ambazo zinaingia

kwenye Daraja la Sibiti mpaka kilometa 25. Na Serikali katika bajeti inayokuja nina hakika tutaanza kwa awamu kujenga vipande vya barabara za lami ili kuunganisha Mikoa ya Singida na Simiyu kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kufanya upembuzi yakinifu wa barabara ya milimani ya Mwembe – Mbaga – Mamba – Ndungu ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Je, barabara hii ya Mwembe – Mbaga ya milimani ni lini itatengewa fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakuwa shahidi barabara hii mimi tayari nimeshaitembelea na kuiona na kuona changamoto zake. Moja ya vitu ambavyo Serikali tunavifanya kwa *nature* ya barabara yake, tumemuagiza Meneja wa *TANROADS* hata kabla ya kuanza kufikiria kuijenga yote kwa kiwnago cha lami, aainishe maeneo yote korofi ambayo kipindi cha masika hayapitiki ili Serikali iweze kuyajenga na kuhakikisha kwamba mwaka wote barabara hii inapitika. Lakini taratibu zipo kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara yote aliyoitaja ya Mwamba – Miamba – Ndungu ili kufanya maandalizi kwa ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masasi – Nachingwea yenye kilometa 45 upembuzi yakinifu na wa kina umefanyika zaidi ya miaka tisa iliyopita. Ni lini Serikali itaanza ujenzi sasa barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chinguile, Mbunge wa Nachingwea, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ambayo inaunganisha Wilaya ya Masasi na Wilaya ya Nachingwea, kwa maana ya Mikoa wa Mtwara na Lindi, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii kama bajeti ambayo tunategemea kuiwasilisha wiki ijayo itapita, ipo kwenye mpango kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Nduguti – Iguguno yenye urefu wa kilometa 42 inayopita Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum - Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mattembe kwa kufuatilia miundombinu ya Mkoa wa Singida. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama ilivyo kwenye Ilani ya CCM barabara hii itaanza kufanyiwa usanifu wa kina na kukamilisha mwaka unaokuja wa fedha ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, tuna barabara inayounganisha Mikoa ya Kagera na Geita kutokea Katoke – Buharamulo kwenda kwenye Bandari ya Nyamirembe, na tuliahidiwa kwamba ingeanza kufanyiwa ujenzi mwaka huu wa fedha. Sasa tunaelekea ni mwezi wa tano sasa hivi imebaki miezi miwili hatujaona mkandarasi *site.*

Ni lini sasa barabara hii itaanziwa ujenzi ili wananchi wale waweze kuanza kuitumia ikiwa katika kiwango cha lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nyamirembe – Katoke inatoka kwenye Bandari ya Nyamirembe ambayo tayari imeshakamilishwa na lengo ni kuunganisha hii bandari na Biharamulo.

Mheshimiwa spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ipo kwenye mpango na imeshaombewa kibali ili iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni lini barabara ya kutoka Bukombe kuja Katoro yenye urefu wa kilometa 65 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Maana ni siku nyingi iliahidiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja inatekelezwa kwa mradi wa.... na taratibu zipo zinaendelea kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa barabara ya Makambako – Songea ni mbovu na nyembamba sana na hivi juzi imeleta ajali na watu tisa wamefariki.

Je, lini Serikali itatengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami yenye ubora kutoka Makambo mpaka Songea? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Njombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa kwamba barabara ya Makambako – Njombe hadi Songea ni barabara ambayo kwa kweli imechoka, ni barabara ya zamani sana, barabara ya tangu miaka ya 1984. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii tayari usanifu ulishakamilika na *World Bank* wameshaonesha nia ya kuijenga barabara hii upya ikiwa ni pamoja na kuipanua kwenye viwango vya sasa na mradi huu utahusisha pia na kujenga barabara ya *bypass* katika Mji wa Songea. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa ya swali la nyongeza.

Mchakato wa mkandarasi wa kujenga barabara ya Ntendo – Muze imechukua muda mrefu takribani miezi 11 mpaka sasa. Nataka kujua ni lini mkandarasi anaripoti *site* kuanza ujenzi wa lami katika barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deus Sangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ntendo – Muze – Kiliamatundu ina *package* mbili; mkandarasi tayari ameshasaini kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa za awali na kilometa zingine zinazoongezeka zipo kwenye taratibu za manunuzi. Kwa hiyo, muda wowote nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge mkandarasi atakuwa *site* kwa ajili ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaelekea Wizara ya Afya Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ikupa Stella Alex.

Na. 226

**Kurahisisha Mchakato wa Upatikanaji Bima ya Afya**

**MHE. STELLA I. ALEX K.n.y. MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha huduma ya upatikanaji wa bima ya afya kwa wananchi wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua ya ukamilishaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ambao utawezesha kurahisisha huduma ya upatikanaji wa bima za afya kwa wananchi wote. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, swali la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali Mheshimiwa Mariam Kisangi ana maswali mawili ya nyongeza.

Swali lake la kwanza linasema; ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam kumekuwa kuna ucheleweshwaji wa upatikanaji wa kadi za bima za afya yaani toka tarehe mtu analipia mpaka kuja kuipata ile kadi inaweza kuchukua hata miezi sita. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba kadi hizi zinapatikana kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili; linasema kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa figo wagonjwa ambao wanahitaji huduma ya kuzisafisha hizi. Nini kauli ya Serikali kuruhusu wagonjwa hawa kuwa na Bima za Afya hata kama ni zile za vifurushi vikubwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, labda nijibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja; ni ucheleweshaji wa bima ya afya ukilipia; ni ukweli kwamba umewekwa utaratibu kwamba toka unapolipia basi upate bima yako baada ya miezi mitatu na lengo lilikuwa ni moja tu kwamba watu wengi wakiwa na afya, wakiwa salama, wanakuwa hawana tabia ya kujiunga na bima watu wakadhani kwamba ni vizuri mtu akajiunga wakati hana ugonjwa wowote ili kulinda mfuko huo.

Lakini hili la miezi sita kwakweli nilakushughulikia kwamba tulishughulikie mapema ili watu wapate ndani ya muda uliopo. Lakini sasa wakati muswada unakuja hapa ambao sisi Wabunge ndiyo tutakaojadili basi tujadili tuone tunatakiwa upate kwa wakati gani na tutaweka utaratibu mzuri ambao hautaleta matatizo ambayo sasa mnayaona.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu wenzetu wenye matatizo ya figo; moja ni kwamba sisi wote tushirikiane kwa sababu suala moja ni kuhakikisha kwamba watu hawafiki mahali wanapata matatizo hayo ya figo, lakini ikitokea sasa wamepata basi kwa kweli Serikali inajitahidi.

Moja; ilikuwa kufanya *dialysis* kwa mara moja ni shilingi 380,000 lakini sasa hivi imeshuka mpaka shilingi 120,000 lakini bado ni gharama kubwa. Tutaendelea kuona namna ya kufanya ili hao watu wapungukiwe na mzigo kwa sababu kwanza wengi hawana uwezo wa kufanyakazi na wengine hawana kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 227

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi- Wilaya ya Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkalama ambacho ni gofu la ghorofa kwa muda mrefu sasa ilhali Wilaya haina kituo chenye hadhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi kinachojengwa katika Wilaya ya Mkalama ni Kituo cha Daraja A na ni cha ghorofa moja. Ujenzi wake umeanza Juni, 2015 na unatarajia kutumia jumla ya shilingi 792,450,000.00 hadi kumalizika kwake. Hadi sasa fedha zilizotumika ni shilingi 100,000,000.00 na kazi iliyobaki ni kumwaga silabu, kupaua na kazi za kumalizia. Katika mwaka ujao wa fedha 2022/2023 zimetengwa fedha kiasi cha shilingi 692,450,000 kwa ajili ya kumalizia kazi ya ujenzi wa kituo hicho. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali ninamaswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa mfumo wetu wa bajeti niwakutumia kadri unavyokusanya. Je, na kwa sababu kituo hiki ni cha Wilaya na ni chamuhimu sana Waziri ananiambiaje kuhusu kunipa kipaumbele katika fedha za maendeleo za kwanza tu zitakazopelekwa katika bajeti inayoanza Julai? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa upya wa Wilaya ya Mkalama tuna askari 83 tu, tuna upungufu wa askari 57. Je, Waziri ananipa *commitment* gani kuhusu vijana askari wanaomaliza kozi muda mfupi ujao kupeleka katika Wilaya yangu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja; tunamuhakikishia kwamba fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha ujao shilingi milioni 992 tutahakikisha kwamba zinapelekwa katika jimbo lake ili kukamilisha kituo hicho kama kipaumbele miongoni

mwa vipaumbele vilivyotajwa na Waziri wakati wa kuwasilisha bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, pili; tunatambua kwamba wanao askari 84 na katika mgao wa askari wanaotarajia kumaliza mafunzo zaidi ya 4000 waliopo vyuoni Wilaya ya Iramba ni moja ya maeneo ambayo yatazingatiwa ili kuhakikisha kwamba wanapata askari wa kutosha, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi kilichopo Kata ya Keza Wilayani Ngara kilijengwa kwa nguvu za wananchi, lakini mpaka sasa hakijamalizika; je, ni lini Serikali itamalizia kituo hicho? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wewe nisikilize mimi, achana na hao. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Ngara wamejitahidi kujenga kituo hicho na tunampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake pamoja na Mbunge wa Jimbo la Ngara na ahadi yetu ni kwamba katika mwaka ujao vituo vya kumalizia kwa mujibu wa bajeti yetu ni 13, vituo vingine vitaendelea kupangwa kwa kipaumbele

katika bajeti zinazofuata katika miaka ijayo huko mbele. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante; Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu ambapo kila Halmashauri mmeanzisha vituo vya Wilaya lakini vituo hivyo vya wilaya havina vituo vya polisi.

Sasa nataka kufahamu ni lini Serikali itaanzisha ujenzi wa kituo cha polisi nakwakuzingatia kwamba mimi Mbunge wao nipo tayari sasa kutoa tofali 4000 ili tuanze ujenzi huo haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim, Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tumpongeze kwa juhudi zake za kusaidia sekta ya usalama wa raia na mali zao kwa kuchangia idadi hii ya 4,000 ya matofali lakini mpango wetu ni kujenga vituo vya polisi vya Wilaya zile halmashauri ni kuimarisha tu kwa kuweka vituo vingine kwa hivyo kipaumbele kitakuwa kujenga kituo kikuu cha Wilaya ya Kahama na zile Halmashauri zitaendelea kuwekewa vituo visaidizi kwa ngazi ya tarafa na kata kama ambavyo sera yetu ya usalama wa raia inavyoelekeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimesimama kwa hiyo mkae.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu, lakini majibu kutoka Serikalini na sasa nitaleta matangazo na mambo kadhaa niliyonayo hapa mbele; la kwanza kabisa ni tangazo la wageni tutaanza na wageni wangu ambao ni wageni kutoka *Banc ABC* kwanza ni Ndugu Salehe Ramadhani ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Mikopo wa *Banc ABC Tanzania*, karibu sana. *(Makofi)*

Ameongozana na Anna Wesiwasi ambaye ni Meneja wa Tawi la Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Priscus Boniface ambaye ni Meneja Mahusiano Msaidizi Tawi la Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Gilbert Kamugisha ambaye Meneja Mahusiano Makao Makuu Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Dinah Titus ambae ni Afisa Mahusiano Tawi la Dodoma, karibuni sana wageni kutoka wetu kutoka *Banc ABC. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax ambaye ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na hawa ni Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Jenerali Venance Salvatory Mabeyo ambaye ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua kazi nzuri anayoifanya Jenerali Venance Mabeyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ameongozana pia na Luteni Jenerali Methew Edward Mkingule ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yupo pia Meja Jenerali Rajab Nduku Mabele ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Amri Salim Mwami ambaye ni Mkuu wa Tiba Jeshini, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Ibrahim Michael Mhona ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Ramson Godwin Mwaisaka ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Anthony Chacha Sibuti ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Shaban Baraghashi Mani ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Jacob John Mkunda ambaye ni Mkuu wa Tawi la Opereshini na Utendaji Kivita, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko pia Meja Jenerali Salum Haji Othman ambaye ni Kamishna wa Tafiti na Maendeleo ya Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Hawa Issa Kodi ambaye Mkuu wa Tawi la Uhandisi na Lojistiki, karibu sana. *(Makofi/ Vigelegele)*

Yupo Brigedia Jenerali Fadhili Omari Nondo ambaye ni Brigedi Kamanda 101 kundi la Vikosi Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Yuko Brigedia Jenerali Pilly Mohamed Kambenga ambaye Mkurugenzi wa Rasilimali Watu Makao Makuu ya Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Brigedia Jenerali Sorotina Bernard Nshushi ambaye ni Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Bwana Obedi Sayore ambaye ni Kamishna wa Sera na Mipango, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri anao wageni wengine ambaye ni Luteni Jenerali Mstaafu Samuel Ndomba ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Shirika la Mzinga, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali Mstaafu Wynjones Kisamba ambaye ni Mwenyekiti Bodi ya Shirika la *TATC,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Mstaafu Farah Mohamed ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya SUMA JKT, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Charles Mbuge ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kagera, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Brigedia Jenerali Marco Gaguti ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Yupo Kamishna Jenerali wa Zimamoto Mstaafu Thobias Andengenye ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yuko pia Mheshimiwa Adam Malima ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Ali Hapi Mkuu wa Mkoa wa Mara *(Makofi)*

Yuko pia Mheshimiwa John Mongella Mkuu wa Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Salum Kalli ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Magu. *(Makofi)*

Yuko Bwana Agapinus Tax ambaye ni *Risk and Compliance Director Vodacom* Tanzania *PLC* Kaka wa Mheshimiwa Stargomena Tax, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Bwana Exuperius Tax ambaye ni *Investment Associate Frontier Investment Management Africa* ambaye pia ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Profesa Faustine Bee ambaye ni Makamu Mkuu wa Chuo UDOM, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Profesa Emmanuel Mjema ambaye ni Mkuu wa Chuo cha *CBE*, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Padri Onesmo Wissi ambaye ni Paroko, Parokia ya Mtakatifu Paulo wa Msalaba Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Padri Onesmo Shingelwa ambaye ni Paroko, Parokia ya Mtakatifu Petro Claveri Magu na Katibu wa Kamati ya Haki na Amani Wilaya ya Magu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Sheikh Nuhu Zaidi Khamis ambaye ni Sheikh Mkuu wa Wilaya ya Magu na Mwenyekiti wa Kamati ya Haki na Amani Wilaya ya Magu, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia *Mr. Mpangala Renatus Mpangala* huyu hajaandikwa yeye ni nani, lakini na yeye anakaribishwa sana naye ni mgeni wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni pia wa Waheshimiwa Wabunge wengine; kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ni Mwasisi na Mkurugenzi wa Kituo

cha Redio Jamii cha *Buha FM* Sauti ya Kigoma ndugu Prosper Laurent Kwigize, karibu Sana. *(Makofi)*

Wako wageni wawili wa Mheshimiwa Wakili Stephen Byabato ambaye Naibu Waziri wa Nishati na hawa ni wapiga kura wake kutoka Bukoba Mkoani Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Mohamed Suleiman ambao ni wapiga kura wake na pia ni wanafunzi wa Chuo cha Iringa kutoka Mjini Magharibi, Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Amina Hassan ambao ni familia yake kutoka Kusini – Unguja, Zanzibar wakiongozwa na mume wake Ndugu Khamis Fikirini Khamis, karibuni sana. Shemeji ndiyo yupi hapo mume wa Mheshimiwa, karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunao pia wageni 22 wa Mheshimiwa Mohamed Monni ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni wapiga kura wake kutoka Msalala, Mkoani Shinyanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni viongozi wa *Ruaha Academy* kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambao ni wanafunzi wenzake wa *MPA - UDOM* kutoka hapa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza ni wanafunzi 100 na walimu 12 kutoka *Saint Home Primary* ya Dodoma Mjini, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 50 wanaosoma kozi ya saikolojia kutoka Vyuo Vikuu vinne, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Jordan na Chuo Kikuu cha Iringa wakiongozwa na Ndugu Barnabas Mkinga, karibuni sana, sana, sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa wanasoma saikolojia nadhani watatusaidia sana kwenye ile afya ya akili iliyochangiwa sana hapa, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Ninayo matangazo mengine, kwanza Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka juzi Mheshimiwa Husna Sekiboko aliomba mwongozo hapa kuhusu majibu ya swali lake na sasa nitoe mwongozo.

Awali wakati wa kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Sekiboko aliuliza swali la msingi namba 213 kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwamba je, ni hatua gani zinachukuliwa na Wizara kukomesha kuvuja kwa mitihani nchini?

Naibu Waziri wa Wizara hiyo alijibu kwa kuainisha hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kukabiliana na tabia ya udanganyifu katika mitihani ya Taifa ikiwemo mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, sekondari na vyuo. Katika swali la nyongeza Mheshimiwa Sekiboko aliuliza kwamba pamoja na hatua hizo zinazochukuliwa na Serikali bado tatizo hilo linaendelea.

Aliuliza, nanukuu; "Ni vipi Serikali inaenda kukomesha tabia hii?." Waheshimiwa Wabunge katika majibu yake kwa swali hili la nyongeza, Naibu Waziri pamoja na mambo mengine alieleza kuwa, nanukuu; "Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa suala la uvujaji wa mitihani halipo. Mara ya mwisho mitihani ilivuja mwaka 2008 na ulikuwa mtihani mmoja wa somo la hisabati wa kidato cha nne. Kutoka mwaka 2008 hakujawahi kutokea uvujaji wa mitihani.

Mheshimiwa Spika kinachotokea ni udanganyifu katika mitihani kwenye baadhi ya maeneo." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge kutokana na majibu hayo, Mheshimiwa Sekiboko aliomba mwongozo wa Spika na kueleza kuwa Naibu Waziri amejibu kuwa mitihani haikuwahi kuvuja tangu 2008. Lakini Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilipewa kazi na Mheshimiwa Spika ya kujadili taarifa iliyohusu tatizo la kuvuja mitihani mnamo mwezi Agosti na Septemba mwaka jana yaani 2021 ambayo ni mitihani ya vyuo vya afya vya kada ya kati inayosimamiwa na *NACTE.*

Waheshimiwa Wabunge, niliupokea mwongozo huo na kwa kuwa katika majibu ya Naibu Waziri kulikuwa na mambo mawili yalijitokeza ambayo ni udanganyifu kwenye mitihani na kuvuja kwa mitihani. Hivyo nilisema kuwa nitaipitia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuona ni jambo lipi kati ya hayo mawili Kamati ilielekezwa iyafanyie kazi ili niweze kutoa mwongozo huu.

Waheshimiwa Wabunge, nimeipitia taarifa ya Kamati ya tarehe 11 Novemba, 2021 na kubaini yafuatayo:-

Katika Kikao cha Tano cha Bunge kilichofanyika tarehe 8 Novemba, 2021 kilichokuwa kinajadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa, Kiti kiliagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ikutane na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa lengo la kupokea taarifa kuhusu kuvuja kwa mitihani ya vyuo vya afya vya kada ya kati. Kikao hicho kilifanyika siku ya Jumatano, tarehe 10 Novemba, 2021 Bungeni, Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge Kamati ilipokea taarifa iliyowasilishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inayoonesha kulikuwepo na kuvuja kwa mitihani ya utabibu

ngazi ya tano kwa mitihani ya kitaifa iliyofanyika Agosti na Septemba, 2021.

Hivyo kutokana na tatizo hilo, Wizara ilifuta matokeo ya mitihani hiyo na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* ililichukua hatua ya kuelekeza mitihani hiyo irudiwe ndani ya wiki sita kuanzia tarehe 1 Novemba, 2021.

Waheshimiwa Wabunge, vilevile Kamati ilipokea taarifa ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliyoonesha kuwa kulikuwepo na viashiria vya kuvuja kwa mitihani ya muhula wa pili iliyofanyika kitaifa kuanzia tarehe 16 Agosti, 2021 hadi tarehe 30 Septemba, 2021.

Waheshimiwa Wabunge, kikao kati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Wizara hizo kilikuwa na ajenda kuhusu kuvuja kwa mitihani ya vyuo vya afya kada ya kati.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuisoma taarifa hiyo ya Kamati nimejiridhisha kulikuwepo na tatizo la kuvuja mitihani ya kada ya afya inayosimamiwa na *NACTE* kati ya Agosti na Septemba, 2021. *(Makofi)*

Kwa maelezo hayo, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba suala la uvujaji wa mitihani halipo, mara ya mwisho mitihani ilivuja mwaka 2008, hayakuwa majibu sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kujibu maswali umewekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Juni, 2020 ambapo Waziri anayejibu hutakiwa kutoa majibu kwa ukamilifu kama swali lilivyoulizwa.

Kwa hiyo, kwa kuwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Sekiboko halikupata majibu ya kuridhisha, naelekeza kwamba swali hilo lipatiwe majibu sahihi na Waziri. *(Makofi)*

Huo ndio mwongozo wangu kuhusu jambo alilokuwa amesimama Mheshimiwa Husna Sekiboko wakati majibu yalikuwa yametolewa ya swali lake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo lingine tena kwenye hoja ya maswali ambalo limejitokeza jana wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi akijibu maswali mbalimbali ya nyongeza kwenye swali la msingi namba 216 ambalo lilikuwa linahusu ajira za vijana nchini.

Aliulizwa swali na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kuhusu mikopo inayotolewa kwa vijana, kwa maana ya ile mikopo inayotolewa na Halmashauri ile asilimi nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu, majibu yake yaliashiria kana kwamba vijana wote ambao wanauhitaji wa mikopo wanapata mikopo hiyo. *(Makofi)*

Sasa majibu hayo hayana uhalisia na wakati akieleza hivyo, aliendа mbali zaidi na kwa ujumla wake alieleza kwamba Serikali inachukua hatua mbalimbali na akaeleza mambo ambayo Serikali inafanya ili kuhakikisha vijana wanapata ajira, lakini pia vijana wanaweza kujiajiri kwa maana ya alitoa maelezo ya mafunzo ya aina mbalimbali na pia mikopo. *(Makofi)*

Sasa swali lilikuwa linauliza mahsusi kuhusu mikopo na kwamba wapo vijana ambao ile mikopo hawapati, Serikali ina mpango gani kuhusu vijana hao?

Sasa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu hapa yaani akaonesha ishara kwenye majibu yake kwamba vijana wote wenye uhitaji wa mikopo wanapata mikopo na kama wapo ambao hawapati mikopo pengine siyo Watanzania, ni Wakenya. *(Kicheko)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ni lugha ya mazungumzo kwa hiyo, mtu kidogo anakuwa yale majibu si kwamba ameyaandaa kabla kwa sababu ni swali la

nyongeza. Lakini hata hivyo kwa sababu majibu haya hayajapeleka picha nzuri kwa vijana wetu ambao wanahangaika hapa na pale kujaribu kutafuta ajira, lakini pia kutafuta hiyo mikopo ili waweze kuboresha shughuli zao ambazo wamezianzisha na wengine hawajaweza kuanzisha wanatafuta mikopo ili waanzishe hizo shughuli zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, majibu ya namna hii hayakuwa yamejibu swali la Mheshimiwa Mbunge ambaye alitaka kujua wale vijana watasaidiwaje?

Kwa hivyo, hili swali nalo ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ili Mheshimiwa Waziri apate nafasi ya kurekebisha yale majibu yake aliyokuwa ameyatoa awali, swali hili litajibiwa upya hapa Bungeni. *(Makofi)*

Lakini pamoja na kujibiwa upya, maneno hayo yanayoashiria kwamba vijana ambao wamekosa mikopo ni Wakenya si maneno mazuri pamoja na kwamba ni lugha ya mazungumzo, lazima Waheshimiwa Wabunge tunapozungumza humu ndani na Waheshimiwa Mawaziri tuwe na lugha ambayo itapeleka ujumbe mzuri huko nje bila kuwakatisha tamaa vijana wetu ambao wanajishughulisha na mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na haya huwa yanajitokeza na ndio maana huwa siku zote tunasisitiza hapa maswali ya nyongeza yaendane na swali la msingi. Swali la msingi lilikuwa halihusu mikopo, swali la msingi lilikuwa linahusu ajira. Kwa hiyo, kama wote tungejielekeza kwenye kuuliza maswali ya nyongeza yanayohusu ajira, pengine huu mkanganyiko usingejitokeza. Kwa hiyo, tuendelee kujielekeza kwenye maswali ya nyongeza ambayo yanaendana na maswali ya msingi ili tuweze kupata majibu mahsusi kwa maswali tunayoyatoa.

Waheshimiwa Wabunge, mambo mawili ya kukumbushwa hapa nilikuwa nimeshatoa maelekezo kuhusu michango inayotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa

sababu ya hisia ya changamoto za wananchi zilizoko kwenye maeneo yao basi hujisahau na kuweka maneno ya kuashiria kwamba kuna ubaguzi wa mikoa hivi, maendeleo na mambo kama hayo. Nilishalikataza hapa ndani, jana limerejea tena. *(Makofi)*

Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, maelekezo yanavyotoka hapa mbele yanamuhusu Mbunge aliyeyoko Bungeni na ambaye hayupo. Kwa hiyo, likirejea tena jambo ambalo tumeshalikataza hapa mbele, tutachukua hatua kuanzia sasa. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kupita hapa mbele ya Siwa. Wabunge mnatakiwa kutoka sehemu hizi ni hawa wasaidizi wanaruhusiwa kupita kwenye hili eneo ambalo Siwa yetu iko hapo mbele kwa sababu ndiyo Siwa inayoonesha mamlaka yetu sisi kama Wabunge. Kwa hiyo, tunapita huko pembeni, si hapa katikati. Kwa hiyo, hilo nimeona nalo niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya kutoa maelezo hayo, sasa tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wamesimama Wabunge wawili wakiashiria kuna jambo ambalo wanataka kujua na kwamba limetokea hapa ndani, wanataka kujua kama linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Mheshimiwa Waitara.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuomba Mwongozo wa Kiti chako.

Mheshimiwa spika, wakati umenipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwenye swali namba 224 leo asubuhi la

Wizara ya Nishati, nikamuuliza Mheshimiwa Waziri juu ya bei ya umeme hasa wa *REA* ambao unaendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na tumewahi kuzungumza na Mheshimiwa Waziri juu ya jambo la gharama ya umeme wa *REA.* Bahati nzuri wiki iliyopita nilikuwa Jimboni Tarime na nimeongea na Meneja wa *TANESCO* pale Tarime akaniambia amepata maelekezo ya kutoka *TANESCO* kwamba eneo langu, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini hata Halmashauri yangu hata viti vya Madiwani hatujapata, wala jengo la Halmashauri halipo.

Mheshimiwa Spika, lakini wametoa maelekezo kwamba kwa kuwa pale Nyamwaga, Makao Makuu ya Halmashauri kwa sababu kuna Hospitali ya Halmashauri imejengwa na Nyamongo kuna Kituo cha Afya cha Sungusungu, kwa hiyo, hivyo vigezo ni kwamba bei ya umeme imepandishwa kutoka shilingi 27,000 mpaka shilingi 515,000 na mwananchi wangu mmoja na ushahidi ninao hapa ameenda kulipia umeme anaeneo lake pale Nyamwaga, ana nyumba analipia umeme anahitaji nguzo tatu. Kwa hiyo, akapigiwa mahesabu kwamba kila nguzo moja ni shilingi 515,000 piga mara tatu hiyo ndiyo gharama aliyopewa. Kwa hiyo, yule mwananchi akalazimika kurudi kutafuta umeme kwenye eneo lake, anasubiri labda kama kutakuwa na huruma ya Mheshimiwa Rais ama Serikali ili bei ishushwe.

Mheshimiwa Spika, ndio maana nikauliza, nini kauli ya Serikali? Bei ambayo tumeelezwa hapa na majibu ya Naibu Waziri ni kwamba vijijini bei ni shilingi 27,000 na jambo hili ni nchi nzima najua kwenye Majimbo yote ya Vijijini bei imetangazwa ni zaidi ya shilingi 27,000. Naibu Waziri amejibu gharama shilingi 27,000 hali halisi kijijini kule ambako hajaenda, gharama yake wameelekezwa ni 515,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 53(4) kama itakupendeza swali hili lipate

majibu sahihi ili waende *site* kule, awasiliane na Wabunge aone kama kweli bei aliyoitangaza hapa Bungeni ndiyo bei ambayo wananchi wetu wanapewa kule kulipia umeme kwenye majumba yao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimesimama kwa Kanuni ya 76.

Wakati majibu yanatolewa katika maswali ya leo, swali namba 225 la Wizara ya Ujenzi ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Massare lilijibiwa vizuri, lakini Mheshimiwa Massare aliuliza swali la nyongeza kuhusu barabara inayounganisha Mkoa wa Simiyu na Mkoa wa Singida na Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa majibu kwamba barabara ile imeshamaliza upembuzi yakinifu na Daraja la Sibiti limejengwa na bajeti inayoanza barabara ile itajengwa kwa vipande.

Mheshimiwa Spika, lakini palepale ukampa Mheshimiwa Aysharose Mattembe nafasi ya swali la nyongeza akauliza kuhusu barabara hiyo hiyo na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ikawa ni tofauti kabisa kwamba barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu.

Sasa naomba nipate Mwongozo wako kuhusu majibu haya ya Serikali ukizingatia kwamba Bunge hili ni Bunge *live* na wananchi wa Mkalama wanahamu na barabara hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Mwita Waitara akiomba Mwongozo na tunaongozwa na Kanuni yetu ya 76 ambayo inasema utaomba Mwongozo kwa kuashiria kwamba kama hilo jambo

ambalo limefanyika hapa ndani linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Kwa hiyo, yeye amesimama hapa akitaka Mwongozo juu ya majibu yaliyotolewa na hali halisi inayoendelea kule. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Mwita Waitara aliuliza swali la nyongeza, siyo swali la msingi na katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwa mujibu wa taratibu ambazo wanazo wao na *TANESCO* na maelekezo waliyowapa wale wakandarasi wanaotoa hizo huduma huko vijijini.

Kwa hiyo, kama kuna hali ya tofauti kwa Jimbo hili mahsusi la Tarime Vijijini basi wewe utawafuata watu wa Wizara, lakini majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yako sawasawa kwenye hoja hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Francis Mtinga akieleza kuhusu swali ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Yahaya Massare na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Lakini pia na swali la nyongeza ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Aysharose Mattembe na kwamba Mheshimiwa Francis Mtinga yeye alivyokuwa anasikiliza ameelewa kwamba majibu yaliyotolewa kwa maswali yanayofanana majibu ni tofauti kwa hilo swali namba 225.

Sasa hapa ulishawahi kutolewa mwongozo kwamba yule aliyeuliza swali kama anaona majibu hayajatoka kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 53 ndiye anayetakiwa kusimama kutoa hayo maelezo. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Francis Mtinga pamoja na kwamba anasema barabara hii inamhusu, lakini wale waliojibiwa maswali hawajaomba Mwongozo, kwa hiyo wameridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Fungu 57 - Wizara, Fungu 38 - Ngome, Fungu 39 - JKT na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda nitawasilisha kwa muhtasari hivyo naomba hotuba yangu ya bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2022/2023 isomeke na kuchukuliwa yote kama nilivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana wakati nchi yetu ikiwa katika hali ya amani na usalama. Aidha, kwa unyenyekevu mkubwa namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumwahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa uwezo wangu wote. Pia

namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kumuamini Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na Jenerali Venance Salvatory Mabeho kuwa Mkuu wa Majeshi ambao wameendelea kunipa ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa jitihada mahsusi ambazo zimeliwezesha Taifa letu kuendelea kuwa na amani na mshikamano. Vilevile, napenda kuwashukuru Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao makini, na kwa maelekezo na miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuongoza Mhimili wa Bunge. *(Makofi)*

Vilevile nampongeza aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Napenda pia kumshukuru sana na kwa dhati kwa  uongozi wake thabiti na miongozo aliyotupatia wakati akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya NUU. Miongozo hiyo iliwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa tija na ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa maarifa, hekima, busara na nguvu ili muendelee kuliongoza vyema Bunge letu tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, na namshukuru kwa ushirikiano

mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza kwa dhati waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioaminiwa na kuteuliwa kuziongoza Wizara mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nawapongeza Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Ushetu, Mheshimiwa Emmanuel Lekisho Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumpongeza Luteni Jenerali Mathew Edward Mkingule kwa kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi. Aidha, napenda kuwapongeza Meja Jenerali Anthony Chacha Sibuti kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenerali Shaban Barghashi Mani kuwa Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, *Rear Admiral* Ramson Godwin Mwaisaka kuwa Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji na Brigedia Jenerali Idd Said Nkambi kuwa Mkuu wa Kamandi ya Vikosi chini ya Makao Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako Mheshimiwa Spika na Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, mtangulizi wangu Hayati Elias John Kwandikwa, na aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro Hayati William Tate Ole Nasha na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Rukwa, Marehemu Irene Alex Ndyamkama.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole pia Mheshimiwa dada yetu mpendwa Anna Lupembe kwa kuondokewa na binti yake mpendwa Irene, naomba nitoe pole vilevile kwa familia, ndugu na jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na wapendwa wao. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema, peponi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa akisaidiana na Wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri wanaoendelea kutupatia, maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati, vimesaidia kuboresha mapendekezo ya makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ninayowasilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; katika kikao kilichofanyika tarehe 29 Machi, 2022 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kamati ilitoa maoni, ushauri, na maelekezo kwa Wizara yaliyolenga kuboresha utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu.

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa maoni, ushauri, na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa wakati wa kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 ninayowasilisha.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Dira ya Taifa 2025 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 katika utekelezaji wa mpango na bajeti; katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kwa masuala yaliyoainishwa katika Sura ya Tano Ibara ya 105 ya Ilani utekelezaji wake

umeeleweshwa katika aya ya 11 (a) mpaka (j) ya hotuba hii ninayoiwasilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 makadirio na makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 85,103,000 kutoka katika mafungu yake matatu; Fungu 38 - Ngome, shilingi 22,000,000, Fungu 39 - JKT, shilingi 61,903,000 na Fungu 57 - Wizara shilingi 1,200,000.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 120,558,848.50 ikiwa sawa na asilimia 141.66 ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38 - Ngome yamekusanywa Maduhuli yenye jumla ya shilingi 43,191,408.

Mheshimiwa Spika, Fungu 39 - JKT limekusanya shilingi 61,900,000; Fungu 57 - Wizara imekusanya shilingi 15,467,440.50 mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa kwenye katika Jedwali Na. 1. la hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,358,694,986,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya maendeleo katika mafungu yake matatu Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo shilingi 2,182,116,562,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 176,778,424,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Fungu 38 - Ngome limeidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida shilingi 1,779,475,285,000 na fedha za maendeleo shilingi 32,578,424,000; Fungu 39 - JKT limeidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida shilingi 382,474,955,000 na fedha za maendeleo shilingi bilioni 4.

Mheshimiwa Spika, Fungu 57 - Wizara limeidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida shilingi 20,166,322,000 na fedha

za maendeleo shilingi bilioni 140. Muhtasari na mchanganuo wa bajeti kwa kila Fungu umeainishwa katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni ,hilingi 1,929,384,355,845.61 sawa na asilimia 81.8 ya bajeti iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo shilingi 1,798,774,637,752.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,306,067,180,102.56 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Katika kiasi hiki Fungu 38 limepokea fedha za matumizi ya kawaida shilingi 1,477,45706,363.96 na fedha za maendeleo shilingi 32,504,52178.52.

Mheshimiwa Spika, Fungu 39 - JKT limepokea fedha za matumizi ya kawaida shilingi 307,109,843,712.78 na fedha za maendeleo shilingi 3,272,048,797 na Fungu 57 - Wizara imepokea fedha za matumizi ya kawaida shilingi 14,619,087,675.31 na fedha za maendeleo shilingi 94,383,617,127.04 Mhutasari na mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika jedwali Na. 3.

Mheshimiwa Spika, fedha za matumizi ya kawaida zimeweza kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kijeshi, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, mafunzo ya Jeshi la Akiba, huduma za afya na tiba, ushiriki wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika shughuli za ulinzi wa amani huko Lebanon, *DRC*, Sudani ya Kusini na Afrika ya Kati pia zimetumika katika diplomasia ya ulinzi na ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine, ushirikiano na mamlaka za kiraia, mapambano dhidi ya magonjwa ambukizi na yasiyoambukiza, utawala bora na utunzaji wa mazingira. Maelezo ya kina yanapatikana katika aya ya 17 mpaka aya 32 ya hotuba.

Mheshimiwa Spika, matumizi katika shughuli za maendeleo; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imeweza kutumia fedha za maendeleo kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Ununuzi wa zana za vifaa;

(b) Uhuishwaji na uboreshaji wa zana za ulinzi wa anga, matengenezo na matunzo ya zana za kiopareshehi za nchi kavu na majini;

(c) Ujenzi wa mahanga ya kuhifadhia helkopta;

(d) Kugharimia matunzo ya mkataba wa matunzo ya helkopta;

(e) Kugharimia ujenzi wa maghala ya kuhifadhia zana na vifaa;

(f) Kuboresha miundombinu ya huduma za afya na makazi;

(g) Kugharimia miradi ya mawasiliano salama jeshini;

(h) Kutatua migogoro ya ardhi kwa kupima na kufanya uthamini pamoja na kulipa fidia kwa wananchi katika maeneo matano ambayo ni Kaboya, Muleba - Mkoa wa Kagera, Nyamisangula Mkoa wa Mara, Mitwero Mkoa wa Lindi Nyangungulu, Ilemela Mkoa wa Mwanza na Usule Mkoa wa Tabora.

(i) Fedha hizo zimetumika kwenye ujenzi wa maabara katika Shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga na Karakana katika Shule ya Anga;

(j) Ununuzi wa zana za kilimo za Jeshi la Kujenga Taifa; na

(k) Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa Kikombo, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani imeanza ujenzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi Msalato, Dodoma hospitali hii itakuwa na adhi ya daraja la nne, aidha Wizara

kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China kupitia Jeshi la Ukombozi la watu China *(PLA)* imekamilisha ujenzi wa jengo la mafunzo ya utawala katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi *(NDC).* Jengo hili limeanza kutumika baada ya kuzinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu hapo tarehe 14 Novemba, 2021 na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia JKT imefanikiwa pia kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani miradi hiyo ni kama inavyooneshwa katika aya ya 35 (a) mpaka (j) ya hotuba.

Mheshimiwa Spika, mashirika yanayosimamiwa na Wizara; nianze na *Tanzania Automotive Technology Centre* (*TATC)* ambalo linajulikana zaidi kama Nyumbu. Hadi kufikia Aprili, 2022 *TATC* imepokea kiasi cha shilingi 8,974,278,587.25 kati ya kiasi cha shilingi bilioni tisa zilizotengwa hii ikiwa ni sawa na asilimia 99.7 na hii ni sehemu ya fedha za maendeleo zilizopokelewa na Wizara, na shirika limeweza kutekeleza shughuli za maendeleo zifuatazo; ununuzi wa mitambo kwa ajili ya kupima ubora wa chuma na maabara na kwa kuhakiki ubora wa bidhaa zinazozalishwa na ujenzi wa jengo la kusimika mitambo ya kuzalisha bidhaa za chuma zisizoshika kutu.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa mitambo hii ni hatua kubwa itakayoliwezesha Shirika la *TATC* kukidhi mahitaji ya ndani na kutumia fursa za masoko nje ya Tanzania. Katika kipindi husika *TATC* imetekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani kama ilivyoainishwa katika aya ya 40 (a) mpaka (e) ya hotuba.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Mzinga limepokea kiasi cha shilingi 5,465,210,662.68 kati ya shilingi bilioni 5.5 zilizotengwa hii ikiwa ni sawa na asilimia 99.3 na ikiwa ni sehemu ya fedha za maendeleo zilizopokelewa na Wizara. Kwa fedha hizi shirika limeweza kutekeleza shughuli za maendeleo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ununuzi na

ukarabati wa mitambo na uzalishaji wa zao la msingi vipuli na zana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli za msingi shirika limeendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha za ndani kama ilivyoainishwa katika aya ya 42(a) mpaka (d) ya hotuba.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la JKT; SUMA JKT kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani imeendelea na shughuli za uzalishaji mali kupitia kampuni tanzu na viwanda vyake ili kuipunguzia Serikali gharama za malezi ya vijana wanaojiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Shughuli hizo zinatekelezwa kupitia sekta ya ujenzi, viwanda na biashara, kilimo, mifugo, na ulinzi kama zilivyoainishwa katika aya ya 43 (a) mpaka (e) ya hotuba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha zilizotolewa kwa Wizara katika kutekeleza Mpango wa Bajeti wa mwaka wa fedha 2021/2022, naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kutoa uzito mkubwa katika shughuli za ulinzi ikiwa ni pamoja na kutoa nyongeza ya fedha kiasi cha shilingi 87,910,623,094.47 kwa ajili ya kugharamia operesheni maalum, ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa – Kikombo, ulipaji wa madeni, ununuzi wa kitambaa cha vazi la medani, ununuzi wa magari ya makamanda Waambata Jeshi na Utawala na kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma waliopandishwa vyeo na madaraja.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi; hali ya mipaka ya nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilometa 5,461.20 ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji, imeendelea kuwa shwari. Katika kipindi hiki cha mwaka ninaotolea taarifa hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina yetu na nchi tunazopakana nazo, changamoto kadhaa zilizojitokeza zimeendelea kushughulikiwa kwa njia ya amani na makubaliano.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu hali ya ulinzi na usalama ya mipaka ya nchi yetu kwa kila mpaka kwa nchi tunazopakana nazo ni kama ilivyoainishwa katika aya ya 47 hadi aya ya 56 ya hotuba ninayoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na maombi ya fedha; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelenga kutekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia Dira na Dhima ya Wizara, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026), Malengo ya Maendeleo Endelevu yaani *SDGs* 2030, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Mwongozo wa Maandalizi na Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makadirio ya makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 87,603,000 kutoka katika mafungu yake matatu ambayo Fungu 38 - Ngome linalotarajiwa kukusanya kiasi cha shilingi 22,000,000; Fungu 39 - JKT linatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 64,403,000; na Fungu 57 - Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 1,200,000 kama inavyoonekana katika jedwali Na. 4.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida na maendeleo; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ikiwa ni jumla ya shilingi 2,713,787,405,453 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 2,483,454,234,453 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 230,333,171,000 ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Fungu 38 - Ngome

linatarajia kutengewa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida shilingi 2,047,723,503,453 na fedha za maendeleo shilingi 56,367,636,000; Fungu 39 -JKT linatarajia kutengewa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida shilingi 411,863,641,000 na fedha za maendeleo shilingi 13,965,535,000; Fungu 57 - Wizara inatarajiwa kutengewa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida shilingi 23,867,090,000 na fedha za maendeleo shilingi 160,000,000,000 kama ilivyoainishwa katika jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Spika, shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ni pamoja na :

(a) Kuimarisha Jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, mawasiliano pamoja na rasilimali watu;

(b) Kuendelea kuweka na kuboresha na mazingira ya utendaji kazi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ikiwemo mafunzo, matunzo ya zana na miundombinu;

(c) Kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi kwa kuboresha miundombinu na kuwezesha kujitosheleza kwa chakula na kuchangia katika usalama wa chakula wa Taifa;

(d) Kuendeleza kutatua changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;

(e)Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;

(f) Kulipa malipo ya posho kwa wanajeshi, mishahara na stahili kwa watumishi wa umma;

(g) Kuimarisha na kuratibu mafunzo ya Jeshi la Akiba;

(h) Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa *(UN),* Umoja wa Afrika *(AU),* Jumuiya za Kikanda, na Nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi;

(i) Kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura;

(j) Kutatua migogoro ya ardhi kwa kupima mipaka ya maeneo ya Jeshi, kufanya uthamini, na kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa.

Mheshimiwa Spika, shukrani; kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa michango yao madhubuti katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 na kutayarisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwa ni pamoja na Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Jenerali Venance Salvatory Mabeyo - Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; Luteni Jenerali Mathew Edward Mkingule - Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Meja Jenerali Rajab Nduku Mabele - Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wakuu wa Matawi - Makao Makuu ya Jeshi, Wakuu wa Idara - Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa, Maafisa, askari na watumishi wa umma waliopo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Nawashukuru sana kwa moyo wa kujituma na kazi kubwa wanayoifanya katika kulinda Taifa letu na kulijenga Taifa letu na kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kufanikisha majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kutoa shukrani kwa Serikali za nchi mbalimbali na washirika wa maendeleo kwa ushikirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara yangu ikiwa ni pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Canada, India, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Ufaransa, Ujerumani na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za ulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Algeria, Bangladeshi, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, Indonesia, Israel, Jordan, Misri, Morocco, Nigeria, Oman,

Pakistani, Sri Lanka, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Urusi na Uswisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru familia yangu kwa kuendelea kuniombea kwa upendo na ushirikiano na uvumilivu wao kwangu unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga la Taifa ambayo ni www.modans.go.tz

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. STERGOMENA LAWRENCE TAX (MB.), WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A: UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Fungu 57 : Wizara, Fungu 38 : NGOME, na Fungu 39 : JKT

pamoja na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana, wakati nchi yetu ikiwa katika hali ya amani na usalama. Aidha, kwa unyenyekevu namshukuru kwa dhati **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Pia, namshukuru kwa kuendelea kumuamini **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe** kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

***3. Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, nampongeza **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa jitihada mahsusi ambazo zimeliwezesha Taifa letu kuendelea kuwa na amani na mshikamano. Vile vile, napenda kuwashukuru **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao makini, na kwa maelekezo na miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

***4. Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi **Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)**, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuongoza Mhimili wa Bunge. Vile vile, nampongeza aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nampongeza pia kwa uongozi wake thabiti na miongozo aliyotupatia akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya NUU. Miongozo iliwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa tija na ufanisi. Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa maarifa, hekima, busara na nguvu ili muendelee kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Aidha, nampongeza **Mhe. Vita Rashid Kawawa (Mb.)** kwa kuteuliwa

kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

***5. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza kwa dhati waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioaminiwa na kuteuliwa kuziongoza Wizara mbalimbali katika Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, nawapongeza **Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, na **Mhe. Shamsi Vuai Nahodha** kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***6. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, **Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)**, Spika wa Bunge hili, **Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.)**, Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa mafanikio makubwa.

***7. Mheshimiwa Spika,*** naomba kumpongeza **Luteni Jenerali Mathew Edward Mkingule,** kwa kuteuliwa kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi. Aidha, napenda kuwapongeza **Meja Jenerali Anthony Chacha Sibuti,** kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, **Meja Jenerali Shaban Barghashi Mani,** kuwa Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, **Rear Admiral Ramson Godwin Mwaisaka,** kuwa Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, na **Brigedia Jenerali Idd Said Nkambi** kuwa Mkuu wa Kamandi ya Vikosi Chini ya Makao Makuu ya Jeshi.

***8. Mheshimiwa Spika,*** ninaungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako Mhe. Spika na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, **Hayati Elias John Kwandikwa**, aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro **Hayati William Tate Ole Nasha** na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa, **Marehemu Irene Alex Ndyamkama**. Naomba kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa, na watanzania wote kwa kuondokewa na

wapendwa hao. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema, peponi.

***9. Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na **Mhe. Vita Rashid Kawawa (Mb.)** akisaidiana na wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri wanaoendelea kutupatia, na kwa maandalizi ya bajeti hii. Maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati wakati wakichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, na mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, vimesaidia kuboresha mapendekezo ya makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ninayowasilisha leo hapa bungeni.

## B: UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

***10. Mheshimiwa Spika,*** katika kikao kilichofanyika tarehe 29 Machi, 2022 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipitia na kujadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kamati ilitoa maoni, ushauri, na maelekezo kwa Wizara yaliyolenga kuboresha utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri, na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 ninayowasilisha leo hapa bungeni.

## C: UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2020 NA DIRA YA TAIFA 2025 KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

***11. Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa mpango na bajeti katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 kwa masuala yaliyoainishwa katika **Sura ya Tano** Ibara ya 105 ya Ilani ambayo ni:

*a. "Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake ili kudumisha Muungano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, umoja, mshikamano, amani na usalama wa raia na mali zao;*

*b. Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;*

*c. Kuwezesha ushirikiano wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kufanya utafiti na ubunifu kwa kushirikiana na taasisi za utafiti;*

*d. Kuhusisha kikamilifu Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati;*

*e. Kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Akiba na ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;*

*f. Kuimarisha uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kushiriki shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda katika sekta ya ulinzi na maeneo mengine ya kimkakati;*

*g. Kuimarisha viwanda vya NYUMBU na Mzinga ili viweze kutimiza azma ya kuanzishwa kwake;*

*h. Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi;*

*i. Kupanua na kuongeza idadi ya kambi za JKT na JKU ili kuwezesha vijana wengi zaidi wakiwemo wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya mafunzo ili kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea; na*

*j. Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia makazi bora na kuongezea uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama*

*kwa kuvipatia mafunzo ya kitaaluma na kitaalam, vitendea kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa;*

**D: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

***12. Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 85,103,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu; Fungu 38 : NGOME, **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39 : JKT, **Shilingi 61,903,000.00** na Fungu 57 : Wizara **Shilingi 1,200,000.00**.

***13. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili 2022 Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 120,558,848.50** sawa na **asilimia 141.66** ya makadirio. Kwa upande wa Fungu 38 : NGOME, yamekusanywa maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 43,191,408.00** sawa na **asilimia 196.32** ya makadirio, yanayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, na malipo ya kamisheni zinazotokana na makato ya bima kwa wanajeshi kutoka makampuni mbalimbali ya bima. Fungu 39 : JKT limekusanya **Shilingi 61,900,000.00** sawa na **asilimia 99.99** ya makadirio, zilizotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mauzo ya mazao ya bustani (mboga mboga na matunda), bidhaa za mifugo, nafaka na bidhaa zitokanazo na ufugaji wa nyuki. Fungu 57 : Wizara, imekusanya **Shilingi 15,467,440.50** sawa na **asilimia 1,288.95** ya makadirio**,** zilizotokana na huduma ya Mtandao wa Mawasiliano Salama na mapato ya *Ulinzi Channel* iliyopo kwenye mtandao wa *YouTube*. Muhtasari wa mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1**.

***Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mchanganuo wa Makusanyo ya Maduhuli Kuanzia Julai, 2021 hadi Aprili 2022***

| Na. | Fungu | Makadirio ya Mapato 2021/2022 | Makusanyo Julai 2021 hadi Aprili, 2022 | Makusanyo (%) |
|---|---|---|---|---|
| | 38 - NGOME | 22,000,000.00 | 43,191,408.00 | 196.32 |
| | 39 – JKT | 61,903,000.00 | 61,900,000.00 | 99.99 |
| | 57 – Wizara | 1,200,000.00 | 15,467,440.50 | 1,288.95 |
| **Jumla** | | **85,103,000.00** | **120,558,848.50** | **141.66** |

***14. Mheshimiwa Spika*, **katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,358,694,986,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake matatu: Fungu 38 : NGOME, Fungu 39 : JKT na Fungu 57 : Wizara. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,182,116,562,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **Shilingi 176,578,424,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika kiasi hiki; Fungu 38 : NGOME limeidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 1,779,475,285,000.00,** na fedha za maendeleo **Shilingi 32,578,424,000.00**, Fungu 39 : JKT limeidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 382,474,955,000.00,** na fedha za maendeleo **Shilingi 4,000,000,000.00**, Fungu 57 : Wizara limeidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 20,166,322,000.00,** na fedha za maendeleo **Shilingi 140,000,000,000.00**. Muhtasari wa Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 2.**

***Jedwali Na. 2: Muhtasari wa Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022***

| Na. | Fungu | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 38 - NGOME | 1,779,475,285,000.00 | 32,578,424,000.00 | 1,812,053,709,000.00 |
| 2 | 39 - JKT | 382,474,955,000.00 | 4,000,000,000.00 | 386,474,955,000.00 |
| 3 | 57 - Wizara | 20,166,322,000.00 | 140,000,000,000.00 | 160,166,322,000.00 |
| | **Jumla** | **2,182,116,562,000.00** | **176,578,424,000.00** | **2,358,694,986,000.00** |

***15. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2022 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni **Shilingi 1,929,384,355,854.61** sawa na **asilimia 81.80** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,798,774,637,752.05** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **Shilingi 130,609,718,102.56** ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Katika kiasi hiki; Fungu 38 : NGOME limepokea fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 1,477,045,706,363.96,** na fedha za maendeleo **Shilingi 32,504,052,178.52**; Fungu 39 : JKT

limepokea fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 307,109,843,712.78,** na fedha za maendeleo **Shilingi 3,272,048,797.00**; na Fungu 57 : Wizara limepokeaa fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 14,619,087,675.31,** na fedha za maendeleo **Shilingi 94,833,617,127.04**. Muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika **Jedwali Na. 3**

***Jedwali Na. 3: Muhtasari wa Mchanganuo wa Fedha Zilizopokelewa Kuanzia Julai, 2021 hadi Aprili, 2022***

| Na. | Fungu | Matumizi Yaliyoidhinishwa | Bajeti ya Mwaka 2021/2022 | Kiasi Kilichopokelewa Hadi Aprili, 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 38 - NGOME | Malipo na Posho (Pay and Allowance) | 1,457,024,047,000.00 | 1,211,840,186,673.43 | 83.17 |
| | | Chakula naPosho ya Chakula | 219,284,700,000.00 | 182,737,250,000.00 | 83.33 |
| | | Matumizi Mengineyo | 41,086,938,000.00 | 33,577,569,690.53 | 81.72 |
| | | Misamaha yakodi | 62,079,600,000.00 | 48,890,700,000.00 | 78.75 |
| | | Maendeleo | 32,578,424,000.00 | 32,504,052,178.52 | 99.77 |
| | | **Jumla ya Fungu** | **1,812,053,709,000.00** | **1,509,549,758,542.48** | 83.31 |
| 2 | 39 - JKT | Malipo na Posho (Pay and Allowance) | 253,578,848,000.00 | 207,153,323,435.00 | 81.69 |
| | | Chakula na Posho ya Chakula | 60,150,270,000.00 | 47,768,858,500.00 | 79.42 |
| | | Matumizi Mengineyo | 35,376,602,524.00 | 27,738,009,701.78 | 78.41 |
| | | Mafunzo ya Vijana wa Mujibu wa Sheria | 21,636,234,476.00 | 16,349,652,076.00 | 75.57 |
| | | Posho ya Msamaha wa kodi | 11,733,000,000.00 | 8,100,000,000.00 | 69.04 |
| | | Maendeleo | 4,000,000,000.00 | 3,272,048,797.00 | 81.80 |
| | | **Jumla ya Fungu** | **386,474,955,000.00** | **310,381,892,509.78** | **80.31** |

| Na. | Fungu | Matumizi Yaliyoidhinishwa | Bajeti ya Mwaka 2021/2022 | Kiasi Kilichopokelewa Hadi Aprili, 2022 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | 57 - Wizara | Mishahara (Wizara na Mashirika) | 10,221,977,000.00 | 7,081,687,000.00 | 69.28 |
| | | Ruzuku (Mashirika na Majenerali) | 6,874,634,814.00 | 4,893,672,862.99 | 71.18 |
| | | Matumizi Mengineyo | 3,069,710,186.00 | 2,643,727,812.32 | 86.12 |
| | | Maendeleo | 140,000,000,000.00 | 94,833,617,127.04 | 67.74 |
| | | **Jumla ya Fungu** | **160,166,322,000.00** | **109,452,704,802.35** | **68.34** |
| **JUMLA KUU** | | | **2,358,694,986,000.00** | **1,929,384,355,854.61** | **81.80** |

***Fedha za Matumizi ya Kawaida***

***16. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kwa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida, Wizara imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na: mafunzo ya kijeshi, mafunzo ya Jeshi la Akiba, huduma za afya na tiba, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine, ushirikiano na mamlaka za kiraia katika shughuli mbalimbali za kitaifa, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, mapambano dhidi ya magonjwa ambukizi na yasiyoambukiza, utawala bora na utunzaji wa mazingira.

***Mafunzo ya Kijeshi***

***17. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi katika shule na vyuo vya kijeshi ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya kuwapatia wanajeshi mafunzo ya awali, na kuwaendeleza katika taaluma mbalimbali za uongozi. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara imeendelea kuratibu na kuendesha mazoezi na mafunzo. Katika kipindi husika, JWTZ ilifanikiwa kufanya zoezi la pamoja liitwalo '*Joint Combined Exchange Training'* (JCET) ambalo lilifanyika kuanzia tarehe 28 Julai 2021 hadi tarehe 10 Septemba 2021 kwa ushirikiano na Jeshi la Marekani. Zoezi hili lilifanyika Kunduchi Mkoa wa Dar es Salaam, likiwa na lengo la kuimarisha uwezo wa kukabiliana na matishio ya kigaidi nchini na nchi tunazopakana nazo.

***18. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kupanga, kuratibu na kusimamia mafunzo ya Maafisa na Askari nje ya nchi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya Maafisa na Askari 490 wanahudhuria mafunzo nje ya nchi.

***Mafunzo ya Jeshi la Akiba***

***19. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba kwa wananchi katika ngazi ya awali.

Mafunzo hayo hufanyika katika mikoa yote ya Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Aprili 2022, jumla ya wananchi walioandikishwa na kuhitimu mafunzo hayo ni **12,510**, kati yao wanaume **10,750** na wanawake **1,760.** Vile vile, JWTZ kupitia kamati za usalama za Mikoa na Wilaya, imeendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya Ulinzi na Usalama.

***Huduma za Afya na Tiba***

***20. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi husika, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa huduma za tiba kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma, familia za wanajeshi, na wananchi wanaoishi karibu na vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Katika kuboresha huduma hizo, juhudi mbalimbali zimefanyika ikiwemo: kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, huduma ya usafishaji wa Figo katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo (GMH), kuboresha huduma katika Hospitali za Kanda na vituo vya tiba vikosini, na utoaji wa huduma za Bima ya Afya Jeshini.

***Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine***

***21. Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeendelea kushirikiana na nchi rafiki katika masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali, ikiwemo mafunzo, misaada ya kitaalamu, zana na vifaa. Vile vile, JWTZ inashirikiana na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) katika mafunzo na ubadilishanaji wa wataalamu. Pia, JWTZ inaendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kutoa mafunzo kwa Maafisa na Askari. Nchi hizo ni pamoja na Algeria, Bangladeshi, Canada, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israeli, Jamhuri ya Watu wa China, Jordani, Marekani, Misri, Morocco, Nigeria, Omani, Pakistani, Sri Lanka, Sweden,Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, na Uswisi.

***22. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) imeendelea kutoa mafunzo ya Usalama na Stratejia kwa Maafisa wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, pamoja na Viongozi katika Utumishi wa Umma kuanzia ngazi

ya Wakurugenzi Wasaidizi. Aidha, katika kipindi husika, Chuo kimetoa mafunzo hayo kwa washiriki kutoka nchi za Afrika Kusini, Bangladeshi, Botswana, Burundi, China, Kenya, Malawi, Misri, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Rwanda, Uganda, Zambia, na Zimbabwe.

***Ushiriki wa JWTZ katika Shughuli za Ulinzi wa Amani***

***23. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa. Hadi sasa, Kikosi kimoja na Vikundi vidogo vidogo vipo mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, chini ya Misheni ya Umoja wa Mataifa (The United Nations Organization Stabilization Mission in the Democratic Republic of the Congo–MONUSCO). Kikosi kingine kipo Jamhuri ya Afrika ya Kati, chini ya Misheni ya Umoja wa Mataifa (United Nations Multi dimensional Integrated Stabilization Mission in the Central African Republic - MINUSCA), na Kombania mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanon (United Nations Interim Force in Lebanon - UNIFIL). Aidha, JWTZ linashiriki operesheni ya kupambana na ugaidi nchini Msumbiji (SADC Mission in Mozambique - SAMIM). Vile vile, Jeshi lina Maafisa wanadhimu na Makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani nchini Sudan, Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ushiriki wa JWTZ katika operesheni za Ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Mataifa umeiwezesha nchi yetu kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa na Jumuiya za Kikanda wa kushiriki katika ulinzi wa amani kimataifa na kikanda. Vile vile, ushiriki huu unaendeleza Diplomasia ya Kijeshi (Military Diplomacy), na unasaidia JWTZ kupanua uwezo kwa kufanya kazi na Nchi nyingine.

***Ushirikiano na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali za Kitaifa***

***24. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali ikiwemo, kutoa misaada wakati wa majanga na maafa, kushiriki katika utekelezaji na ulinzi wa miradi ya kimkakati ikiwa ni

pamoja na Reli ya Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway), Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP), Mgodi wa *Tanzanite*, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), na maeneo ya Viwanja vya Ndege.

***Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa***

***25. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JKT imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Katika kipindi husika mafunzo kwa Vijana wa Mujibu wa Sheria na Kujitolea yamefanyika kwenye Kambi mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa kupitia **Operesheni Samia Suluhu** ambapo jumla ya vijana **25,503** wa Mujibu wa Sheria wamepatiwa mafunzo na kati yao **19,544** ni wa kiume na **5,959** ni wa kike. Aidha, vijana **11,739** wa Kujitolea wamepatiwa mafunzo na kati yao **8,165** ni wa kiume na **3,574** ni wa kike.

***26. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa watanzania kwamba, dhumuni la mafunzo yanayotolewa kwa vijana ni kuwapatia stadi za kazi na stadi za maisha ili baada ya kumaliza muda wa mafunzo na kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa, waweze kurejea majumbani kwao wakiwa raia wema wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa. Nitoe rai kwa vijana wote wanaopata fursa za kupata mafunzo hayo kuzitumia stadi za kazi walizozipata kujiajiri na kujitegemea.

***Mapambano Dhidi ya Magonjwa Ambukizi na Yasiyoambukiza***

***27. Mheshimiwa Spika,*** katika kupambana na Virusi vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini, Ugonjwa wa Upungufu wa Kinga Mwilini, na Magonjwa yasiyoambukiza, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI, magonjwa yasiyoambukiza pamoja, na UVIKO – 19. Wizara imeunda kamati inayoshughulikia masuala ya VVU, UKIMWI na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ili kutoa elimu ya kujikinga na magonjwa hayo. Aidha, Wizara imeunda

kamati ya UVIKO – 19, ili kuhamasisha na kutoa elimu kwa watumishi namna ya kujikinga na UVIKO – 19. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe kwa watumishi wenye maambukizi ya VVU. Hatua hizi zinachukuliwa kwa kuzingatia mwongozo wa udhibiti VVU na UKIMWI. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imetoa elimu na kuhamasisha upimaji wa hiari, na uchangiaji damu.

***Utawala Bora***

***28. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara pamoja na Taasisi zake imechukua jitihada mbalimbali ili kuimarisha Utawala Bora. Taasisi hizi zimekuwa zikiandaa taarifa za kila Robo Mwaka ambazo huwasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Vile vile, Semina mbalimbali kwa watumishi, kuhusu jinsi ya kupambana na kuzuia rushwa mahala pa kazi zimeendelea kutolewa. Aidha, Wizara imekuwa ikishirikisha watumishi katika kutoa maoni na ushauri kupitia vikao mbalimbali, hususan Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya Maadili, Bodi ya Manunuzi, na Kamati ya Ajira. Juhudi hizi zimelenga kuimarisha dhana ya Utawala Bora kwa Wizara na Taasisi zake.

***Utunzaji wa Mazingira***

***29. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za utunzaji wa mazingira, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara kupitia Taasisi zake imeendelea na utunzaji wa mazingira katika maeneo yake yenye miti ya asili, kuyalinda maeneo hayo yasivamiwe kwa shughuli za kijamii na kuendelea kupanda miti mipya. Vile vile, Wizara imeendelea na utunzaji wa fukwe katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi. Aidha, maeneo yote ya Jeshi yana zuio la ukataji miti, kuchoma mkaa, na kulisha mifugo. Napenda nitoe wito kwa wananchi wote kuzingatia zuio hili na kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

***30. Mheshimiwa Spika,*** katika dhana hii ya utunzaji wa mazingira Wizara imefanikiwa kupanda miti **147,724** katika

maeneo mbalimbali ikiwemo katika kambi za JWTZ, JKT na Shirika la Mzinga. Baadhi ya miti hiyo imepandwa pembezoni mwa kingo kuzunguka Bwawa la Mindu, kwa ushirikiano kati ya Shirika la Mzinga na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Morogoro Water Supply and Sanitation Authority – MORUWASA). Pia, Kikosi cha Mzinga hufanya doria kwenye eneo hilo ambalo ni chanzo kikubwa cha maji katika Mkoa wa Morogoro kuhakikisha mazingira yake yanaendelea kuwa salama.

***31. Mheshimiwa Spika,*** mashirika yaliyo chini ya Wizara ambayo ni *Tanzania Automotive Technology Centre* (TATC), MZINGA na SUMAJKT yameendelea na uzalishaji kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na njia za kisasa za kutibu maji yenye kemikali yanayotoka viwandani. Vile vile, viwanda vimeendelea na utaratibu wa kuwapa wafanyakazi wake vifaa kinga vyenye mfumo wa kudhibiti sauti ili kuzuia kelele.

***32. Mheshimiwa Spika,*** kama wote tunavyoelewa Jeshi letu linamiliki maeneo ya kimkakati katika mikoa mbalimbali nchini, na maeneo haya yametengwa maalum kwa matumizi ya kijeshi. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kutoa rai na kuwaasa wananchi kutovamia maeneo ya Jeshi kwa ajili ya makazi au kuendesha shughuli zao za kila siku, kwani kufanya hivyo ni kuhatarisha usalama na maisha yao kutokana na uhalisia wa shughuli za kijeshi zinazofanyika katika maeneo hayo ikiwemo mafunzo na mazoezi mbalimbali ambayo yanatumia risasi za moto na milipuko. Aidha, kwa kufanya uvamizi katika maeneo hayo, ni kuhatarisha usalama wa Taifa, na kukwamisha baadhi ya shughuli muhimu za kuliweka tayari Jeshi letu kukabiliana na matishio yeyote yanayoweza kujitokeza. Uvamizi huo hupelekea pia migogoro ya ardhi isiyo ya lazima.

***Matumizi ya Fedha za Maendeleo***

***33. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara imeweza kutumia fedha za maendeleo kutekeleza shughuli zifuatazo :

a. Ununuzi wa zana, vifaa, risasi na mabomu;

b. Uhuishaji na uboreshaji wa zana za ulinzi wa anga, matengenezo na matunzo ya zana za kiooperesheni za nchi kavu, na kwenye maji;

c. Ujenzi wa mahanga ya kuhifadhia helikopta katika mikoa ya Dodoma na Geita;

d. Kugharamia mkataba wa matunzo ya helikopta;

e. Kugharamia ujenzi wa maghala ya kuhifadhi zana na vifaa katika mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga, Ruvuma na Mwanza;

f. Kuboresha miundombinu ya majengo katika Hospitali ya Jeshi ya Kanda – Mwanza ambapo *VIP ward*, chumba cha kuhifadhia maiti, na Bweni la Askari Kapera wa kike yamejengwa;

g. Kugharamia Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini;

h. Kutatua migogoro ya ardhi kwa kupima na kufanya uthamini pamoja na kulipa fidia kwa wananchi wa maeneo matano (5), eneo la Kaboya - Muleba Mkoa wa Kagera, Nyamisangura Mkoa wa Mara, Mitwero Mkoa wa Lindi, Nyangunguru - Ilemela Mkoa wa Mwanza, na Usule Mkoa wa Tabora;

i. Ujenzi wa Maabara katika Shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga, umaliziaji wa ujenzi wa Karakana katika Shule ya Anga ya Kijeshi – Tanga;

j. Kugharamia ununuzi wa magari kwa ajili ya Makamanda, Waambata Jeshi na shughuli za utawala;

k. Kugharamia ununuzi wa zana za kilimo za JKT;

l. Kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika mradi wa ujenzi wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC);

m. Mafunzo, ufuatiliaji na tathmini ya miradi;

n. Kununua magari mawili ya usimamizi wa miradi; na vifaa vya upimaji wa ardhi;

o. Kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu ya JKT; na

p. Kuendeleza ukarabati wa miundombinu na usambazaji wa maji katika vikosi.

***34. Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia *German Armed Forces Technical Advisory Group* (GAFTAG) imeanza ujenzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi, Msalato – Dodoma. Hospitali hii itakuwa na hadhi ya Daraja la Nne (Level IV Hospital). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Jeshi la Ukombozi la Watu wa China (PLA) imekamilisha ujenzi wa Jengo la Mafunzo na Utawala katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC). Jengo hili limeanza kutumika baada ya kuzinduliwa na **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu tarehe 14 Novemba, 2021.

***35. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JKT imefanikiwa pia kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia rasilimali za ndani ifuatavyo:

a. Ujenzi wa miundombinu ya Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Kikosi cha Chita Mkoa wa Morogoro;

b. Kilimo cha Chikichi (Migazi) katika Kikosi cha Bulombora Mkoa wa Kigoma;

c. Kilimo cha Mkonge katika vikosi vya Maramba na Mgambo Mkoa wa Tanga;

d. Kilimo cha kahawa katika vikosi vya Itende Mkoa wa Mbeya na Rwamkoma Mkoa wa Mara;

e. Kilimo cha Korosho katika vikosi vya Nachingwea, Makutopora, Ruvu na Kibiti katika mikoa ya Lindi, Singida na

Pwani mtawalia. Aidha, shamba la Korosho la Kikosi cha Ruvu limepewa hadhi ya kuwa shamba darasa Mkoa wa Pwani;

f. Ufugaji wa Samaki katika vikosi vya Rwamkoma Mkoa wa Mara, Chita Mkoa wa Morogoro, na Ruvu Mkoa wa Pwani; na

g. Ufugaji wa nyuki katika vikosi vya Msange Mkoa wa Tabora, Kanembwa na Mtabila Mkoa wa Kigoma.

***36. Mheshimiwa Spika,*** shamba la Korosho katika Kikosi cha Kibiti limezinduliwa tarehe 02 Mei, 2022 na Kiongozi wa mbio za Mwenge kama shamba Darasa litakalotumika kutoa mafunzo kwa wakulima wa Wilaya ya Kibiti na maeneo jirani.

***37. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Shirika la TATC, Shirika la MZINGA na SUMAJKT imeendelea kutekeleza majukumu yake ifuatavyo;

***Tanzania Automotive Technology Centre (TATC) - NYUMBU***

***38. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2022, TATC imepokea kiasi cha fedha **Shilingi 8,974,278,587.25** kati ya **Shilingi 9,000,000,000.00** sawa na **asilimia 99.71** ikiwa ni sehemu ya Fedha za maendeleo zilizopokelewa na Wizara, na kuweza kutekeleza shughuli za maendeleo zifuatazo:

a. Ununuzi wa mitambo kwa ajili ya kupima ubora wa chuma katika kitengo cha kukalibu chuma na maabara ya kuhakiki ubora wa bidhaa zinazozalishwa; na

b. Ujenzi wa jengo la kusimika mitambo ya kuzalisha bidhaa za chuma zisizoshika kutu (metal galvanizing plant).

***39. Mheshimiwa Spika,*** ununuzi wa mitambo hii ni hatua kubwa itakayoliwezesha Shirika la TATC kukidhi mahitaji ya ndani na kutumia fursa za masoko nje ya Tanzania.

***40. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, TATC imetekeleza shughuli zifuatazo kwa kutumia rasilimali za ndani:

a. Kukamilisha ukarabati wa magari ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, na kuendelea na uundaji wa magari mapya ya kuzimia moto ya kiwango cha Manispaa;

b. Utengenezaji wa vifaa kwa ajili ya matumizi ya JWTZ ikiwemo; vitanda vya chuma na *mobile field kitchen*;

c. Utengenezaji wa vipuri mbalimbali (*domestic flour milling machine, briquette rollers, brake blocks, hot plate holes* na *scrap crusher);*

d. Ukarabati wa pampu za maji za Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma; na

e. Ukarabati wa *incinerator* za Hospitali ya Rufaa ya Tumbi mkoani Pwani na Temeke mkoani Dar es Salaam.

***Shirika la MZINGA***

***41. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mzinga limepokea kiasi cha **Shilingi 5,465,210,622.68** kati ya **Shilingi 5,500,000,000.00** sawa na **asilimia 99.37** ikiwa ni sehemu ya Fedha za maendeleo zilizopokelewa na Wizara, na kuweza kutekeleza shughuli za maendeleo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na;

a. ununuzi na ukarabati wa mitambo,

b. uzalishaji wa zao la msingi, vipuri na zana.

***42. Mheshimiwa Spika***, pamoja na shughuli za msingi, Shirika limeendelea na utekelezaji wa shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha za ndani ifuatavyo:

a. Ukarabati wa silaha kutoka katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama;

b. Uzalishaji wa vipuri kwa ajili ya mashine za uzalishaji wa zao la msingi;

c. Uzalishaji wa mabomu ya kufukuzia wanyama ambayo yanatumiwa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, pamoja na Halmashauri zinazopakana na Hifadhi hizo;

d. Ununuzi na uuzaji wa milipuko na silaha ndogo;

e. Kusimamia na kutunza zana na silaha zinazomilikiwa na makampuni yanayofanya ulinzi katika meli zinazotia nanga kwenye bandari zilizopo nchini;

f. Utengenezaji wa samani za aina mbalimbali;

g. Kupitia Kampuni Tanzu ya *Mzinga Holding Company Limited*, Shirika linaendelea na ukamilishwaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi, ikiwemo Ofisi za Serikali; na

h. Ujenzi na ukarabati wa majengo ya hospitali ya Mzinga na Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Mzinga.

***Shirika la Uzalishaji Mali la JKT***

***43. Mheshimiwa Spika*,** SUMAJKT kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani imeendelea na shughuli za uzalishaji mali kupitia kampuni tanzu na viwanda vyake, ili kuipunguzia Serikali gharama za malezi ya Vijana wanaojiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Shughuli hizo zinatekelezwa kupitia sekta ya ujenzi, viwanda na biashara, kilimo, mifugo, na ulinzi ifuatavyo:

a. Miradi ya Ujenzi ya Serikali ikiwemo: majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi zilizopo Mji wa Serikali – Mtumba mkoani Dodoma; ujenzi wa Maabara ya Sayansi katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine – Morogoro; ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji, na Makao Makuu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa iliyopo mkoani Dodoma; kusawazisha eneo la mradi wa ujenzi wa Hanga la Helikopta uliopo Chato mkoani Geita na ujenzi wa Maabara ya Shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga iliyopo mkoani Tanga;

b. Ujenzi wa miundombinu na usambazaji wa umeme vijijini katika mikoa ya Morogoro na Shinyanga, kufunga

(installation) umeme katika Ofisi za Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Singida, Shule ya Mfano Mkoa wa Dodoma, na Ofisi ya Rais (Ikulu) Chamwino;

c. Kuimarisha viwanda vyake ikiwemo: Kiwanda cha Samani - Chang'ombe; Kiwanda cha kuzalisha maji ya kunywa ya *Uhuru Peak*; Kiwanda cha Ushonaji; Kiwanda cha Kuchakata Nafaka – Mlale JKT;

d. Ulinzi wa Taasisi za Umma na binafsi katika mikoa mbalimbali; na

e. Shughuli za kilimo katika shamba lililopo Mngeta, Mkoa wa Morogoro.

***44. Mheshimiwa Spika*****,** pamoja na fedha zilizotolewa kwa Wizara katika kutekeleza Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2021/2022, naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kutoa uzito katika shughuli za ulinzi, ikiwa ni pamoja na kutoa fedha nje ya Bajeti kiasi cha **Shilingi 87,910,623,094.47** kwa ajili ya kugharamia operesheni maalum, ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (MMUT – Kikombo), ununuzi wa kitambaa cha vazi la medani (Kombati), kulipa madeni ya maji na umeme, na kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma waliopanda vyeo na madaraja.

## E: HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

***45. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, hali ya mipaka ya nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilomita **5,461.20,** ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji, imeendelea kuwa shwari. Mipaka hiyo ni baina ya Tanzania na Msumbiji, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Katika kipindi hicho hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina yetu na nchi tunazopakana nazo, licha ya kuwepo changamoto kadhaa.

***46. Mheshimiwa Spika,*** naomba nielezee hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo ifuatavyo;

***Mpaka wa Tanzania na Msumbiji***

***47. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu ni ya wastani kutokana na mashambulizi yanayofanywa na kundi la kigaidi la **Ansar Al Sunna Wal Jamaah (AASWJ)** maeneo ya Kaskazini mwa Msumbiji, katika Jimbo la Cabo Delgado linalopakana na Mkoa wa Mtwara. Kundi hilo limekuwa likiathiri usalama kwa kuharibu na kupora mali za wananchi. Katika kupambana na changamoto hii, JWTZ imeendelea kuimarisha ulinzi kwa kufanya operesheni za ndani ya nchi na kukabiliana na kundi hilo. Aidha, JWTZ inashiriki operesheni chini ya Mwamvuli wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika nchini Msumbiji (SADC Mission in Mozambique - SAMIM) katika jitihada za kudhibiti ugaidi. Operesheni hizi zimeendelea kuimarisha ulinzi katika eneo la Mpaka, kudumisha amani na utulivu.

***48. Mheshimiwa Spika,*** operesheni zimesaidia kupunguza nguvu ya kundi hilo la kigaidi. Hata hivyo, kundi hilo linatekeleza mashambulizi kwa kuhamahama na kubadili mbinu za kimapigano. Licha ya hali hiyo, vikundi vyetu vinaendelea kupambana kuhakikisha kundi hilo halileti madhara zaidi. Wizara inaishukuru Serikali na hususan **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kutoa kipaumbele katika kupambana na suala hili, na kutoa fedha kwa ajili ya mahitaji mbalimbali yanayosaidia vikundi vya ulinzi kupambana na kundi hilo.

***Mpaka wa Tanzania na Malawi***

***49. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama ya mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama lililoripotiwa. Ushirikiano uliopo baina ya Jeshi letu na Jeshi la Malawi ni mzuri. Hali hiyo inajidhihirisha kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo, ambayo yamepelekea kufanyika michezo ya kirafiki kati ya timu za majeshi ya nchi hizi mbili yaliyofanyika Brigedi ya Kusini mwezi Julai 2021. Changamoto ya mpaka katika

Ziwa Nyasa inaendelea kufanyiwa kazi kupitia Tume Maalum ya Usuluhishi (High Level Mediation Team) iliyoundwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Aidha, Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala hilo.

***Mpaka wa Tanzania na Zambia***

**50. *Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa nchi yetu lililoripotiwa hadi sasa.

***Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo***

**51. *Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama kwa nchi yetu. Hata hivyo, ndani ya nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo yameripotiwa matukio ya waasi kushambulia miji mbalimbali nchini humo. Wizara kupitia JWTZ imeendelea kuwa macho na kujipanga wakati wote. Aidha, ushiriki wa Tanzania katika Misheni ya Umoja wa Mataifa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (United Nations Organisation Stabilization Mission in the Democratic Republic of the Congo - MONUSCO) unaisaidia nchi kujiimarisha kiulinzi ipasavyo.

***Mpaka wa Tanzania na Burundi***

**52. *Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu ni shwari. Hakuna matukio yoyote yaliyoripotiwa kuhatarisha usalama baina ya nchi hizi, ingawa eneo hili linakabiliwa na uwepo wa wahamiaji haramu, uvamizi wa wakulima na uingizaji wa mifugo kwa ajili ya kupata malisho. JWTZ imeendelea kukabiliana na hali hii.

***Mpaka wa Tanzania na Rwanda***

**53. *Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu ni shwari, ingawa yapo matukio machache ya kihalifu ya wahamiaji haramu na uingizaji wa mifugo kwa ajili ya malisho. Wizara

kupitia JWTZ inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti matukio hayo.

***Mpaka wa Tanzania na Uganda***

***54. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama katika mpaka huu ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama wa nchi yetu. Hata hivyo, kuna changamoto ya uingizaji haramu wa mifugo kwa ajili ya malisho. Juhudi za kuimarisha mpaka zinaendelea, kwa kuongeza *Beacon* kati ya marundo ya mawe yaliyowekwa na mkoloni, na kujenga barabara ya usalama kwenye Mpaka.

***Mpaka wa Tanzania na Kenya***

***55. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu, ni shwari. Hakuna tukio la kuhatarisha usalama dhidi ya Tanzania lililoripotiwa. Hata hivyo, ipo changamoto ya kuharibiwa kwa alama za mpaka. Kazi ya kuimarisha Mpaka huu inayotekelezwa na timu ya wataalam kutoka Tanzania na Kenya inaendelea vizuri, ambapo awamu ya kwanza imeanzia eneo la Serengeti hadi Ziwa Natron.

***Mpaka wa Tanzania Katika Bahari ya Hindi***

***56. Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka huu, ni shwari. Katika Mpaka huu tumepakana na nchi za Comoro na Shelisheli. Hakuna tukio lililoripotiwa la kuhatarisha usalama dhidi ya Tanzania. Aidha, JWTZ imeendelea kufanya doria za mara kwa mara katika eneo la Bahari ya Hindi, ili kubaini na kuzuia wahamiaji haramu, usafirishaji haramu wa binadamu, usafirishaji wa madawa ya kulevya na matishio ya kigaidi.

**F: MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

***57. Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelenga kutekeleza mpango na bajeti kwa kuzingatia mambo yafuatayo; Dira na Dhima ya Wizara, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030

(SDGs), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

***58. Mheshimiwa Spika,*** naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ifuatavyo:

***Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli***

***59. Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu, ambapo Fungu 38 : NGOME linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 22,000,000.00,** Fungu 39 : JKT linatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 64,403,000.00** na Fungu 57 : Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 1,200,000.00** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4.**

***Jedwali Na 4: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023***

| Na. | Fungu | Makadirio ya Maduhuli 2022/23 |
|---|---|---|
| 1 | 38 – NGOME | 22,000,000.00 |
| 2 | 39 – JKT | 64,403,000.00 |
| 3 | 57 – Wizara | 1,200,000.00 |
| **Jumla** | | **87,603,000.00** |

***Matumizi ya Kawaida na Maendeleo***

***60. Mheshimiwa Spika*****,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ikiwa na jumla ya **Shilingi 2,713,787,405,453.00** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,483,454,234,453.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **Shilingi 230,333,171,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu ni ifuatavyo; Fungu 38 : NGOME linatarajia kutengewa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 2,047,723,503,453.00,**

na fedha za maendeleo **Shilingi 56,367,636,000.00**; Fungu 39 : JKT linatarajia kutengewa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 411,863,641,000.00,** na fedha za maendeleo **Shilingi 13,965,535,000.00**; na Fungu 57 : Wizara inatarajiwa kutengewa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 23,867,090,000.00,** na fedha za maendeleo **Shilingi 160,000,000,000.00** kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 5.**

***Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Bajeti kwa Kila Fungu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023***

| Na | Fungu | Matumizi ya Kawaida | Matumizi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 38-NGOME | 2,047,723,503,453.00 | 56,367,636,000.00 | 2,104,091,139,453.00 |
| 2 | 39-JKT | 411,863,641,000.00 | 13,965,535,000.00 | 425,829,176,000.00 |
| 3 | 57-Wizara | 23,867,090,000.00 | 160,000,000,000.00 | 183,867,090,000.00 |
| **Jumla** | | **2,483,454,234,453.00** | **230,333,171,000.00** | **2,713,787,405,453.00** |

***61. Mheshimiwa Spika,*** shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 utazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

a. Kuendelea kuliimarisha Jeshi kwa zana na vifaa vya kisasa, mawasiliano pamoja na rasilimali watu;

b. Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi wa Jeshi ikiwemo mafunzo, matunzo ya zana na miundombinu, maslahi, huduma bora za afya, ofisi na makazi;

c. Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;

d. Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;

e. Kuendelea kulipa malipo na posho kwa wanajeshi, mishahara na stahili kwa watumishi wa umma;

f. Kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi

na kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, na stadi za kazi kwa vijana;

g. Kuendelea kujenga uwezo wa JKT ili kuiwezesha kujitosheleza kwa chakula kwa vijana wanaojiunga na mafunzo;

h. Kuendelea kuimarisha na kuratibu mafunzo ya Jeshi la Akiba kwa kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama, na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi wa nchi;

i. Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa (UN), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya za Kikanda, na Nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi;

j. Kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura itapohitajika; na

k. Kuendelea kutatua migogoro ya ardhi kwa kupima mipaka ya maeneo ya Jeshi, kufanya uthamini, na kulipa fidia ya ardhi iliyotwaliwa kutoka kwa wananchi kwa matumizi ya Jeshi.

## G: SHUKRANI

***62. Mheshimiwa Spika,*** kabla sijahitimisha Hotuba yangu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa michango yao madhubuti katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022, na kutayarisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu ya Mwaka wa Fedha 2022/ 2023 ifuatavyo: **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe,** Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Jenerali Venance Salvatory Mabeyo,** Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, **Luteni Jenerali Mathew Edward Mkingule,** Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, **Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele,** Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo (Wizara ya Ulinzi na JKT), Wakuu wa Matawi (Makao Makuu ya Jeshi), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma waliopo Wizara

ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nawashukuru sana kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kufanikisha majukumu ya Wizara.

***63. Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa Serikali za nchi mbalimbali na washirika wa maendeleo kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia Wizara yangu, ikiwa ni pamoja na; Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Canada, India, Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Ufaransa, Ujerumani na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za Ulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Algeria, Bangladeshi, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, Indonesia, Israeli, Jordani, Misri, Morocco, Nigeria, Omani, Pakistani, Sri Lanka, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Urusi, na Uswisi.

***64. Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.

***65. Mheshimiwa Spika,*** napenda kuishukuru familia yangu kwa upendo na uvumilivu wao kwangu unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu.

***66. Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni ***www.modans.go.tz***

***67. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Nitamuita sasa Mwenyekiti wetu wa

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Fungu 38, 39 na 57 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadario ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, utangulizi kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu sita, ya kwanza ikiwa ni sehemu ya utangulizi; sehemu hiyo inatoa maelezo ya jumla kuhusu msingi na muundo wa taarifa; sehemu ya pili inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na sehemu ya tatu hadi ya nne zinachambua utekelezaji wa mipango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na kuchanganua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano inaonesha maoni na ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi. Aidha, sehemu ya sita na ya mwisho inakamilisha taarifa kwa kutoa shukurani na kulishauri Bunge kuhusu hoja hii ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, msingi wa uchambuzi wa Kamati; kifungu cha 6(3) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha

7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimeipa Kamati hii jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii na makadirio ya mapato na matumizi yake kuchambuliwa na Kamati hii kabla ya kujadiliwa Bungeni. Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, masharti hayo yamezingatiwa na sasa, naliomba Bunge liijadili hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya taarifa; taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi yaliyochambuliwa inagusa mafungu matatu ya kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 38 - Ngome, Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kujua yaliyojitokeza wakati wa uchambuzi, naomba kuisoma taarifa hii kwa muhtasari. Hata hivyo, kwa umuhimu wa kumbukumbu kamili, naomba taarifa yote kama ilivyowasilishwa mezani mapema leo hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo; Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Kuendeleza Utafiti katika Shirika la Nyumbu na Mradi wa kuendeleza uzalishaji katika Shirika la Mzinga. Aidha, Kamati ilikagua mradi wa ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji - Chita pamoja na ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi, Kikombo; miradi hiyo ipo Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma. Ili kulisaidia Bunge kufuatilia uchambuzi, naomba kutoa muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa. Aidha, nitasoma kwa kifupi sehemu ya taarifa inayohusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa; Shirika la Nyumbu lilitengewa kiasi cha shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kuendeleza utafiti. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022, Kamati ilipofanya ziara mradi huu ulikuwa umepokea kiasi cha shilingi 8,952,541,837.25 ikiwa ni zaidi ya asilimia 97 ya fedha iliyotengwa. Kwa upande wa

mradi wa kuendeleza uzalishaji katika Shirika la Mzinga, jumla ya shilingi 5,500,000,000 zilitengwa kwa ajili hiyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 fedha iliyopatikana ni asilimia 98 ya kiasi kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa linatekeleza Mradi wa Kilimo cha Mpunga kwenye shamba la ekari 12,000 eneo la Chita. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mradi huu ulianza kwa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji sambamba na mpango wa kuanza kulima ekari 2,500.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu, ilijulishwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kilikuwa kimetumika kuimarisha miundombinu. Mahitaji halisi yaliyobainika ni pamoja na kiasi cha shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu. Aidha, ili kusawazisha sura ya eneo la mradi la ekari 2,500, kiasi cha shilingi bilioni 6.2 kinahitajika. Kwa hali hiyo kuna upungufu wa jumla ya jumla ya shilingi bilioni 9.5.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine uliokaguliwa unahusu ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi katika eneo la Kikombo, Mkoani Dodoma. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2020 na unatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba, 2022. Ujenzi unaendelea kwa utaratibu wa *Force Account* na unakadiriwa kukamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 58.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi baada ya muhtasari huo wa maelezo hayo, naomba kulijulisha Bunge kwamba Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa majukumu ya Mashirika ya NYUMBU na MZINGA unakabiliwa na changamoto zinazoendelea kufanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi.

(ii) Uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Chita unakabiliwa na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji pamoja na gharama nyingine za kilimo; na Uhaba za wa zana na mitambo ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia shamba.

(iii) Iwapo ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi usingetumia utaratibu wa *Force Account*, ungegharimu kiasi cha shilingi bilioni 127 badala ya shilingi bilioni 58 ambayo ni gharama ya sasa. Kwa msingi huo, utaratibu wa utekelezaji wa mradi huu umeokoa kiasi cha shilingi bilioni 69. Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa hadi wakati Kamati ilipotembelea mradi huu, ni asilimia 41.5

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022; kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Mpango wa Maendeleo wa miaka kumi (2020/2021-2029/2030) kwa Shirika la NYUMBU ukitekelezwa kwa ukamilifu wake, itapatikana tija na Manufaa ya kuanzishwa kwa Shirika hili inavyostahili.

(ii) Serikali ikiendelea na juhudi zake za kulisaidia Shirika la MZINGA katika utatuzi wa changamoto za kifedha na kibajeti, Shirika hilo litafanikiwa na kutoa mchango mkubwa katika kufanikisha majukumu ya Wizara hii.

(iii) Utekelezaji wa Mradi wa Kilimo – Chita ukiendelea kuungwa mkono na kupewa kipaumbele na Serikali, utaongeza uhakika wa usalama wa chakula nchini. Hali hiyo inasaidia kukabiliana na changamoto inayoikumba dunia kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame.

(iv) Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi, Kikombo kwa utaratibu wa kutumia *Force Account* umeokoa zaidi ya shilingi bilioni 69. Ikiwa utaratibu huu utatumika kwa uadilifi, Serikali itaokoa fedha nyingi hasa katika miradi ya majengo ya kimkakati. Ni rai ya Kamati kuwa taasisi nyingi za Serikali zitahitaji kujifunza namna Jeshi linavyotumia utaratibu huo kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka

wa fedha 2021/2022; uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ulilenga kulinganisha makusanyo ya mapato na lengo la makusanyo hayo. Aidha, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa na upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ulilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa. Naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato; katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yalikuwa sawa sawa na makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Februari, 2022 makusanyo yalikuwa ni asilimia asilimia 103.03. Ukusanyaji huu ni ongezeko la asilimia 15.23 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

(ii) Ulinganisho wa mchango wa mafungu ya Wizara katika makusanyo, unaonesha kuwa Fungu 38 - Ngome limechangia asilimia 142 ya lengo, Fungu 39 - JKT limechangia asilimia 87 na Fungu 57 - Wizara limechangia asilimia 165 ya lengo kama inavyoonekana katika jedwali namba 01 na grafu namba 01 ya taarifa.

(iii) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 25.85 lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa asilimia 142.75.

(iv) Makusanyo ya Fungu 39 - JKT yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 72.74, lakini katika hali halisi Fungu hilo limechangia kwa asilimia 87.70

Mheshimiwa Spika, kwa ulinganisho huo, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa makusanyo ni mzuri hadi kufikia Februari, 2022 unaridhisha. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa

kuna umuhimu mkubwa wa kupanga lengo la makusanyo kwa kuzingatia uhalisia. Aidha, Upangaji wa lengo la makusanyo uendane na usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; Kamati ilifanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge na fedha zilizopatikana ili kujiridhisha na uzito uliowekwa kwa majukumu ya yaliyopangwa kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti za mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekanaka katika Jedwali Na. 02 na 03 la taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea asilimia 54.04 ya fedha zilizoidhinishwa.

(ii) Asilimia 93.04 ya fedha zilizopokelewa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 6.96 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Wakati wa makadirio, asilimia 92.5 ni matumizi ya kawaida na asilimia 7.49 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(iii) Wakati wa kupitisha bajeti ya Wizara hii uwiano wa bajeti za mafungu matatu ulionesha kuwa Fungu 38 yaani Ngome lilikuwa na asilimia 76.82 ya bajeti ya Wizara; Fungu 39 yaani JKT asilimia 16.39 na Fungu 57 yaani Wizara asilimia 6.79. Hata hivyo katika utekelezaji Fungu 38 - Ngome limepokea asilimia 74.81 ya kiasi kilichotarajiwa, Fungu 39 - JKT asilimia 19.77 na Fungu 57 - Wizara asilimia 5.42.

(iv) Kiasi kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni pungufu ya asilimia 8.20 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa katika kipindi kama hiko kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huo unaonesha jinsi Serikali ilivyozingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti. Kwa mwenendo huu Kamati inaipongeza Serikali kutoa uzito stahiki kwa bajeti ya Ngome, Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara. Hata hivyo Kamati inasisitiza umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii kulingana na ratiba ya utekelezaji wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapitio ya uzingatiaji wa ushauri wa Kamati; wakati wa kuchambua Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ilitoa ushauri katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara hii.

Naomba kuliarifu Bunge kuwa taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri kama inavyoonekana katika kiambatisho namba moja cha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri kama ilivyoripotiwa, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali mathalani ushauri kuhusu Serikali kutoa fedha zote zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi ni jambo linalohitaji kuzingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023; moja, mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kamati ilipitia majukumu Makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yakiidhinishwa na bajeti hiyo kupatikana yatasaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Wizara hii. Makadirio hayo yatawezesha ufikiaji malengo sita ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023; kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu yaani 38, 39 na 57 inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 87,603,000 kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 2.9 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 39 - JKT ambako lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia nne.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza lengo la makadirio kwa fungu hilo hususan kwa kuzingatia kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Fungu 39 - JKT lilikuwa limeshakusanya asilimia 87.7 ya makadirio yaliyowekwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wa lengo hilo la makusanyo na sura ya mchanganuo wake inaonekana katika jedwali namba nne na chati namba tatu ya taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la makusanyo kwa mafungu yote ya Wizara hii limeongezeka kwa asilimia 2.9 ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha unaoisha.

(ii) Fungu 38 - Ngome linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha asilimia 25 kama ilivyokuwa mwaka wa fedha 2021/2022.

(iii) Fungu 39 - JKT linategemewa katika Makusanyo kwa asilimia 75 lakini kwa mwaka 2021/2022 lilitegemewa kwa asilimia 72.7.

(iv) Fungu 57 - Wizara linategemewa katika makusanyo kwa asilimia moja wakati mwaka 2021/2022 lilitegemewa kwa asilimia 1.4. Hata hivyo, kiasi hicho cha makadirio ya makusanyo kwa Fungu 57 kinalingana na makadirio ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 limejumuisha asilimia 91.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 8.49 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa makadirio hayo, umebainisha mambo yafuatayo: -

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imeongezeka kwa asilimia 15. Kwa ongezeko hilo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake wa mara kwa mara wa kuongeza kiwango cha bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia.

(ii) Kiasi cha fedha kilichoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kimeongezeka kwa asilimia 30.4 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Fedha hizi zimeongezeka katika Fungu 38 ambalo limepata ongezeko asilimia 73, Fungu 39 limepata ongezeko asilimia 249.14 na Fungu 57 ambalo limepata ongezeko la asilimia 14.29.

(iii) Gharama za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zimeganywa kwa Fungu 38 - Ngome linalotengewa asilimia 24.47, Fungu 39 - JKT linalotengewa asilimia 6.06 na Fungu 57 - Wizara linalotengenewa asilimia 69.46.

Mheshimiwa Spika, naomba matokeo hayo ya uchambuzi yalisaidie Bunge kujadili makadirio haya ya mapato na matumizi kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; maoni, kwa kuzingatia uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri wake. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(i) Upungufu wa watumishi katika Mashirika ya MZINGA na NYUMBU usipoendelea kufanyiwa kazi na Serikali, utaathiri utekelezaji wa majukumu ya mashirika hayo na kupunguza tija iliyokusudiwa.

(ii) Kuwezesha inavyostahili utekelezaji wa Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji katika eneo la Chita, ni jambo la kimkakati litakaloongeza uhakika na upatikanaji wa chakula.

(iii) Kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi ni jambo linalochangia kufanikisha azma ya Serikali kuboresha makazi ya wanajeshi. Aidha, mahitaji ya kibajeti kwa ajili ya ukarabati yanafaa kutimizwa inavyotakiwa.

(iv) Mantiki ya Msajili wa Hazina kukabidhi shamba la Mngeta yaani *Killimajaro Plantation Ltd.* lenye ukubwa wa ekari 14,545 kwa SUMA JKT, inaweza kupatikana iwapo changamoto za uchakavu wa mitambo, miundombinu na ukosefu wa mtaji kwa SUMA JKT zitatatuliwa.

(v) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati ya Bunge kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa kwa kipindi tofauti umefikia hatua ya kuhitaji kuwekwa katika utekelezaji. Aidha, kupokewa kwa maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wengine muhimu kama ilivyoripotiwa katika Kamati, ni jambo la maana iwapo utekelezaji utaanza.

(vi) Juhudi za Serikali kuimarisha mipaka yetu ili kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zinastahili kuendelezwa. Aidha, ili kuendelea kudhibiti mianya hiyo ya mipaka inayoweza kutumiwa isivyostahili, Serikali inapaswa kuboresha uratibu wa jambo hili.

(vii) Kukosekana kwa hati za maeneo yanayomilikiwa na Wizara ya Ulinzi ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kutumia maeneo hayo na baadaye kuibuka kwa migogoro ya umiliki.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati; kwa maoni hayo, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 57 yaani Wizara kwa mtiririko uliopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za

maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 38 yaani Ngome na Fungu 39 yaani JKT ili kutoathiri utekelezaji wake.

(ii) Jeshi la Wananchi liandae na kutekeleza mkakati wa muda mrefu wa kupeleka askari wenye utaalamu unaohitajika katika Mashirika ya NYUMBU na MZINGA. Kufanya hivyo itapunguza upungufu wa rasilimali watu kwa lengo kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi hiyo ilikuwa ni kengele ya pili, nakuongezea dakika tatu.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Stagomena Tax kwa ushirikiano wake kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Faraji Mnyepe pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo na wakisaidiwa na Bi.

Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu lipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT, kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi huo ulifanyika tarehe 29 Machi, 2022 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Ulinzi na JKT inajumuisha Mafungu Matatu (3) ya Kibajeti yafuatayo: -

i) Fungu 38- Ngome;
ii) Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa; na
iii) Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Wizara).

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne (4) zifuatazo: -

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Kuendeleza utafiti katika Shirika la NYUMBU, kuendeleza uzalishaji katika shirika la MZINGA. Aidha, kamati pia ilitembelea mradi wa ukarabati

miundombinu ya umwagiliaji Chita pamoja na ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi Kikombo. Miradi hiyo ipo Mikoa ya Pwani, Morogoro na Dodoma mtawalia. Maeneo yaliyotembelewa ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili:
a) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizo ziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu maeneo yaliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

#### 2.1.1 Kuendeleza utafiti katika Shirika la NYUMBU- Kibaha

Shirika la NYUMBU lilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 9** kwa ajili ya kuendeleza utafiti katika Shirika hilo. Hadi Kamati inafanya ziara Shirika hilo lilikuwa limepokea kiasi cha **Shilingi 8, 952,541,837.25** ikiwa ni zaidi ya asilimia 97 ya fedha iliyotengwa. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo zimetumika katika ununuzi wa mashine na mitambo mipya kwa ajili ya uzalishaji wa Shirika.

#### 2.1.2 Uendelezaji wa Uzalishaji katika Shirika la MZINGA

Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua utekelezaji wa bajeti katika Shirika la MZINGA Mkoani Morogoro**.** Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali ilitenga kiasi cha **Shilingi 5,500,000,000** kwa ajili ya uendelezaji wa uzalishaji katika Shirika la MZINGA. Hadi Mwezi Machi, 2022 Serikali ilikuwa imetoa fedha kiasi cha Shilingi **5,465,210,622.68** ikiwa ni sawa na asilimia 98 ya bajeti iliyopangwa**.**

### 21.3 Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Chita

**Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) linatekeleza mradi wa kilimo cha mpunga kwenye shamba lake lenye ekari 12,000 lililopo eneo la Chita, Halmashauri ya Mlimba. Katika kutekeleza mradi huo Jeshi limeanza na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji sambamba na mpango wa kuanza kulima ekari 2500. Hadi Kamati inatembelea mradi huu JKT imetumia kiasi cha Shilingi 5.6 bilioni kwa ajili ya kuimarisha miundombinu. Aidha, ili mradi wa miundombinu ukamilike inahitajika kiasi cha Shilingi 3.3 bilioni. Vilevile Kamati ilielezwa kuwa inahitajika kiasi cha Shilingi 6.2 bilioni ili kusawazisha ardhi (Levelling) kwa ekari zote 2,500. Hii inapelekea kuwa na upungufu wa jumla ya Shilingi 9.5 bilioni.

Kamati ilielezwa kuwa ikiwa mradi huu utakamilika na kuanza uzalishaji Utasaidia kupata uhakika wa usalama wa chakula kwa Jeshi na Taifa kwa ujumla. Mathalani, kwa ekari 2,500 zinaweza kuingiza sokoni magunia ya mpunga yenye ujazo wa kilo 100 yapatayo 62,500 kwa msimu mmoja.

### 2.1.4 Ujenzi wa Jengo kuu la Ulinzi wa Taifa- Kikombo

**Mheshimiwa spika,** Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatekeleza mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi katika eneo la Kikombo Mkoani Dodoma. Ujenzi wa mradi huo ulianza Mwezi Machi, 2020 na unatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba, 2022.

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu unajengwa kwa kutumia *Force Account* kwa kiasi cha **Shilingi 58 bilioni.** Ikiwa ujenzi huo usingejengwa kwa F*orce Account* ungetumia kiasi cha Shilingi 127 bilioni. Hivyo utaratibu huo umeokoa kiasi cha Shilingi 69 bilioni. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa umefikia **asilimia 41.5**

### 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako

Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo kwa kutaja yafuatayo:

i) Utekelezaji wa majukumu ya Mashirika ya NYUMBU na MZINGA unaridhisha mbali ya kwamba yanakabiliwa na changamoto mbalimbali. Aidha, ushauri wa Kamati kuhusu changamoto hizo umetolewa kikamilifu kwa Mamlaka husika.

ii) Kamati iliridhishwa na uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Chita. Mradi huu wa kilimo cha umwagiliaji ni muhimu kwa usalama wa chakula kwa Taifa; pamoja na umuhimu wake, Kamati ilielezwa kuwa unakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji pamoja na gharama nyingine za kilimo; na

b) Uhaba za wa zana na mitambo ya kisasa kwa ajili ya kuhudumia shamba.

**2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

i) NYUMBU ni Shirika la Kimkakati na katika kuhakikisha Shirika hilo linakuwa kubwa na kufikia malengo ya uanzishwaji wake tayari lina Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2020/2021-2029/30) ambao ikiwa utatekelezwa kwa ukamilifu, ni dhahiri kuwa Shirika litatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni rai ya kamati kuwa Serikali itasimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa mpango huo.

ii) MZINGA ni Shirika la kimkakati na kutokana na umuhimu wake ni rai ya Kamati kwamba Serikali itoe kipaumbele katika kutatua changamoto zinazokabili Shirika hilo sambamba na kuliongezea bajeti ya maendeleo mwaka hadi mwaka kwa kuzingatia mahitaji na kipaumbele cha Shirika hilo.

iii) Mradi wa kilimo Chita ni wa kimkakati na unalihakikishia Taifa chakula kwa mwaka mzima kwa kuwa ni mradi wa umwagiliaji. Dunia sasa inakabiliwa na changamoto ya Mabadiliko ya Tabianchi ambayo husababisha ukame na hivyo kutishia usalama wa chakula. Kwa msingi huo kilimo cha umwagiliaji kinatoa uhakika wa chakula kwa asilimia 100. Hivyo, ni matarajio ya Kamati kuwa Serikali italiunga Jeshi mkono kifedha na kimkakati ili liweze kutekeleza mradi huu kwa ekari zote 12,000 kwa manufaa ya Taifa.

iv) Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi Kikombo kwa utaratibu wa kutumia *Force account* umeokoa zaidi ya Shilingi 69 bilioni. Ikiwa utaratibu huu utatumika kwa uadilifi ni wazi Serikali itaokoa fedha nyingi hasa katika miradi ya majengo ya kimkakati. Ni rai ya Kamati kuwa Taasisi nyingine za Serikali na watumishi watajifunza namna Jeshi lilivyotumia utaratibu huo wa Force Account kwa uadilifu mkubwa na kwa kuzingatia viwango vya ubora vya ujezi.

v) Ni vema Serikali ikaendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya wizara hii kutokana na umuhimu wake.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo na upatikanaji wa fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa mafungu yote Matatu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari, 2022 na Machi, 2022 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ilikadiria kukusanya Mapato ya jumla ya Shilingi **85,103,000.00** kwa Mafungu yote matatu (3). Makadirio haya yalikuwa sawa na lengo lililowekwa la Makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 kiasi kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa **shilingi 87,679,496.06** sawa na **asilimia 103.03** ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la **asilimia 15.23** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa **Shilingi 76,085,664.16** sawa na **asilimia 89** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa Mafungu yote ya Wizara yamechangia ongezeko hilo; ambapo Fungu 38 (Ngome) limekusanya **asilimia 142** ya lengo lililowekwa, Fungu 39 (JKT) limekusanya **asilimia 87** ya makadirio yake na Fungu 57 (Wizara) imekusanya **asilimia 165** ya lengo lililowekwa.


**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 01** na **Grafu Na. 01** hapa chini.

**Jedwali 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato**

| FUNGU | MAKADIRIO | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO | % YA LENGO LA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 25.85 | 31,405,466.00 | 35.82 | 142.75 |
| 39 - JKT | 61,903,000.00 | 72.74 | 54,292,000.00 | 61.92 | 87.70 |
| 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1.41 | 1,982,030.06 | 2.26 | 165.17 |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***


**Grafu 1: Ulinganisho wa lengo na Makusanyo halisi ya Mapato**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia Mwezi Februari, 2022 na Makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho katika Mwaka 2021 kama inavyoonekana katika **Grafu na 2** hapa chini:-

**Grafu 2: Ulinganisho wa Makusanyo 2020/2021 na 2021/2022**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021 na 2021/2022***

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya Uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa:-

**i) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 25.85** lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa **asilimia 142.75** ya kiasi ilichokusanya.

**ii) Makusanyo ya Fungu 39 –JKT** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 72.74**, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa **asimia 87.70** ya kiasi ilichokusanya.

**iii) Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara**, yalikusudiwa kuchangia kwa **asilimia 1.41** kwenye mapato yote ya Wizara, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya Wizara yamechangia kwa **asilimia 165** ya kiasi ilichokusanya.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo ni mzuri na Wizara hadi kufikia Februari, 2022 ilikuwa imevuka lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, Kamati inapongeza Serikali kwa kuweka makadirio kwa uhalisia.

### 3.1.2 Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha Fedha kilichotolewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo . Ulinganisho huo unaonekana katika **Jedwali Na. 02** na **03** hapa chini:-

**Jedwali 2: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Kiasi cha fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa Kiuwiano | | Fungu | Kiasi cha fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 1,812,053,709,000.00 | 76.82 | | 38 | 53,497,934,254.60 | 52.62 | 74.81 |
| 39 | 386,474,955,000.00 | 16.39 | | 39 | 252,006,541,480.88 | 65.21 | 19.77 |
| 57 | 160,166,322,000.00 | 6.79 | | 57 | 69,081,232,049.00 | 43.09 | 5.42 |
| | **2,358,694,986,000.00** | 100.00 | | | **1,274,522,707,784.48** | 54.04 | 100.00 |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Jedwali 3: Ulinganisho wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Kiasi cha fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa kiuwiano | | Fungu | Kiasi cha fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa Kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 32,578,424,000 | 18.45 | | 38 | 28,317,712,000 | 86.9 | 31.94 |
| 39 | 4,000,000,000 | 2.27 | | 39 | 3,272,048,797 | 81.8 | 3.96 |
| 57 | 140,000,000,000 | 79.28 | | 57 | 57,058,481,631.93 | 40.7 | 64.37 |
| | **176,578,424,000** | 100.00 | | | **88,648,242,428.93** | 50.2 | 100.00 |

Kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea Shilingi **1,274,522,707,784.48** sawa na asilimia 54.04 ya fedha zilizoidhinishwa.

(ii) Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **1,185,874,465,355.55** sawa na asilimia 93.04 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **88,648,242,428.93** sawa na asilimia 6.96 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

(vii) Kati ya fedha zilizopokelewa, asilimia 74.81 ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome), asilimia 19.77 ni kwa ajili ya Fungu 39 (JKT) na asilimia 5.42 ni kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara).

(iii) Kiasi kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni pungufu ya **asilimia 8.20** ikilinganishwa na Fedha zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambapo kwa kipindi kama hicho ilipokea shilingi **95,917,678,289.97** .

(iv) Kati ya Shilingi **88,648,242,428.93** zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, asilimia 64.37 ya Fedha hizo ni kwa

ajili ya Fungu 57 (Wizara) na asilimia 31.94 ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome) na asilimia 3.69 ni kwa ajili ya Fungu 39 (JKT).

(v) Fungu 38 (Ngome) limepokea Shilingi **28, 317,212,000.00** sawa na asilimia 86.92 ya Shilingi **Bilioni 32.5** zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

(vi) Fungu 57 (Wizara) limepokea Shilingi **57,058,481,631.93** sawa na asilimia 40.7 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Fungu hilo.

(vii) Katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu, Fungu 38 (Ngome) lilipokea asilimia 52.6, Fungu 39 (JKT) lilipokea asilimia 65.21 na Fungu 57- (Wizara) lilipokea asilimia 43.09.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti. Kwa mfano, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 (Ngome) ikiwa ni asilimia 76.82 ya Bajeti ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni asilimia 52.6 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, na Fungu 39 lililidhinishiwa asilimia 16.59 ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na fungu hilo hadi kufikia Februari, 2022 ni asilimia 19.77 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara kufikia Februari, 2022 na Fungu 51 ilitengewa asilimia 6.7 ya bajeti yote ya Wizara, hadi kufikia Februari 2022 ilikuwa imepokea asilimia 5.4 ya fedha zote zilizopkelewa na Wizara. Kwa mwenendo huu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipa uzito stahiki kwa Bajeti ya Ngome, Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mwenendo huo mzuri, Kamati haijaridhishwa na mtiririko wa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara) ambapo hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Fungu hilo lilikuwa limepokea **asilimia 40** ya fedha iliyotengewa kwa ajili ya maendeleo.

Ni vema Serikali ikatoa fedha hizo za maendeleo kwa mujibu wa ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyowekwa ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

### 3.2 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri masuala mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge kuwa, taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Taarifa hii.

Mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 39-JKT kwa mtiririko uliopangwa. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Fungu 39 lilikuwa limepokea fedha za maendeleo kwa **asilimia 81.8.** ya bajeti iliyotengewa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri huu na kuisisitiza kuendelea na utaratibu huu kwa Mafungu yote.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uzingatiaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao unahitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Mathalani, ushauri kuhusu Serikali kutoa fedha zote zilizotengwa katika Mwaka 2020/2021 kwa ajili ya kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi. Maelezo yaliyotolewa kwenye Kamati yalibainisha kuwa hakuna fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023,

Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na Kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu sita likiwemo kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa na zana bora,mafunzo na mazoezi, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma pamoja kuwapa viijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa malengo sita (6) ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi wake.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 87,603,000** Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la **asilimia 2.9** ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 39- JKT ambapo lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia 4.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuongeza lengo la makadirio kwa Fungu hilo, hususan kwa kuzingatia kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2022 Fungu 39- JKT lilikuwa limeshakusanya asilimia 87.7 ya makadirio


yaliyowekwa katika mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika **Jedwali Na. 04.** na **Chati Na. 03** hapa chini: -

**Jedwali 4: Mchanganuo wa Makadirio ya mapato**

| Fungu | Makadirio | Asilimia ya lengo la Wizara |
|---|---|---|
| Fungu 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 25 |
| Fungu 39 - JKT | 64,403,000.00 | 74 |
| Fungu 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1 |
| **JUMLA** | **87,603,000.00** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Chati 1: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo 2022/2023**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii limeongezeka kwa **asilimia 2.9** ikilinganishwa na lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

ii) Fungu 38 (Ngome) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 25** Sawa na Mwaka wa fedha 2021/2022.

iii) Fungu 39 (JKT) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 75** ambapo Mwaka 2021/2022 lilitegemewa kwa asilimia 72.7

iv) Fungu 57 (Wizara) linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha asilimia 1 wakati Mwaka 2021/2022 lilitegemewa kwa asilimia 1.4 Hata hivyo, kiasi hicho cha Makadirio ya Makusanyo kwa Fungu 57 kinalingana na Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia Maoni ya Kamati kuhusu lengo la ukusanyaji wa Mapato kwa kuzingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana. Hata hivyo, kwa mara nyingine, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa uhalisia wa makusanyo kwa ajili ya Fungu 57 uangaliwe upya.

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni Shilingi **2,712,787,404,997.00 kati** ya fedha hizo shilingi **2,482,454,233,997.00 sawa** na asilimia 91.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **230,333,171,000 sawa na asilimia 8.49** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma (Items), Vifungu (Subvotes) na Mafungu (Votes) yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

a) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 imeongezeka kwa Shilingi **354,092,418,997** ikilinganishwa na

bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Tofauti hiyo ni ongezeko la asilimia 15. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake wa mara kwa mara wa kuongeza kiwango cha Bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia.

b) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa Shilingi 53,754,747,000 ambayo ni sawa na asilimia 30.4 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Fedha hizi zimeongezeka katika Fungu 38 kwa asilimia 73, Fungu 39 kwa asilimia 249.14 na Fungu 57 kwa asilimia 14.29

c) Kati ya Shilingi **230,333,161,475.00** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, asilimia 24.47 ni kwa ajili ya Fungu 38- Ngome, asilimia 6.06 ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na asilimia 69.46 ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo maoni yanayojenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Naomba kubainisha maoni hayo kama ifuatavyo:-

### 5.1 Maoni ya Kamati

(i) Upungufu wa watumishi katika Mashirika ya MZINGA na NYUMBU usipoendelea kufanyiwa kazi na Serikali, utaathiri utekelezaji wa majukumu ya Mashirika hayo na kupunguza tija iliyokusudiwa.

(ii) Kuwezesha inavyostahili utekelezaji wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika eneo la Chita, ni jambo la kimkakati litakaloongeza uhakika na upatikanaji wa chakula.

(iii) Kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi ni jambo linalochangia kufanikisha azma ya Serikali kuboresha makazi ya Wanajeshi. Aidha, mahitaji ya kibajeti kwa ajili ya ukarabati yanafaa kutimizwa inavyotakiwa.

(iv) Mantiki ya Msajili wa Hazina kukabidhi shamba la Mngeta *(Kilombero Plantation Ltd)* lenye ukubwa wa ekari 14,545 kwa SUMAJKT, inaweza kupatikana iwapo changamoto za uchakavu wa mitambo, miundombinu na ukosefu wa mtaji kwa SUMA JKT zitatatuliwa.

(v) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati ya Bunge kuhusu Sera ya Ulinzi wa Taifa kwa vipindi tofauti umefikia hatua ya kuhitaji kuwekwa katika utekelezaji. Aidha, kupokewa kwa maoni ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wengine muhimu kama ilivyoripotiwa katika Kamati, ni jambo la maana iwapo utekelezaji utaanza.

(vi) Juhudi za Serikali kuimarisha Mipaka yetu ili kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zinastahili kuendelezwa. Aidha, ili kuendelea kudhibiti mianya ya mipaka inayoweza kutumiwa isivyostahili, Serikali inapaswa kuboresha uratibu wa jambo hilo.

(vii) Kukosekana kwa hati za Maeneo yanayomilikiwa na Wizara ya Ulinzi ni jambo linalochangia kuwavutia baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo na baadaye kuibuka kwa migogoro ya umiliki.

## 5.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa maoni hayo, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 57 (Wizara) kwa mtiririko uliopangwa. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 38 (Ngome) na Fungu 39 (JKT) ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

(ii) Jeshi la Wananchi liandae na kutekeleza mkakati wa muda mrefu wa kupeleka Askari wenye utaalamu unaohitajika katika Mashirika ya NYUMBU na MZINGA. Kufanya hivyo itapunguza upungufu wa rasilimaliwatu kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji.

(iii) Serikali kupitia Wizara ya Fedha itenge Shilingi 9.5 bilioni zinazohitajika kwa ajli ya kumalizia miundombinu ya umwagiliaji na kusawazisha *(leveling)* shamba la Jeshi la Chita kwa ekari 2500. Aidha zitolewe fedha za kununua mitambo na mashine za kisasa za kilimo kwa kuanzia mwaka wa Fedha 2022/2023.

(iv) Serikali kupitia Wizara ya Fedha iandae utaratibu mahsusi utakaowezesha upatikanaji wa fedha kwa aijili ya kufanya ukarabati wa nyumba za makazi ya Wanajeshi.

(v) Serikali itoe ruzuku kwa SUMAJKT ili kuendeleza kilimo cha kisasa katika shamba la Mngeta na kuweza kuzalisha mazao ya kutosha.

(vi) Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ulinzi (*The National Defence Policy*) kwa umuhimu wake kwa taiafa kama ambavyo imekuwa ikishauriwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa.

(vii) Serikali ichukue hatua madhubuti za kuendelea kuimarisha miundombinu ya kiulinzi na kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi katika mipaka yetu pamoja na mwambao wa Bahari ya Hindi.

(viii) Serikali itoe kiasi cha fedha kitakachotengwa kwa ajili ya Mashirika ya kimkakati ya NYUMBU na MZINGA kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge na kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

(ix) Uandaliwe mkakati maalum unaotekelezeka wa kupima na kupata Hati za maeneo yote ya Wizara hii ambayo hayajapimwa.

(x) Serikali ikamilishe mchakato wa kuruhusu Jeshi kuwa na Bounded Warehouse yake.

(xi) Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya Taifa.

(xii) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2019/2020, 2020/2021 na 2021/2022.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - | **Mwenyekiti** |
| 2. Mhe. Vicent Paul Mbogo, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb | | Mjumbe |
| 8. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb | - | Mjumbe |
| 9. Mhe. Cosato David Chumi, Mb | - | Mjumbe |
| 10. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | - | Mjumbe |
| 11. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb | - | Mjumbe |
| 12. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - | Mjumbe |
| 13. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb | - | Mjumbe |
| 14. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb | - | Mjumbe |
| 15. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb | | Mjumbe |
| 16. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa | - | Mjumbe |
| 17. Mhe. Ali Juma Mohammed, Mb | - | Mjumbe |

18. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Stagomena L. Tax kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Faraji Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J Mwihambi, ndc kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Omary Magwinza na Bi. Victoria Mizengo na wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**Vita Rashid Kawawa, Mb**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

Mei, 2022

***KIAMBATISHO NA. 1***

**UTELEKEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA (NUU) KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2021/2022**

***(i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 39- JKT kwa mtiririko uliopangwa. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, Fungu hili lilikuwa halijapokea fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 38 (NGOME) na 31 Fungu 57 (Wizara) ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.***

Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Fungu 39 – JKT limeidhinishiwa **Shilingi 4,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 limepokea **Shilingi 3,501,349,288.00**.

Aidha, Fungu 57 – Wizara na Fungu 38 - NGOME yamepokea **Shilingi 83,803,992,017.65** kati ya **Shilingi 150,000,000,000.00** na **Shilingi 9,694,160,292.32** kati ya **Shilingi 10,000,000,000.00** mtawalia katika kipindi husika. Ni matumaini ya Wizara kuwa Serikali itatoa fedha zilizobaki hadi kufikia mwezi Juni, 2021. Tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kuiwezesha Wizara ya Ulinzi na JKT na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake.

***(ii) Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka 2020/ 2021 kwa ajili ya kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli hiyo.***

Wizara ya Ulinzi na JKT inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za makazi ya wanajeshi.

***(iii) Serikali ikamilishe na kuanza utekelezaji wa Mpango wake wa miaka kumi (2021/22-2030/31) wa kuliimarisha Shirika la NYUMBU kuweza kukabiliana na changamoto ya uchakavu***

***wa mitambo na teknolojia iliyopitwa na wakati. Hii italiwezesha Shirika hilo kutekeleza shughuli zake za msingi kwa ufanisi zaidi na hivyo kuokoa fedha nyingi za Serikali.***

- Wizara imekamilisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2021/22 – 2030/31) wa Kuliimarisha Shirika la Tanzania Automotive Technology Centre (TATC) kwa kupitishwa katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwemo IMTC na Baraza la Mawaziri. Aidha, utekelezaji wa Mpango huo unatarajiwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

- Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya Bajeti ya Mashirika ya NYUMBU na MZINGA kutoka **Shilingi bilioni 7.5** hadi **bilioni 9** na **Shilingi bilioni 4** hadi **bilioni 5.5** mtawalia kwa mwaka 2021/22. Aidha inategemewa Serikali itatoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge na kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

***(iv) Serikali ihakikishe kuwa Awamu ya Pili ya Huduma za Bima ya Afya (Oktoba 2021 hadi 2026) inatekelezwe kama ilivyopangwa ili kuwezesha Wanajeshi kupata huduma za afya katika Hospitali za Jeshi, Serikali, Hospitali Binafsi pamoja na Mashirika ya Dini.***

Wizara imepokea maoni ya kamati na imejipanga kuhakikisha Awamu ya Pili ya Huduma za Bima ya Afya kwa Wanajeshi ambayo inatarajia kuanza mwezi Oktoba, 2021 hadi Septemba, 2026 inatekelezwa. Awamu hii itahusisha huduma za afya katika Hospitali za Serikali, Binafsi pamoja na Mashirika ya Dini.

***(v) Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Ulinzi ambayo Kamati imekuwa ikishauri kwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilieleza kuwa tayari maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yameshapokelewa na taratibu nyingine za kuwasilisha katika Baraza la Mawaziri zinaendelea.***

Wizara imepokea maoni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wengine muhimu na inaendelea kuyafanyia kazi. Aidha, ni mpango wa Wizara kuhakikisha kuwa Sera hiyo inakamilika mapema iwezekanavyo.

***(vi) Serikali iendelee kuimarisha miundombinu ya kiulinzi iliyopo katika mipaka yote ya Nchi ikiwa ni pamoja na barabara, alama za mipaka na mengineyo.***

Suala la uimarishaji wa miundombinu ya kiulinzi katika mipaka ya nchi ikiwa ni pamoja na barabara za ulinzi, alama za mipaka na mengineyo ni mtambuka, likihusisha Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikiana na wadau hao itaendelea kuimarisha miundombinu hiyo ikishirikiana na nchi tunazopakana nazo.

***(vii) Serikali iweke utaratibu wa kutoa fidia badala ya kulipa kodi ya pango katika maeneo ya Wananchi ambayo yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara ya Mawasiliano Salama Jeshini. Kwa kufanya hivyo Serikali itamiliki maeneo hayo lakini pia itaokoa fedha nyingi ambazo zingeendelea kulipwa kama kodi ya pango.***

Wizara ilikwishaongea na wamiliki wa maeneo ilikojengwa minara. Baadhi waliridhia maeneo yao yatumike bila kulipiwa kodi ya pango la ardhi. Wengine walitaka walipwe fidia ya ardhi ili ardhi hizo zitwaliwe na kumilikiwa na Wizara ya Ulinzi na JKT. Wizara kwa sasa imekwishaunda timu zitakazokwenda mikoani kufanya uthamini wa maeneo ili wahusika walipwe fidia.

***(viii) Serikali ifanye tathmini ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi kwa Wanajeshi itakayojumuisha nyumba 3,936 zilizobaki katika mradi wa Nyumba 10,000 na kutenga bajeti ya utekelezaji wake ili kupunguza changamoto ya nyumba za makazi kwa Wanajeshi.***

Tathimini ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi ya Wanajeshi imeshaanza na inatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

***(ix) Serikali ihakikishe masharti ya mikopo hiyo yanaruhusu Serikali kuchagua Mshauri elekezi na Mkandarasi wa kujenga nyumba hizo ili kuhakikisha zinakuwa na viwango vya ubora unaotakiwa.***

Maoni ya kamati yamepokelewa. Wizara itajitahidi kuhakikisha kuwa masharti ya mikopo ya ujenzi yanaruhusu Serikali kumchagua Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa kutekeleza miradi inayokusudiwa kwa ufanisi.

***(x) Serikali itoe fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge na kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa.***

Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha bajeti inayoidhinishwa inatolewa kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

***(xi) Serikali ikamilishe Mpango wake wa kuwapatia wahitimu wote wa kidato cha Sita mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria. Aidha, ili kufanikisha mpango huo, Serikali itenge na kutoa fedha kwa ajili ya kuongeza Makambi na kuboresha miundombinu ya Makambi yaliyopo.***

Wizara imeandaa mpango utakaowezesha kuchukua Vijana wote wanaohitimu kidato cha sita kupata mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria. Mpango huo umeanza kwa kutathmini uwezo wa makambi yaliyopo pamoja na kushirikisha wadau muhimu wakiwemo Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) na Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (TCU) ili kubaini muda sahihi wa mafunzo. Pamoja na mpango huo Wizara ya Ulinzi na JKT inategemea kuongeza idadi ya Vijana wa Mujibu wa Sheria kutoka 21,000 mwaka 2020/2021 hadi kufikia vijana 35,000 kwa mwaka 2021/2022.
JKT imepokea fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi 3,501,349,288.00** katika mwaka 2020/21. Fedha hizo

zimetumika kukarabati na kujenga Makambi ya JKT. Aidha, Wizara itaendelea kuongeza bajeti ya kuboresha miundombinu ya Makambi yaliyopo ili yaweze kuongeza idadi ya Vijana wa Mujibu wa Sheria wanaochukuliwa.

***(xii) Serikali ikamilishe kwa haraka Mpango wa kuwawezesha vijana wanaojitolea kwa ajili ya mafunzo ya JKT kupata mitaji kwa kushirikisha Sekta na Taasisi nyingine. Wakati wa majadiliano na Wizara hii Kamati ilielezwa kuwa Utekelezaji wa Mpango huu unasimamiwa na Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi na Ajira, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.***

Jukumu la msingi la Jeshi la Kujenga Taifa ni kutoa mafunzo na malezi ya Vijana ili kuwajengea uzalendo na ukakamavu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Vijana hufundishwa stadi za maisha zitakazowawezesha kujiajiri pindi wanapomaliza mafunzo. Vijana hupata Stadi hizo za maisha kupitia shughuli mbalimbali za JKT zikiwemo kilimo, mifugo, viwanda na kupitia miradi mbalimbali ya ujenzi zinazofanywa na JKT.

Kupitia vyuo mbalimbali vya ufundi stadi vilivyopo JKT Vijana hupatiwa mafunzo ya ufundi stadi ikiwemo useremala, ushonaji, ufundi mchundo, ufundi magari na umeme. Mafunzo haya huwapa ujuzi vijana kuweza kujiajiri wanapomaliza mafunzo. Aidha, Vijana hupatiwa vyeti vinavyotambuliwa na VETA na NACTE ili ujuzi wao uweze kutambuliwa baada ya kumaliza mafunzo. Wizara imefanya mazungumzo na Taasisi zingine zikiwemo Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu Ajira, Kazi, Vijana na wenye Ulemavu kwa lengo la kuwasaidia vijana kuanzisha miradi na kupata mitaji.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza na uchangiaji. Ahsante sana Mheshimiwa Mkundi.

Tutaanza na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma, atafatiwa na Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mheshimiwa Saada Monsour Hussein ajiandae.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nikawa wa kwanza kuchangia katika bajeti hii muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Kwa sababu maendeleo yoyote ni usalama na hata matibabu mazuri yanatendeka vizuri pakiwa na usalama.

Mheshimiwa Spika, napongeza bajeti hii kwa namna ambavyo imesomwa na kwa namna ambavyo nayo imejielekeza pamoja ni masuala ya ulinzi lakini imejielekeza kutekeleza Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi ambayo inasimamiwa na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, napongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze pia kwa namna ambavyo Jeshi letu limeendelea kukabiliana na baadhi ya changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza katika mipaka yetu. Katika moja ya kazi ngumu sana ambazo zinahitaji kujitolea mno ni kazi ya kuwa mwanajeshi. Daktari tunamhitaji pale tunapokuwa tunaumwa tu, tukishapona hatumuhitaji tena daktari. Lakini mwanajeshi ama jeshi letu tunalihitaji tukiwa wazima, tunalihitaji tukiwa tunaumwa, tunalihitaji tukiwa na uchumi imara na tunalihitaji uchumi wetu ukitetereka ili liendelee kudhibiti mipaka yetu tuendelee kuwa salama. Nalipongeza sana kwa namna ambavyo limekuwa likifanya vizuri katika kutimiza wajibu wao huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nizungumzie kuhusiana na mahusiano baina ya majeshi yetu hasa Jeshi letu la Wananchi Tanzania na wananchi wanaokaa karibu na Kambi zao hasa zilizoko Mjini. Mimi hapa nataka nipongeze kupitia Kambi ya JWTZ ya Mwanyanya iliyokuwepo katika Jimbo langu la Mtoni. *(Makofi)*

Kambi ile imezungukwa yote na makazi ya watu, kambi ile ina mahusiano mazuri sana wananchi katika eneo

lile na askari wetu katika Kambi ile wamekuwa ni mfano mzuri wa askari wengine katika Jeshi letu Tanzania nzima. Kambi ile imejitolea baadhi ya vitu ikachanga na wananchi ili watengeneze sehemu ya njia iliyoharibika. Jeshi pale lilitoa kokoto, jeshi lilitoa simenti, jeshi lilitoa mchanga wananchi na vijana wakajikusanya na sisi viongozi tukaongeza nguvu, wakamwaga zege katika eneo korofi ambalo linatumika na wananchi na wao askari wanalitumia kwa uchache sana. Napongeza sana nidhamu na uimara wa Jeshi letu katika kushirikiana na wananchi wetu katika kipengele hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukarimu huu wa Jeshi letu kushirikiana na wananchi umesababisha wananchi wengi katika Jimbo la Mtoni wanaoishi karibu na Kambi ile ya Mwanyanya kupenda kutumia Hospitali ya Jeshi iliyokuwepo katika Kambi ile. Sasa ombi langu kwa sababu ukarimu wao umetuvutia sana pamoja vituo vingine vya afya vilivyokuwepo, lakini tunapenda kutibiwa kwao, ukarimu na namna ambavyo wanatupokea basi naiomba Wizara hii katika fedha zake za kuboresha vituo vya afya vilivyopo katika majeshi na nyingine ipelekwe pale katika Kambi ya Mwanyanya ili pawe na vifaa vingi zaidi vya kuhudumia wananchi. Vifaa hivyo pale vikipelekwa vitahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nikwambie hatuendi pale pia kwa sababu hakuna Hospitali nyingine laa! lakini ni namna ambavyo Jeshi letu limekuwa na ukarimu na linawapa wananchi tiba sahihi. Kwa hiyo, naomba katika bajeti hii pamoja najua kuna mambo pale yanafanywa wakati mwingine linakarabatiwa taratibu naomba mtupelekee fedha katika kambi ile ikaboreshwe hospitali na katika hospitali nyingine zote. Hospitali zilizopo katika kambi zetu zinahudumia sana wananchi yawezekana kuliko majeshi tuliyokuwa nayo. Sasa mimi naomba hospitali ile iboreshwe, hospitali nyingine ziboreshwe na hospitali zote hasa ambazo Kambi zipo karibu na makazi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niendelee kulipongeza Jeshi letu, sisi tuko pamoja, bajeti yenu

tutaipitisha kwa kishindo muendelee kulinda mipaka yetu, tuko pamoja nanyi na Mungu awajaalie kila kheri. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji, atafatiwa na Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami sina budi kukushuruku kwa kuweza kuniona kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa nchi yetu katika ulinzi wa nchi yetu na vilevile Amiri Jeshi Mkuu ndiye mpambanaji wa mambo yote katika nchi yetu hii. Rais wetu ambaye ndiye Amiri Jeshi wetu Mkuu hatuna namna ya kuweza kumpongeza yaani inabidi tumpongeze kwa kiasi kikubwa sana maana yake haya yote ambayo anayoyafanya ni kutimiza wajibu wake na kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi hasa katika Sura 505 katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inahusiana na Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, pili tumpongeze Mkuu wetu wa Majeshi Ndugu Venance Mabeyo kwa umakini wake na uzalendo wake wa kipekee katika kuliongoza Jeshi letu la Tanzania na pia uzalendo wake wa kufanikisha nchi yetu hii kuwa katika hali ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika mchango wa Wizara; moja katika jukumu la msingi la Wizara ya Ulinzi ni kuwapa vijana wa Kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi, ya stadi za kazi, utamaduni, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea. Lakini mimi vilevile ningeongezea kitu kimoja ambacho ni uwezo wa kuzalisha mali, ambalo hilo ni moja ya jukumu lililokuwa katika moja ya Wizara. Sasa tuje katika uzalishaji mali huu nadhani kwamba Jeshi letu au Wizara yetu inafanya kazi kubwa sana ya kuweza kuwachukua vijana wetu kuwapa mafunzo pale ya stadi mbalimbali na vilevile

kuwafundisha ukakamavu pamoja na uzalendo. Lakini bado tunatakiwa kwamba bado tuendelee kujiuliza katika haya mafunzo tunayowapatia vijana wetu je, bado yanakidhi katika uzalishaji mali katika nchi yetu. Maana yake lengo kujenga uzalendo, lengo ni kuwapa stadi, sasa mimi pengine ningeishauri Wizara pamoja na mambo ambayo tunayafanya huko maana yake wakapatiwa zile stadi mbali za kilimo, lakini pia tukawa na stadi za ufundi kama vilivyo vituo vyetu hivi vya mafunzo hivi vituo vya *vocational* ambako nako huko labda pengine tungeweza kujenga wigo zaidi ili vijana waweze kupata ule ujuzi ambao utakaoweza kuwasaidia. Watakapoweza kumaliza mafunzo wakaweza kujitegemea na kuweza kujiendeleza na tusiangalie tu kwamba suala la kuwapeleka vijana kule kujenga uwezo au kupata ukakamavu ikawa ndiyo sababu ya kwenda kuwachukua kwa kuwaajiri. Wao lengo kubwa maana yake twende kwa kuweza kuwaajiri na kuweza kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, nije katika kuimarisha Ulinzi na Usalama wa nchi na mipaka yetu yaani katika suala la ibara ya chama chetu inazungumzia suala la ulinzi na usalama ambalo hilo lipo katika hali njema. Lakini muhimu zaidi ambayo nije vilevile katika kazi zinazotekelezwa kupitia fedha za maendeleo. Katika kifungu kimoja ambacho cha fedha za maendeleo kifungu (h) kinazungumzia kutatua migogoro ya ardhi kwa kupima na kufanya uthamini wa maeneo ya Mikoa kama Singida Kaskazini, Mkoa wa Mjini Magharibi na kulipa fidia kwa wananchi wa maeneo matano ambayo yametajwa pale katika fedha za maendeleo. Lakini katika ulipaji wa fidia zile maana yake kuna migogoro ambayo hii imeshazungumzwa, lakini migogoro...

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika migogoro hiyo kuna baadhi ya maeneo sijaweza kuyaona pia kama Ndunga, pamoja na Udunga, Ubago pamoja na Unguja Ukuu. Ningependa au ningeshauri Serikali

waweze kuliangalia suala hilo ili kuweze kutatua migogoro ya wananchi kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja Wizara yetu hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Saada Monsour Hussein atafatiwa na Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis ajiandae.

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi leo kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yangu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya kwa kuwatumikia wananchi wake wa Tanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi nzuri naye anazozifanya kule Zanzibar. Pia naipongeza Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi hoja yangu kuhusu vijana wanaokwenda JKT. Pamoja na kuwafunza uzalendo na mambo mbalimbali, niiombe Serikali iongezewe fedha Wizara hii ili iweze kuwaajiri vijana hawa katika vitengo mbalimbali. Tukifanya hivyo, tutaweza kuwanusuru vijana hawa wasirudi mitaani bila ya kuwa na shughuli rasmi ya kufanya, kwa kuwa vijana hawa wameshafundishwa hadi kushika silaha.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya pili, Mheshimiwa Waziri unapokuja hapa kujibu hoja ya bajeti yako, uniambie Serikali imefikia wapi kuhusu ujenzi wa jengo la Wizara ya Ulinzi ndani ya Zanzibar. Pia kuhusu majengo ya Hospitali ya Bububu kwa ajili ya faragha ya viongozi wetu wa Kitaifa pale wanapoumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara hii ya Ulinzi. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipongeze sana Jeshi letu la Ulinzi wa Tanzania, kwa kweli wamekuwa ni kielelezo, wazalendo na wachapakazi. Jeshi letu linafanyakazi vizuri, lakini siyo tu kwenye masuala la ulinzi na usalama, wanatoa huduma za afya, lakini kwenye elimu, ujenzi na huduma nyingine za kijamii, hongereni sana makamanda wetu na wapiganaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maeneo mawili naomba kuchangia; kwenye jimbo langu la Nachingwea kuna mgogoro wa muda mrefu wa ardhi baina ya wananchi na Jeshi letu. Jeshi linafanyakazi nzuri na kwa kweli tunaishi nao vizuri sana. Upo mgogoro kati ya 41KJ na 843KJ; mgogoro huu ni wa muda mrefu, aliwahi kuja aliyekuwa Waziri wa Ulinzi wa wakati huo ambaye sasa ni Rais wa Zanzibar na alitoa maelezo, alizungumza na wananchi akasema watalipwa. Lakini baada ya muda alikuja afisa mwingine kutoka Makao Makuu ya Jeshi, akasema hawatalipwa ardhi badala yake watalipwa yale maendelezo waliyoyafanya kwenye ile ardhi. Wananchi wale kwa upendo mkubwa na jeshi na mahusiano mazuri waliridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya muda alikuja afisa mwingine kutoka Makao Makuu ya Jeshi, akaongea na wananchi hawa tena akasema hakuna malipo mengine yatakayofanyika, si yale ya ardhi wala si yale ya maendelezo.

Hawa wananchi wana mapenzi mazuri na tunaishi nao vizuri sana hawa wanajeshi na kati ya huduma za afya ambazo zinatolewa vizuri ni kwenye Hospitali Kuu ya Jeshi Majimaji Nachingwea, wanafanyakazi nzuri na wananchi wakawaida wanakwenda kupata huduma hapo. *(Makofi)*

Sasa niiombe sana Wizara ione umuhimu wa kuondoa changamoto hii kwa haraka ili wananchi hao waweze kujua hatima yao. Hawana maneno wananchi hawa, wapo tayari kupokea maelekezo yoyote ambayo yatatolewa na Serikali. Kwa unyenyekevu mkubwa naiomba sana Wizara ili hao wananchi waweze kujua hatima yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna shule ya sekondari *Farm 17;* eneo hili ni la Jeshi lakini kielelezo cha kwamba tuna maisha mazuri, tunaelewana vizuri na wanajeshi, jeshi wametupa Halmashauri eneo hili tulitumie kama shule ya sekondari. Eneo hili ni muhimu na sisi tunahudumia zaidi ya kata tatu wanatumia hii shule ya sekondari.

Sasa ombi langu, eneo hili sasa niiombe sana Serikali, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, mfikirie kutuachia, kwa sababu kwa sasa tukitaka kufanya miundombinu ukarabati ni lazima tupate kibali kutoka jeshini. Eneo hili tukilipata, mkituachia rasmi, mkitukatia eneo hili ambalo linazunguka shule tutawashukuru sana ili tuweze kuboresha miundombinu na wananchi wa maeneo yale waweze kupata huduma bora kwa ajili ya kupata ile elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya ameingia kwa kweli tunaona Wizara hii inamelemeta. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, sina budi kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuipongeza na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Waziri wao na watendaji wote ambao leo wamewasili hapa ili kuangalia mwenendo wa bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka nizungumzie ukosefu wa hati miliki katika kambi zetu. Ukosefu wa hati miliki katika kambi zetu ndiyo unaoleta migogoro baina ya jeshi na wananchi. Utawakuta wananchi wanakwenda kuvamia sehemu za jeshi, wakati sehemu zile hazina hati miliki sehemu ni za jeshi lakini hati miliki hawana na hawafuatilii kuzitafuta matokeo yake watu wanalima, wanajenga, migogoro inaanza wanaanza kuvutana baina ya Jeshi na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano; ukija Kambi ya Ubago iliyopo Zanzibar, Unguja Ukuu iliyoko Zanzibar na baadhi ya kambi nyingi hukuhuku Tanzania Bara. Pia nina wasiwasi kama kambi yangu ya Mtoni au Mazizini zimezungukwa na raia/ wananchi na bado wanapenya wanaingia. Utakuta hakuna uzio, kuna msitu na ule msitu mtu anaweza akapenya, sasa na hilo waliangalie, watafute mbinu kupatikane hati miliki waweze kudhibiti sehemu zao kuondoa mgogoro baina ya jeshi na wananchi wakaiingize na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia suala la Sera ya Ulinzi wa Taifa. Toka Bunge la Tisa, la Kumi, la Kumi na Moja na la Kumi na mbili kelele ndiyo hizo hizo. Lakini tushukuru hili Bunge la Kumi na Mbili taarifa iliyokuwepo tayari kwa sababu walikuwa wanazungumza kwamba bado kwamba Serikali ya Zanzibar haijatoa maoni yao, wadau hawajatoa maoni yao na sasa hivi tayari wadau wameshatoa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshatoa. Je, itaanza kutekelezwa lini? Maana yake sera ikifanyakazi ndipo jeshi litakapozidi kuimarika, kwa wafanyakazi na jeshi lenyewe. Lakini bila kuwa sera kufanyakazi inamaana ipo ndani vitabu au ndani ya mafaili itakuwa bado utekelezaji wake haujaonekana, bado elimu haijatolewa na bado wananchi watakuwa hawajafahamu nini kinachoendelea. Hatutaki kwamba mambo yao ya siri yatoke, tunataka yale

yaliyokuwa ni wajibu ambao kila mmoja ayatambue aweze kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija na hili la mashirika haya, Shirika la NYUMBU na MZINGA. Haya mashirika ni mazuri, yanazalisha lakini kwanza wana upungufu wa wafanyakazi na hao wafanyakazi waliopo pale wawe na utaalam kwa sababu sehemu ile inafanyakazi ya kitaalam; bila ya kuwa na wataalam haitaweza kuzalisha kama anavyofikiria. Ina uhaba wa rasilimali watu na hao watakaoajiriwa wawe wataalam waweze kufanyakazi za kuweza kutambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la umwagiliaji maji; wanacho kilimo cha umwagiliaji maji, tulikwenda tukaona Chita, wapo vizuri wanalima, kuna samaki wazuri, watamu maana tulipewa tukala. Lakini tatizo lililopo pale hawana vitendea kazi vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga atafuatiwa na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, ajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya ya kuwalea vijana lakini kuwajenga katika kulitumikia taifa lao, katika uzalendo wa Taifa lao, lakini kwa sasa kuwatengeneza katika mazingira ya kujitegemea kwenye uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru kwa moyo wa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, lakini pia kumpongeza na kumshukuru Mkuu wetu wa Majeshi kwa

namna ambavyo waliweza kuwalea, kuwachukulia vijana kwamba wanaweza wakakosea, lakini wakaendelea kulelewa vijana wale ambao walifukuzwa kambini na leo wamerudishwa, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika vijana wale walifanyakazi kubwa sana ya ujenzi wa miradi mbalimbali katika nchi yetu. Lakini ninaombi kwa Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana, wapo vijana ambao walikuwa kwenye kambi ya Ukonga wao walitumika kabla ya wale ambao walikwenda kujenga ukuta wa Ikulu na Mererani. Vijana wale walishiriki kujenga maeneo mbalimbali, wamejenga Bwawa la Umeme Rufiji, wamejenga ujenzi wa Chuo cha *VETA* Lindi; Chuo cha Ualimu Kigoma; Bandari Kavu Kwala; Ofisi ya Manispaa Kinondoni; majengo mapya Mzumbe na maeneo mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kazi kubwa hiyo yote vijana ambayo waliifanya, vijana wale waliweza kuchukuliwa na kurudishwa Mgulani na baada ya hapo wakatawanyishwa kurudi majumbani na sasa vijana wale wapo tu majumbani wamekaa. Lakini tunaiomba sasa Serikali, tunaiomba sana Serikali iweze kuwafikiria vijana wale kwa jicho la pili kwa sababu ni hazina kwa taifa letu kwa kuwa wamepata ujuzi mbalimbali ujuzi wa kijeshi lakini na ujuzi pia wakuweza kujiwezesha wao wenyewe kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia Wizara hii inawatengeneza vijana vizuri sana katika kwenda baadaye kujiajiri. Wanajengwa katika kilimo, ufugaji, uvuvi, lakini baada ya hapo pamoja na Serikali kwamba imewekeza nguvu kubwa kwa vijana hawa, vijana hawa wanaondoka wanakwenda kuwa hawana tija kwa sababu hawana uchumi mwingine ambao unawawezesha kuweza kuendeleza ule ujuzi wao ambao wamepata wa kilimo, lakini pia uvuvi pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, JKT inafanya mausala ya kilimo, tumeweza kuambiwa hapa pale Chita mwaka jana walilima

kilimo cha mpunga, walitumia fedha nyingi sana kuwekeza, lakini hatima yake faida waliyopata ni ndogo kuliko fedha ambayo wamewekeza. Niombe sasa waweze kuwafikiria vijana wale ambao wanawapatia mafunzo wanapotoka kwa sababu bado Jeshi lina maeneo makubwa vijana hawa kwa sababu wana ujuzi na Serikali iweke mkono wake hapa. Ofisi ya Waziri Mkuu ina mikopo mbalimbali ya kuwawezesha vijana, tuone wanawezaje kuwawezesha vijana hao kwa sababu wana ujuzi wanapokuwa wametoka waandaliwe kwenye kilimo ili wanapolima wao, jeshi hili linajua kwamba sisi tunalima hapa mpunga, lakini tuna vijana pembeni ambao wanazalisha na wataleta kwenye jeshi ili tuweze kuunganisha nguvu ya pamoja na hatimaye jeshi hili katika upande wa kilimo liwe lina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini halikadhalika, niombe jeshi letu hili linafanyakazi kubwa sana ya kuwaanda vijana, basi lisijifungie liweze kuunganisha nguvu na Wizara ya Kilimo kwa sababu tayari tunaona Wizara ya Kilimo imeshatoa fursa kwa vijana na vijana hawa tayari wameshaandaliwa siyo vijana tena wa kwenda kuanza kuwafundisha. Lakini Wizara ya Viwanda na Biashara ili vijana hawa waweze kupatiwa fursa ya masoko pale ambapo watakuwa wamepewa mitaji na kuweza kuwajenga vijana vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vijana wale ambao niliwaongelea mwanzo walikuwa chini ya Kanali Ashraf Bakari Hassan. Niendelee kusisitiza kwamba tuone vijana wale waangaliwe kwa jicho la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa inafanyika Kikosi cha Mizinga, tuombe sasa nguvu kubwa ipelekwe kule ili kuweza kuendeleza vipaji vya Watanzania vya kuweza kutengeneza vitu mbalimbali na vikaweza kutusaidia sisi wenyewe bila ya kutumia gharama kubwa ya kwenda kuagiza vitu nje ya nchi. Jeshi letu lipo vizuri sana ni kiasi tu cha kuwezeshwa ili waweze kutenda miujiza, kutenda maajabu ambapo itasaidia sana kupunguza gharama ya hivyo vitu ambavyo tunaviagiza kutoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda ajiandae.

Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shaban Ng'enda, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia katika Wizara yetu hii muhimu ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa kuanza na mimi ningependa vilevile kumshukuru sana Mwenyeezi Mungu *Sub-hanallah Wataallah* kwa kutujaalia uhai uzima na salama lakini halikadhalika kumshukuru Jemedari Mkuu au Amiri Jeshi Mkuu wetu, Mama Samia kwa jitihadi ambazo amekuwa akizichukua katika kuliendeleza Taifa hili. Mheshimiwa Rais ametuletea jembe Waziri wetu ambaye kwa kweli anatusaidia sana katika kuiendeleza Wizara hii na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri muda mfupi lakini ameweza kufanya makubwa katika Wizara hii pamoja na timu yake, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja katika mchango wangu mimi nikiwa kama Balozi wa Mazingira na nimpongeze sana Mheshimiwa Jafo kwa kunipa nafasi hii, ili niende kuitendea haki ningekwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu katika *page 13* ambayo inaelezea utunzaji wa mazingira katika *speech* yake Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri umepanda miti 147,000 katika makambi yetu kwa kweli hiki kiwango kidogo tukizingatia mahitaji ya nishati ya kupikia, miti ya kujengea katika makambi yetu. Kwa hiyo, ningeomba tu kwamba katika bajeti hii inayokuja tukaongeza kidogo kiwango cha upandaji miti katika makambi yetu kwa sababu miti 100,000 ni kidogo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili Mheshimiwa Waziri kule Zanzibar kuna uharibifu mkubwa wa mazingira katika makambi yetu na zaidi kuna Kambi ya *Ali Khamis Camp* ambayo ilipanda miti mingi kipindi cha nyuma, lakini pia kuna kambi ya Mwanyanya ambayo ilipanda miti mingi kipindi cha nyuma lakini hivi sasa miti ile inavunwa lakini bila ya kurejeshewa miti mingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba tu katika kipindi kinachokuja tukajikita zaidi katika upandaji miti katika makambi yale haya ile miti ambayo tunavuna basi tuirudishe tena. Lakini kuna Kambi ya Makuwe na Bububu kuna uharibifu mkubwa wa mazingira Mheshimiwa Waziri, ningeliomba pia ukaweka jicho lako kule kwa sababu Idara ya Misitu na Maliasili kwa miti isiyorudishwa wamekuwa wakigombana mara kwa mara na kambi hizi kwa ukataji miji hovyo. Kwa hiyo, ningelipenda tu pia tukawaelimisha kambi zetu kwamba wakachukua jitihada za kutunza mazingira kama ulivyoahidi katika hotuba yako hapa kwamba miti hii ya asili inalindwa na kutunzwa. Kwa hiyo, nafikiri kambi hizi kwa sababu vilevile kuna miti ya asili basi tungeitunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika Mheshimiwa Waziri katika suala la uwekezaji katika kambi zetu hizi za Zanzibar kumekuwa na uwekezaji ambao siyo sahihi, kwa sababu mfano kama kuna msitu mdogo katika Kambi ya Bavuai, ulikuwepo msitu ambao ni mzuri na umetunzwa kipindi kirefu, lakini hivi karibuni tumeanza kuumega, tumejenga vituo vya mafuta *(shell)* pale na tukitoka Kiembesamaki, Uwanja wa Ndege mpaka Mwanakwerekwe kuna karibu vituo vya mafuta *(shell)* saba. Sasa sijui kama kulikuwa na umuhimu wa kuwa vituo vya mafuta *(shell)* nyingine pale.

Kwa hiyo, mimi ushauri wangu tu Mheshimiwa Waziri tunapowekeza katika Kambi zetu hizi tuangalie uhalisia na tuangalie vilevile ramani za Manispaa na Miji yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini halikadhalika, tukiangalia katika Kambi ya Mtoni kuna vi-*garage* pale vya ajabu ajabu, sasa sijui kama kulikuwa na umuhimu wa zile *garage* pale

kwa sababu zinaharibu haiba ya Mji; tunataka vikosi vyetu viwekeze kiuchumi, lakini vilevile tufanye tathmini ya kuangalia huu uwekezaji kama una tija. Lakini halikadhalika kuwema mazingira ya mji kwa sababu katika Mji wa Zanzibar kuna Kambi karibu tano na Kambi zote hizi zipo ndani ya mji. Sasa kama tutakuwa tunawekeza katika lengo siyo zuri tunaweza tukaaribu mazingira. Lakini pia kuna Kambi ya Welezo, ndani kule wamechimbisha mchanga ni mashimo matupu. Kwa hiyo, pia ningelikuomba Mheshimiwa Waziri ikiwekana ungefanya ziara ukaenda Zanzibar...

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Asya.

**T A A R I F A**

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, naomba ni mpe taarifa mchangiaji siyo tu kwamba kuna uharibifu wa kimazingira kwenye kambi, lakini kuna wananchi wanaishi pembezoni mwa kambi, yaani Kambi ya Jeshi kwa mfano kambi anayozungumza Mheshimiwa Soud ya Mtoni watu wanaishi hapa ndani ya Kambi. Kwa hiyo, ni hatari zaidi hata mabomu muda mwingine yanaporipuka madhara huwa yanatokea kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Soud unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, naipokea hiyo taarifa. Naomba niendelee haraka haraka muda wangu nafikiri utakuwa umenichungia kidogo.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kuna Kambi ya Welezo kuna Mheshimiwa mmoja pale alijenga jengo na akaambiwa kwamba lile jengo litakuwa sio salama na ikabidi afidiwe aondoke. Sasa utashangaa sasa hivi yeye ameondoka, lakini sasa hivi pana maduka ya miti, pana maduka ya *garage*, yameanzishwa pale sasa utashangaa

kama je, ilikuwa ni usalama ndio tukamuondosha yule. Sasa je, huu uwekezaji tunaouweka sasa hivi nao ni sahihi? *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningemuomba tu Mheshimiwa Waziri ukafanya ziara ukaenda Zanzibar na ikiwezekana ikikupendeza, ukafuatana na Mkurugenzi wa Mazingira, Mkurugenzi wa AZEMA...

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa muda umekwisha.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, na Mkurugenzi wa Misitu ili waweze kushauri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika bajeti hii nyeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na kupitia nafasi hii napenda nimpongeze sana Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuitazama na kuiongeza bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara Bwana Faraji Mnyepe na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Jenerali Venance Mabeho, mzalendo, mchapakazi na wasaidizi wake, makamanda na wanajeshi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wana mgambo hawa ni wakubwa sana kwetu maana sisi wale ma-*private soldier* ndio wamekuwa wakitufundisha sisi wana mgambo. Kwa hiyo, leo nilipoona makamanda hawa nilikuwa nasema sasa sijui nitoe

mchango wangu nikiwa nimebana mikono sasa, lakini kwa ujumla naonesha tu kwamba utii mkubwa sana kwa makamanda hawa ambao wanafanya kazi nzuri ya kizalendo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaanza na suala la doria kwenye mpaka wa maji wa DRC na Tanzania. Hali ya mipaka yetu kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri ni nzuri, mpaka wetu sisi na Burundi ambao tuko kule Kigoma na mpaka wetu sisi na Kongo ni nzuri sana. Isipokuwa yamekuwepo matukio katika Ziwa Tanganyika ambayo yamekuwa yakijitokeza na haya sio matukio ambayo unaweza ukasema ni ya kivita, hapana, ni matukio ya maharamia tu wa ziwani ambao wengine wanatoka nchi jirani, wanakuja maharamia hawa wana silaha wengine walikuwa kwenye majeshi ya nchi hizo huko zamani basi wanakuja wanachukua nyavu, mashine za wavuvi wetu na wanaondoka nazo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika nafasi hii ningependa kuomba kupitia bajeti hii kwamba jeshi letu liongeze doria katika Ziwa Tanganyika ili kusaidia wavuvi na wasafiri wengine katika mpaka wetu huu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa niliseme ni suala la fidia. Nakumbuka eneo la Kibirizi kule Kigoma jeshi letu kupitia kikosi cha 24KJ kimeongeza eneo lake na katika kuongeza eneo lake, kimechukua maeneo ya raia na wale raia hawana tatizo wamekubali na wako tayari kulipwa fidia. Lakini sasa tunakwenda mwaka wa tatu hawajalipwa fidia na hawawezi kuendeleza maeneo yale, wanataka fidia ile ikawasaidie kujenga maeneo mengine na kupata makazi bora.

Mheshimiwa Spika, ningeomba katika bajeti hii muwatazame wananchi hawa waliotoa maeneo yao kwa ajili ya jeshi, ili waweze kulipwa fidia na kwenda kuendeleza maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninge...

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Naona mchangiaji kama anasikitika, nilishawaambia Wabunge taarifa muda unaohusika ni wa yule mchangiaji mwenzio, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka kumpa taarifa ndogo tu kaka yangu pamoja na mchango mzuri, nchi hii kuna maeneo mengi sana yamechukuliwa na jeshi ikiwemo eneo la Kigamboni Amani Gomvu, wananchi wamechukuliwa eneo muda mrefu, lakini jeshi hawajasema chochote hawajalipa fidia na hawajatoa msimamo wao. Nilitaka kumpa hiyo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya mafunzo mtakuwa mnapeana wenyewe mkikutana kantini. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza taarifa naipokea kwa manufaa ya Taifa sio kwa manufaa ya eneo nililokuwa nachangia.

Mheshimiwa Spika, nimalizie hoja yangu kwa jambo dogo sana ambalo ningependa ndugu zangu na hasa kwenye jeshi walielewe vizuri. Kuna vijana hawa wanaoingia katika jeshi iwe JKT, iwe Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, wanachukua mazoezi wanaimba nyimbo zao wakati wa mazoezi. Mimi ningeomba maana kuna nyimbo zingine tumekuwa tukizisikia sasa hivi ukisikia tu wimbo ule unawaambia mabinti zako ingieni ndani mkae mara sijui fulani wewe, nilikusubiri sana nikalala mlango wazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwani hakuna nyimbo za kizalendo mimi naomba sana turudishe nyimbo za kizalendo kwenye jeshi. Nyimbo za kusifia waasisi wa Taifa letu, nyimbo za kumsifia Amiri Jeshi Mkuu, nyimbo za kumsifia Mkuu wa Majeshi

kama Jenerali Mabeho anavyofanya kazi vizuri, nyimbo za kulinda mipaka yetu, tuachane na hizi nyimbo ambazo ukizisikia tu unaona hawa vijana... *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha ahsante.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** ... mawazo yao yote yako kwenye ngono. Ahsante sana nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sina uhakika sana na mazoezi ya Mheshimiwa Kilumbe kama huwa anafanya, lakini sisi tunaofanya mazoezi nadhani nyimbo zote ni muhimu kulingana na jambo lenyewe linalokuwa linafanyika wakati huo. Kwa sababu nyimbo zingine zinakufanya ushindwe kupanda mlima, kwa hiyo, inakuwa mtihani kidogo. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma atafuatiwa na Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ajiandae.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti iliyokuwa mbele yetu.

Awali ya yote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako tukufu, lakini naomba uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuuliza swali hapa Bungeni kuhusiana na mgogoro uliopo Kijiji cha Tondoroni, Kata ya Kiluvya, Wilaya ya Kisarawe, Mkoani Pwani na majibu ya Mheshimiwa Waziri yalikuwa kama ifuatavyo kwamba; "tayari imeshaundwa *task force* kwa ajili ya kupitia migogoro yote iliyopo baina ya wananchi pamoja na Jeshi letu la Wananchi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo nitapenda kujua sasa *status* ikoje ya mgogoro unaoendelea wa Kijiji cha Tondoroni, Kata ya Kiluvya, Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani na Jeshi letu *task force* inasemaje? Nini hatma ya wananchi wa eneo hilo la Tondoroni? Mara ya mwisho katika eneo lile Serikali ililipa fidia lakini kile kilicholipwa kilikuwa kiduchu (kidogo), wananchi wakagoma kuondoka kwa ajili ya kupata nyongeza ama mapunjo ya madai yao. Lakini kilichofuata ni kwamba nyongeza hawakupewa na wananchi hawakuruhusiwa kuyaendeleza yale maeneo. Walipolima, walipojenga Jeshi lilikuwa linaingia usiku linabomoa na asubuhi linazua taharuki kubwa kuharibu mali za watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitapenda sana kupata majibu Mheshimiwa Waziri ukija ku-*wind up* ni nini majibu ya hiyo *task force* kuhusiana na wananchi wale?

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili na wa mwisho ni kuhusiana na suala hilo hilo la migogoro kati ya wananchi pamoja na Jeshi letu la Wananchi. Kwa sasa tunaangazia eneo la Kata ya Kazimzumbwi, Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wetu wa Pwani. Kuna mgogoro mkubwa unaoendelea kati ya wananchi wa Kata ya Kazimzumbwi pamoja na Jeshi Kikosi Na. 191KJ Kisarawe. Hali sio shwari kiasi kwamba kuna malalamiko na masikitiko ambayo tayari yameshawasilishwa katika Ofisi ya CCM Wilaya, juu ya wananchi kupigwa, kuvunjiwa mali zao, nyumba zao pamoja na mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa katika eneo lile la Kazimzumbwi Jeshi lilikuja likaomba nafasi ama likaomba eneo tukaweza kuwapatia eneo, lakini baadaye walirudi wakaomba waongezewe eneo la ukubwa wa mita 200. Serikali ya Kijiji iliwajibu kwamba hakuna hilo eneo, lakini Jeshi lilikaa kimya kwa muda na baadaye likafika likaanza kupiga watu, likaanza kudhuru watu na hatimaye wakatwaa hilo eneo la mita 200 na wakaongeza mita nyingine 300 kufika mita 500. Ni kwa nini Jeshi linatumia nguvu kubwa hivi, hivi imekosekana njia ya namna ya kutumika ili kama hilo eneo

linahitajika kwa sababu za kiusalama na bado wananchi wakaendelea kupata haki zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hii migogoro ni ya tangu na tangu tangu enzi ya Mkuu wa Mkoa akiwa Mwantumu Mahiza mpaka sasa *RC* wetu ni *RC* Kunenge bado majibu hayajapatikana. Watu hawa wanapata shida sana.

Mheshimiwa Spika, nimeonelea nizungumzie hoja hizi mbili za maeneo haya mawili kwa sababu haya ni maeneo yao kutoka kwa mababu zao. Kama Serikali mnataka lipeni fidi kwa wananchi, mnawaweka wananchi wetu katika hali tatatishi.

Kwa hiyo, nitakuomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujibu nipate majibu ya kina ya hoja na haja wana Kisarawe wanataka kusikia juu ya hatma yao na haki yao ya ardhi yao ya maeneo mawili niliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Zahor, hapana, Mheshimiwa Janeth nilikuwa nimekutaja kabla ya hawa.

Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa ruhusa ya kusimama leo, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa kibali na pumzi yake ya bure na kuweza kuchangia katika masuala ya ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu

Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, amefanya kazi kubwa tumetembelea vikosi tumekuta amefanya kazi kama alivyoahidi kwamba kazi inaendelea, lakini sisi tulikuja tuliona kazi zinaendelea maana ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Ulinzi kwa kazi kubwa pia wanayoifanya. Lakini kipekee nimpongeze Mkuu wa Majeshi Jenerali Mabeho, Mnadhimu Mkuu, Makamanda wote kwa kazi nzuri na njema wanayoifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona mara nyingi panapotokea maafa wanajeshi wamekuwa mstari wa mbele katika kwenda kusaidia wananchi. Lakini pia tulipata simanzi mwaka jana kwa kuondokewa na Rais wetu mpendwa wa Awamu ya Tano Dkt. John Magufuli, lakini Jeshi la Wananchi lilisimama imara likahakikisha nchi imetulia na mpaka sasa wananchi wana amani katika nchi yao, hongereni sana majeshi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalipongeza tena Jeshi tumetembelea Makao Makuu ya Ulinzi pale Kikombo tumekuta vitu vya ajabu, hatukutegemea kuona kama kuna wakandarasi wa kiwango cha juu cha aina ile. Ukipata nafasi nenda katembelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tulikuwa tunauliza hili jengo limejengwa na Mchina, Mjapani kama tulivyozoea, lakini jengo lile limejengwa na wataalam wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Lakini limetumia fedha kidogo lakini kwa ubora na hadhi ya hali ya juu, limeokoa shilingi bilioni 69; nani kama Jeshi la Wananchi wa Tanzania? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Hongereni sana makamanda. Hawa ni wazalendo, ni waadilifu iwapo Serikali itawajengea uwezo wataweza kufanya vitu vikubwa sana katika nchi hii. Kuna mambo mengine ambayo tunaweza

kuyasema kuna mengine hayasemeki, wanahitaji fedha. Kuna mazao ya kila aina ambayo wakipata kiwango kikubwa cha fedha, tutaweza kuuza katika nchi za jirani, tutaweza kuwaongezea uwezo Jeshi letu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu suala la...

**SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mama yangu weee. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, leo hunipi kidogo dakika moja basi niongee kimoja tu. Leo nihurumie najua umenikubalia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba barabara zilizopo pembezoni za Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya doria ya ulinzi ziwekewe lami zitengenezwe, kwa sababu nchi jirani wana barabara lakini huku wanajeshi wetu wanapata ugumu sana kwa sababu hatuna barabara ambazo zitasaidia doria katika mambo ya ulinzi. *(Makofi)*

Mwisho naomba bajeti iongezwe, bajeti ya ulinzi ni ndogo bajeti ya vyombo vya ulinzi vyote ziongezwe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma yuko pale nadhani amekusikia vizuri.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi miaka ya nyuma ilikuwa inaonesha hali nzuri sana katika hali za michezo. Tunajua michezo inatambulisha Taifa, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba Jeshi hili liendelee kuhimiza wanamichezo jeshini waweze kuisaidia Tanzania. Tunakumbuka kina Nyambui waliitambulisha Tanzania vizuri sana nyakati zile, sasa hivi mimi kama *promoter* wa ngumi tuna wachezaji watatu tu kutoka jeshini. Tuna wanangumi watatu wanatuwakilisha nje ya nchi kutoka jeshini, sasa Jeshi haliwezi kutupa wanangumi watatu, tunaomba muongeze wachezaji wa ngumi maana ngumi inalipa na inatambulisha Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumtambua Suleiman Gariatano ambaye ni mwanajeshi anatuwakilisha vizuri, Suleiman Kidunda anatuwakilisha vizuri, Bonabuchi anatuwakilisha vizuri, lakini JKT ina msichana Mnyakyusa mwenzangu Grace Mwakimere naye ni mpiga ngumi mzuri sana. Ninaomba tusimamie michezo ya ngumi Jeshini maana itasaidia kuisaidia Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye nyumba za wanajeshi. Mimi nimezaliwa kwenye Kambi ya Jeshi nyumba za jeshi kwa mfano *quarter* zile za Keko mpaka leo zimechaka, ukienda nyumba za Mwenge pale Mwenge magorofa ni chakavu sana. Ninashukuru kwamba mmejenga mwaka 2025 mpaka mwaka 2020 mmejitahidi sana kujenga nyumba, lakini zile za zamani mmeziacha kuzikarabati. Ninaomba bajeti hii muweze kuzikarabati wazazi wetu waweze kuendelea kukaa katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la maduka yale ya bei nafuu yaliyokuwa jeshini, yalikuwepo kwa muda mwingi mpaka sisi tunakua yalikuwepo, lakini miaka sita iliyopita yalisitishwa. Ninaomba yarudishwe kwa sababu wazazi wetu hawa na wanajeshi wetu na makamanda hawa hawana muda wa kufanya biashara zingine. Kwa hiyo, mkiwapa eneo la kwenda kununua vitu bei rahisi mnakuwa

mmewasaida na kuwapa motisha. Tusiwaache tu wakaishia kufuga bata na kuku kwenye *quarters* zetu. Tunaomba warudishiwe yale maduka ili waweze kupata vitu kwa bei rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la upandishwaji vyeo hasa wanawake, ninajua Waziri wewe ni mwanamke, ninaomba utazame wanawake makamanda, ambao bado wako Jeshini wanaofanya kazi vizuri wapandishwe vyeo kwa haraka. Najua hatupandishi cheo kwa sababu ni mwanamke, ninafahamu, kwa sababu, wako jeshini ni makamanda ninajua wana uwezo wa kupandishwa vyeo na wana uwezo wa kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo suingi hoja, aah naunga hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia sijasikia vizuri umeunga mkono hoja ama umesemaje? Ahsante sana kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Ali Juma Mohammed ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwanza nianze kwa kushukuru kumekuwa na ufuatilio wa muda mrefu wa kutaka kulipwa fidia kwa wananchi wa Kata ya Nyamisangura kwa maana ya Mtaa wa Bugosi, lakini na wananchi wa Kata ya Nkende kwa maana ya Mtaa wa Kenyam kwa takribani zaidi ya miaka 13. Kwa hiyo, tunapenda kushukuru sana kwanza nianze kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Fedha ambaye sasa hivi ni Makamu wa Rais, lakini aliyekuwa Waziri wa Ulinzi ambaye sasa hivi ni Rais wa Zanzibar na aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha kwa kweli Dkt. Ashatu Kijaji nimekuwa nikiwasumbua sana enzi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hatimaye pia niwashukuru mama yangu hapo Mama Tax Waziri wa Ulinzi, nimshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe lakini pia nimshukuru Meneja wa *Estate* Kanali Kamuhambwa na Mhasibu wa Wizara kwa kweli Meja Ndombwe. Nimekuwa nikiwasumbua sana wamekuwa wakitoa ushirikiano wa kutosha lakini vilevile Wizara ya Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Katibu Mkuu Tutuba. Wananchi wanawashukuru sana kwa sababu wameweza kupokea kiasi cha shilingi 2,182,000,000 ambapo wananchi zaidi ya 211 wamepewa fidia. Lakini kuna wananchi sita ambao walifanyiwa tathmini, lakini zoezi la uhakiki lilipokuwa kupita pale hawakuwepo kwa bahati mbaya sana, kwa hiyo, wao hawakuweza kupata fidia yao kwa kipindi hiki, lakini tathmini walishafanyiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba Wizara iweze kupeleka jopo la kufanya uhakiki, ili waweze kuwahakiki wale wananchi sasa waweze kulipwa fidia yao, wananchi sita bado wamebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna wananchi wawili ambao wenyewe hawakufanyiwa kabisa tathmini, walisema kwamba maeneo waliyopo yanakaribia mtoni kwa hiyo hawawezi kufanyiwa tathmini, lakini wananchi hawa ambao ni Samuel Mwita Maveiko pamoja na Marwa Mlimi walikuwa wemepanda miti pale na hiyo miti imefikia kuvunwa na kuweza kutengeneza mbao, lakini wamekataliwa wasivune miti ile na cha ajabu wanajeshi wenyewe wanavuna ile miti. Kwa hiyo, kama hawawalipi fidia basi wawaache wavune mazao yao waweze kuondoka kwenye lile eneo. Ningeomba sana Wizara muweze kuhakikisha kwamba mnawaruhusu wananchi hawa wanavuna yale mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia yale amaeneo ambayo tumewaachia sasa yako mjini na kuna barabara kama vile ilipo Lugalo pale, wananchi wa Kata ya Bumela, Mwema, Susuni, Nyandoto wanatumia ile barabara, lakini pia wananchi wanaotoka mjini kwenda kulima huko mashambani wanapita pale. Tungeomba sana waweze kupunguziwa zile adha ambazo wanakutananazo, waweze

kufanya kama ambavyo wanafanya kwenye miji mingine ambayo unakuta kuna jeshi lakini barabara inapita katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwa kumalizia ni kuhusu kwa kweli, kuna malimbikizo makubwa sana kwa wanajeshi ya likizo hawajalipwa. Tunaomba takribani miaka 10 walipeni hawa wanajeshi haya malimbikizo ya likizo ili waweze kujikimu. Wengine mpaka wanafariki hawajalipwa haya malimbikizo yao ya likizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Juma Mohamed. Mheshimiwa Jumanne Sagini ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na uchache wa muda, naomba nizungumze mambo machache yafuatayo; kwanza naomba kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye Amiri Jeshi Mkuu, lakini naomba nimshukuru pia kwa kututeulia kiongozi mzuri wa Wizara hii ambaye sisi kama Kamati ya Ulinzi tunafanya naye kazi kwa karibu na kwa kweli, amekuwa mtendaji wa karibu sana kwetu sisi kama Wanakamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nilishukuru jeshi letu likiongozwa na afande *CDF,* lakini pia likisaidiwa na wenzetu wa Jeshi la Kujenga Taifa, niwashukuru sana. Naomba nitoe shukrani kwa sababu kwanza nchi yetu imetulia, nchi yetu inafanya kazi kwa amani, imejenga mahusiano mazuri pamoja na majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu ya muda naomba kuzungumza mambo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; wenzangu wamezungumza maneno mengi sana ambayo ni muhimu na kwa kweli inasaidia kulijenga jeshi letu hili, lakini na kuweka usalama wa nchi yetu pamoja na mipaka yake. Ningeomba

la kwanza, tusaidie kwanza kuipitisha bajeti hii, lakini kama itawezekana tuone namna ambavyo tunaweza kuiongezea bajeti kwa sababu jeshi ni utafiti, jeshi ni vifaa na jeshi ni nyenzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuwa na jeshi ambalo tunaliminya minya tunataka lifanye kazi yetu ya kutulinda halafu bajeti yake tumeifinya. Tunamshukuru mama yetu kwa kuongeza bajeti, lakini bado jeshi letu linahitajika liwe na bajeti ya kutosha ili liweze kufanya kazi zetu kwa sababu jeshi kazi yake ni moja tu, ni kulinda mipaka ya Taifa letu kuhakikisha kwamba, sisi tunaishi vizuri, lakini tunalinda Taifa letu bila migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili; wakati wa amani jeshi letu linatumika kuzalisha mali. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge, Jeshi hili limeonesha uimara na weledi mkubwa katika kutekeleza mambo yake. Amesema dada yangu pale, tumekwenda kutembelea Makao Makuu ya Ulinzi, chombo hiki kimetengeneza au kinajenga Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa letu ambayo kwa kweli haijapata kutokea, lakini inatengeneza kwa gharama ndogo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake jeshi letu kwa kutumia wenzetu pia wa Jeshi la Kujenga Taifa wanatumia gharama ndogo. Nawaombeni sana tutawawezeshe na iwe ndio *priority* yetu sisi kama Bunge kuhakikisha kwamba tunatumia gharama ndogo lakini kwa utaalamu wetu wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano hapa, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alitangaza kuondoa wenzetu wanaoishi kwenye mbuga zetu kule. Mimi nilitegemea kwamba *priority* tungewapa wenzetu wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa sababu gharama ni ndogo, lakini utaalamu ni mkubwa. Sina hakika, lakini nina wasiwasi tumewatumia wenzetu wale wa JKT kama ndio ni *substitution,* hatukuwapa *priority. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuwaamini wenzetu wa Jeshi la Kujenga Taifa, lakini tuamine kwamba, uwezo wao ni mkubwa. Tusiwafanye kwamba hawa ni *second class* wajenzi, hapana, tuwatumie, tuwape kipaumbele. Ninaamini watafanya kazi kubwa, ninaamini watafanya kazi kwa kuzingatia uzalendo wa hali ya juu kwa hiyo, ningeomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kuliko yote nilizungumza juzi hapa kwamba, namna tunavyowaajiri vijana wetu kwenye jeshi vigezo vinatumika vingi. *(Makofi)*

Naomba nirudie tena leo kwamba kigezo pamoja na elimu, kigezo cha kwamba, vijana wetu wanaopitia Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi kwamba ndio kigezo kikubwa naomba sana hii iwe ni *addition* kwa sababu sisi kama jeshi hatuna uwezo wa kuwachukua vijana wote waliomaliza kidato cha pili, cha nne na cha sita kuingia ili wakapate mafunzo haya ya msingi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba sana tusiwanyime vijana wetu wengine ambao wanao uwezo wa kuingia katika vyombo vyetu hivi, *simply* kwa sababu, hawakupata nafasi ya kupita kwenye majeshi haya, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru sana. Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Sagini, mtoa hoja ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuweza kunijalia kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa dhati kabisa nilikuwa napenda sana nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa

kuweza kuwasilisha vizuri hotuba yake ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda nimpongeze Mkuu wa Majeshi *(CDF)* Jenerali Mabeyo, kwa kazi nzuri anayoifanya kupitia Jeshi letu hili, Jeshi la Ulinzi la wananchi wa Tanzania. Vilevile napenda nimpongeze kwa dhati Mnadhimu Mkuu wa Jeshi naye kwa kuendelea kufanya kazi nzuri kwa ajili ya Taifa letu na jeshi letu hili la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kaka yangu Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, amekuwa ni kiongiozi mwadilifu na anayetoa miongozo mizuri katika Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kwa ajili ya kulipongeza zaidi jeshi letu, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Katika kipindi kirefu katika nchi yetu wananchi wengi walikuwa wanachukua dhana ya kuwa jeshi letu kazi yake ni kulinda nchi pamoja na mipaka yake, lakini hivi sasa Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limejikita zaidi katika kuinua na kuimarisha uchumi wa Taifa letu na katika haya tumeona, Kamati tumetembelea mambo mengi na kiukweli tumeridhika na namna Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania wanavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jeshi letu sasa limekuwa lina taswira nzuri katika jamii yetu hasa katika mambo yale ya ujenzi majengo tofauti tofauti katika nchi yetu. Tumejionea majengo makubwa likiwemo la Ikulu ya Chamwino, Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa na Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji; haya ni majengo makubwa yamejengwa na wanajeshi wetu wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa katika nchi yetu ukitaka kuona majengo makubwa na mazuri, basi uangalie majengo

ambayo yamejengwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitaka kupata huduma nzuri za afya, basi angalia Jeshi la Wananchi wa Tanzania; ukitaka kuona mashamba mazuri ya kilimo pamoja na ufugaji wa samaki na mifugo mingine, basi liangalie Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania; ukitaka kuona elimu, shule ambazo zinasomesha vizuri, basi ni shule ambazo zinamilikiwa na Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania; ukitaka kuona wanamichezo wazuri, basi vilevile uangalie Wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania; na hata ukitaka kuona burudani na mambo mengine mazuri, basi pia uangalie Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile jeshi letu limeikuza nchi yetu...

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ukitaka pia kuona afya nzuri ya akili liangalie jeshi letu, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Taarifa hiyo.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea Taarifa ya dada yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jeshi letu vilevile limeipaisha vizuri nchi yetu ya Tanzania kwenye kada ya diplomasia ya nje. Jeshi letu mara kwa mara limekuwa likishiriki katika *mission* mbalimbali za kimataifa na hii imeipa taswira nzuri nchi yetu

ya Tanzania ya kuonekana ni nchi ambayo inajitolea kwa ajili ya mataifa mengine duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote ambayo nimeyazungumza yamekuja kutokana na usimamizi mkuu wa Amiri Jeshi Mkuu kwa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, mama yetu Samia Suluhu Hassan. Yeye ndiye ambaye anatoa miongozo mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kumalizia katika nchi yetu kuna *scheme* nyingi za umwagiliaji ambazo zimetelekezwa. Kwa vile jeshi letu linafanya kazi vizuri, hasa kupitia SUMA-JKT, nilikuwa naomba hizi *scheme* zote za umwagiliaji ambazo zimetelekezwa basi wapatiwe JKT ili waweze kuziendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba nzuri iliyojaa

ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika kuendeleza ulinzi na usalama wa Taifa letu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness).*

Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama ni mojawapo ya nguzo kuu katika kuongeza imani kwa wawekezaji hasa wa kutoka nje *(FDI).* Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu."

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, bado kuna wapiganaji wetu ambao ni wastaafu na wengine walishiriki kwenye vita kwa kulinda mipaka yetu hususani vita ya Kagera, wanalalamikia stahiki zao kutolipwa kikamilifu. Kwa kuzingatia kuwa wamefanya kazi kwa uzalendo mkubwa na iwe motisha kwa askari wetu wote kwenye majeshi yetu yote, napendekeza Serikali iangalie jinsi ya kutatua changamoto hii na kuangalia upya stahiki zao ikiwemo kuboresha mafao ya pensheni zao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ya Ulinzi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuangalia jinsi ya elimu ya ulinzi na usalama kuunganishwa kwenye mitaala ya elimu. Pia Serikali iendelee kuboresha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa ikiwemo mafunzo ya uzalendo na ujasiriamali. Kutokana na mafaniko makubwa huku nyuma ya mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, Serikali irudishe utaratibu wa mafunzo hayo kwa miezi kumi na mbili na mafunzo haya yawe maandalizi ya kuwajenga vijana kwenye uzalendo na ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na watendaji wake kwa kazi nzuri wanazofanya kuilinda nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966 Sura 192 na Sheria ya JKT ya mwaka 1963 Sura 193, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekabidhiwa jukumu la kusimamia Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina wajibu wa kuvipatia vyombo hivi mahitaji yake ya kimsingi ili kuviwezesha kutekeleza majukumu hayo. Katika hili, bado baadhi ya wanajeshi wetu hawajapatiwa huduma ya msingi ya kupatiwa nyumba za kuishi na walio wengi kuishi uraiani.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi duniani huwezi kumkuta mwanjeshi akipanga kwenye nyumba uraiani. Hii imewasaidia kuwajenga kisaikolojia askari wao na kutanguliza utaifa kwanza kutokana na Serikali zao kuwawekea mazingira bora ya kuishi pamoja.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza wanajeshi wetu wote wajengewe mazingira bora na familia zao kwa kujengewa makazi na kuishi kambini. Kwa kufanya hivi, hii itarahisisha kufuatilia nyendo zao na kusimamia maadili yao ya kazi za kijeshi. Vilivile, wakikaa pamoja kambini itarahisisha kuwapatia huduma muhimu kama maji, umeme, tiba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ina majukumu ya kulinda mipaka ya nchi yetu na kuandaa umma wa Watanzania kushiriki katika shughuli za ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha azma hii, ninapendekeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania lieendelee kutoa mafunzo ya ulinzi ya kimkakati wa mgambo kama sehemu muhimu ya jeshi la akiba. Napendekeza mafunzo haya yawe ni lazima kwenye mikoa yote inayopakana na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, uzoefu tulioupata kwenye vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine imeonesha kwamba jeshi la akiba linalohusisha wananchi wa rika mbalimbali huko Ukrane limetoa mchango kubwa kukabiliana na Taifa kubwa la Urusi lenye uwezo mkubwa wa kivita na silaha za kisasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali yetu chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na viongozi wetu wakuu na watendaji wote Serikalini. Kwa namna ya pekee nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Stergomena Tax, Waziri wetu wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na wakuu wote wa vyombo vya ulinzi kwa kuendelea kuitunza na kuilinda heshima ya kulinda mipaka ya Taifa katika nyanja za kitafa, kikanda na kimataifa. Rai yetu kwa vyombo vyetu waendelee kudumisha utii, uzalendo, ukakamavu, weledi na utaifa kwanza. Kwa kweli wanatuheshimisha mbele ya mataifa, hongereni sana Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, aidha niungane na Watanzania wote kukupongeza sana wewe Spika wetu na waheshimiwa Wabunge, viongozi wote waliochaguliwa na walioteuliwa kwenye nafasi zao mbalimbali tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kuwajalia kufanikisha majukumu yenu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe mchango wangu kupitia hotuba ya Wizara hii muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu; kwanza kutokana na umuhimu wa ujenzi wa Makao Makuu ya JWTZ Kikombo, Dodoma, tunaiomba sana Serikali itoe fedha za kukamilisha ujenzi huo. Hata hivyo tunaipongeza sana Serikali kwa kutumia mfumo wa *force account* kwani kutokana mfumo huu umeisaidia

sana Serikali kuokoa gharama kubwa za fedha katika ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali iangalie vyombo vyetu vingine vya ulinzi ili wawezeshwe kupata fedha za kutumia kujenga miradi ya maendeleo na miundombinu mingine kama vile magereza, vituo vya polisi, ofisi za mikoa na wilaya.

Pili, Serikali iangalie mpango wa kuwezesha upatikanaji wa fedha za kutosha, vitendea kazi, wataalam, kwenye mashirika ya NYUMBU, MZINGA na SUMA JKT ili mashirika hayo ambayo yana dira ya uzalishaji mali yaweze kutanua matawi ili kuongeza wigo wa ajira kwa vijana wote wanaomaliza mafunzo ya JKT na kuzalisha bidhaa ambayo zitakidhi haja kwenye masoko ya ndani ya nchi na nje.

Tatu, kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu katika mji wa Ddodoma hali itakayochochea mahitaji makubwa sana ya huduma za jamii hususan sekta ya afya, tunaiomba sana Serikali yetu ijitahidi sana kutoa fedha za ujenzi wa Hospitali ya Jeshi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nne, kutokana na mabadiliko ya teknolojia kubwa sana duniani, tunaiomba sana Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii katika nyanja za vifaa vya ulinzi na mafunzo ya muda mfupi, muda wa kati na mrefu ili kuongeza medani za kisasa zaidi katika ulinzi wa mipaka yetu na Taifa letu kikanda, kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho siyo kwa umuhimu naendelea kuvipongeza sana vyombo vyetu vya ulinzi katika utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Stergomena Tax (Mb) Waziri wa Ulinzi na Jeshi la

kujenga Taifa, Katibu Mkuu pamoja na Mkuu wa Majeshi kwa niaba ya Jeshi letu lote la Ulinzi na Kujenga Taifa nchini. Kipekee kabisa napenda kumpongeza sana Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiweka nchi yetu kuwa salama, yenye amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika napenda pia kuwapongeza kwa ushirikiano wanaotoa kwa mamlaka mbalimbali katika kuleta amani na kuifanya dunia kuwa mahali salama pa kuishi. Nawapongeza pia kwa kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, ombi letu, kama ambavyo nimekuwa nikichangia katika mipango mikakati yenu ni vema barabara za mpakani ikiwemo Mbamba bay – Lituhi; kufungua barabara ya mpaka wa Tanzania na Msumbilji ikiambaa na mpaka wetu, kama ambavyo miaka 1970 ililazimu kufungua barabara ya Mbamba bay - Lituhi kufuatia chokochoko za Malawi. Ni vema kujiweka sawa; na kuboresha makazi ya kiteule cha Liuli na gari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kukupongeza kwa kazi nzuri. Pia naomba kipekee nimpongeze Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa fursa hii nichangie kwenye hoja ya bajeti ya Wizara hii muhimu ya Ulinzi na Jeshi ya Kujenga Taifa na naomba niongelee unyang'anywaji wa mashamba Kijiji cha Luwa na Jeshi la Kujenga Taifa Kambi ya Luwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi limenyang'anya wananchi mashamba mnamo mwaka 2017 na mpaka kati ya jeshi na wananchi ni Mto Sopa lakini jeshi limevuka hadi kufika barabara ya mkoloni kuelekea Rukwa na kuchukua

mashamba ya wananchi wa Kijiji cha Ntendo, Luwa na Fyengelezya.

Mheshimiwa Spika, kipindi mashamba yananyang'anywa, kuna mali ziliharibiwa sana kwani walipewa muda mfupi kuondoka eneo hilo. Kuna mifugo ilikufa (ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na bata), pia kulikuwa na matanuli yaliyochukuliwa, nyumba tatu, mabanda ya mifugo, mazao ya kudumu ambayo ni matunda aina mbalimbali vipo shambani, majenereta na vifaa vya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika *operation* hii hakuna maongezi zaidi ya kuondolewa licha ya barua nyingi zilizoandikwa Serikalini bila majibu ya kuridhisha. Ushahidi ni nyumba zilizobaki pale maana hadi leo zipo.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri atoe majibu na afuatilie suala hii na kutupatia ufumbuzi wa mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimuite sasa Mheshimiwa Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, akichangia tutamalizia na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu asubuhi hii.

Kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao tumeona walio wengi kwa kweli wamechangia *very positively* kuhusu kazi nzuri ya ulinzi wa Taifa letu unaofanya na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na kwa kweli, hii kama alivyomaliza mzungumzaji wa mwisho, ni kazi nzuri na miongozo mizuri inayofanywa na Amiri Jeshi Mkuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Waziri wangu wa Ulinzi Dkt. Tax, lakini Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Majeshi na wasaidizi wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi zimezungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge, katika kuchangia naomba na mimi niseme machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja kuhusu umuhimu wa barabara za mpakani; hili kweli Serikali inajua umuhimu wake. Wizara ya Ulinzi na JKT itawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa madhumuni ya kuimarisha barabara hizi za mpakani. Hoja imezungumzwa ya kuweka lami, lakini nadhani jambo la msingi hizi barabara zote zianze kupitika halafu ziimarishwe kuwa barabara za lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja iliyoibuliwa na Mheshimiwa Ng'enda, tunashukuru moja umeisema, lakini nilitaka nichangie hii ya doria katika Ziwa Tanganyika, lakini pia tuseme na maziwa mengine hata na bahari yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili jeshi letu liko imara, lakini litaimarisha ushirikiano na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ikiwemo polisi na vyombo vingine, ili kuimarisha doria kwenye maeneo hayo. Tusingependa kuona wananchi wetu wanadhalilishwa na wahalifu au kama alivyowaita majambazi au maharamia kutoka nchi za jirani, lakini pia nikiri wapo hata miongoni mwa wananchi wa Tanzania wanaofanya vitendo hivi vya uhalifu, wote hawa wanahitajika kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, hili la nyimbo za kizalendo majeshini; tunaimarisha hilo sana. Zinaimbwa nyingi ila nyingine akiziona ni za hamasa tu. Na tunashukuru umetusaidia kwamba kuna mazingira fulani fulani ili waweze kufanya mazoezi hayo kwa ufanisi wanahitaji nyimbo zinazogusa hisia kama hizo ambazo Mheshimiwa Ng'enda alitaka kama vile kuzinyanyapaa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni hili la ajira; naomba nichangie kwenye hili la ajira; imeelezwa hapa, lakini nataka niseme kwa kweli, ajira si kwamba iko *restricted* kwa Jeshi la Wananchi tu, wale wanaopitia JKT. Hiki ni kigezo muhimu kwa sababu, tunazungumzia uzalendo, utayari, uchapakazi na JKT

ndio hutoa mafunzo ya namna hiyo. Kwa hiyo, sio Jeshi la Wananchi tu wanaolazimisha waajiriwa wao wapite huko, bali hata Polisi mmeona tumesema juzi hapa, Magereza pia, Uhamiaji, wote wanakuwa wamepitia huko, lakini hata taasisi za kiraia pia wanapitia huko.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo sasa naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamuita mtoa hoja kuhitimisha, wako wageni walioingia wakati tumetangaza tayari matangazo ya wageni; wako wageni nane wa Mheshimiwa Mhandisi Samuel Hhayuma ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania *(CWT)* wa Wilaya na Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 34 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 87 kutoka Chuo Kikuu Cha Tumaini, Mkoani Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrance Tax, aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, muda mchache uliopita niliwasilisha katika Bunge lako tukufu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2022/2023. Napenda kukushukuru kwa namna ulivyosimamia na kuongoza kwa umakini mjadala wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza, sina uhakika kama waliopo wamechangia kwa maandishi, lakini kama wapo hoja tutazipokea na tutazifanyia kazi, kwa hoja

nzuri zitakazochangia katika kuimarisha utendaji na ufanisi wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie kuwa maoni na ushauri wenu tumeuchukua na tutaufanyia kazi ili kuendelea kuboresha utendaji wa Wizara yetu na kutatua changamoto ambazo mmeziainisha. Wizara inatambua na kuthamini michango iliyotolewa ambayo imetolewa kwa nia njema iliyotawala mjadala na msingi wake ni kuboresha shughuli za utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni na ushauri waliotupatia. Ushauri tumeupokea tumeuzingatia, iliwasilishwa kwa muhtasari, lakini tumekwishaipata hiyo hotuba, kwa hiyo, tutafanyia kazi yale yote yaliyomo kwenye maoni mliyoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upekee napenda niwapongeze watendaji wote wa Wizara na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, kwa upande wa Wizara na Jenerali Venance Salvatory Mabeyo kwa upande wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kufanya kazi kwa weledi na kujituma na kuwezesha kufikia hatua hii ambapo tunaelekea kuhitimisha mjadala wa bajeti ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ujumla wao ambao katika mjadala wa asubuhi hii Waheshimiwa Wabunge 16 wameweza kuchangia. Asanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda napenda kuwahakikishia kuwa maelezo na majibu ya kina kuhusu hoja zote na michango yote iliyotolewa yataandaliwa

kwa maandishi na kila hoja itajibiwa na tutawasilisha Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia hotuba niliyoiwasilisha leo. Naomba nijikite katika hoja chache, kama nitaweza nitajibu zote ambazo kwa sehemu kubwa zimetawala mjadala wa hotuba ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kusema kwamba Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania tangu kuanzishwa kwake hapo tarehe 01 Septemba, 1964 limeendelea kukua na kuimarika kizana, kinyenzo, kiteknolojia na kiweledi kulingana na mahitaji ya wakati. Hali hii imeliwezesaha jeshi letu kutekeleza majukumu yake kwa umahiri mkubwa na kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuwa na amani na usalama hata pale ambapo pamekuwa na matishio, matishio hayo yamedhibitiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nalijibu hili kutokana na msisitizo mkubwa ambao mmeutoa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati kwamba Jeshi letu na taasisi zake halina budi kuongezewa nyenzo, halina budi kuongezewa rasilimali fedha na niwahakikishie tu kwamba hii imekuwa ni dhamira ya Serikali na Serikali imeendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi zimetolewa kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita na Amiri Jeshi Mkuu, na ni kweli ametoa uzito mkubwa sana kuhakikisha kwamba Jeshi letu linawezeshwa na taasisi zote. Kwa hiyo, pongezi zote ambazo mmezitoa mafanikio yote ambayo yametolewa naomba pongezi hizo ziende kwa Amiri Jeshi wetu Mkuu ambaye ametoa uzito stahiki, Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja iliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Waheshimiwa Wabunge wamechangia pia kuitaka Wizara

kuhakikisha kuwa miundombinu ya kiulinzi mipaka kwenye Kamati wamesema pia mpaka katika mwambao wa bahari inaimarishwa napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania tangu kuanzishwa kwake limeendelea kuwezeshwa kivifaa kama nilivyosema kizana na kiteknolojia kulingana na mabadiliko yanayotokana duniani. Ni dhamira ya Serikali kuendelea kuliwezesha Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania ipasavyo. Aidha, Wizara imeupokea ushauri huu muhimu na Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika eneo hili mahsusi kwa ulinzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Sera ya Ulinzi wa Taifa, hili pia limezungumzwa kwa nguvu sana na Mheshimiwa Saada nadhani naomba tu nitoe maelezo kwamba mchakato wa Sera ya Ulinzi wa Taifa ulianza mwaka 2008 ni kweli kama mlivyosema Waheshimiwa Wabunge kwamba mchakato huu ulianza muda mrefu sana. Hata hivyo sera hii ilichelewa kupata maoni kutoka kwa baadhi ya wadau muhimu, baada ya kupata maoni toka pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hii ilikuwa ni mwaka 2021 baada ya kupokea maoni hayo ilibainika pia kuwa yamekuwwepo maendeleo ya kitaifa na kimataifa katika sekta ya ulinzi yanayohitaji kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spik,a mwaka 2008 na mwaka 2021 ni muda mrefu sana kwa hiyo ilibidi kuirejea hii sera upya. Kwa hiyo kazi hii imekwishafanyika na rasimu iko tayari kwa hiyo sasa hivi kinachoendelea ni kuhakikisha tunakamilisha sera hii na kwa umuhimu wake sera hii inakamilishwa kwa pamoja na Mkakati wa Usalama wa Taifa na Mkakati wa ulinzi wa Taifa letu. Kwa hiyo mpango tulionao tunatarajia kwamba katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 Sera hii itaweza kuwa imekamilika Wizara imetoa kipaumbele kikubwa sana kwa sera hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutoa ufafanuzi kuhusu umuhimu wa kuliwezesha Jeshi ikiwa ni pamoja na taasisi zake ikiwemo NYUMBU na ikiwemo Shirika la MZINGA

kirasilimali fedha na watu. Kama ilivyo kwa taasisi nyingine Jeshi na taasisi zake zinahitaji rasilimali fedha na zinahitaji rasilimali watu ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuilinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mipaka yake, kufanya tafiti na ubunifu, lakini pia kuzalisha mazao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nikiwasilisha hotuba asubuhi hii nilieleza wazi kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan ambaye ni pia ni Amiri Jeshi Mkuu imetoa uzito sana katika sekta ya ulinzi na kwa muktadha huu katika bajeti ambayo nimeiwasilisha tumepata ongezeko la shilingi 53,754,747,000 ikiwa ni sawa na 15% kama ambavyo pia ilielezwa na Kamati ya Bunge wakati ikiwasilisha taarifa yake ambapo Wizara imepata ongezeko la 14%; Ngome imepata ongezeko la 16%; na JKT imepata ongezeko la 10%. Pia kuhusu rasilimaliwatu tayari tumekwishapata vibali vya kuandikisha askari na kuajiri watumishi wapya katika mwaka wa fedha 2023 kwa hiyo hii itatusaidia kuziba pengo ambalo mmelisisitiza Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mashirika ya NYUMBU, *TATC* na MZINGA pamoja na kutoa fedha kwa ajili ya kununua mitambo mashine na malighafi jitihada zinaendelea ili kuhakikisha kuwa mashirika haya yanawezeshwa kikamilfu ili kutimiza azma ya kuanzishwa kwake. Kwa kutambua umuhimu wa Shirika la *TATC* ambayo ni NYUMBU inavyoeleweka zaidi mpango wa maendeleo wa miaka 15 ambao ulirejewa wa kuliimarisha Shirika la NYUMBU utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha huu 2022/2023 na kiasi cha shilingi 20,445,970,300 tayari kimeshatengwa. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba mawazo yenu, maoni yenu Kamati imesema kwamba imekuwa ikitoa maoni haya kwa muda mrefu yamezingatiwa na sasa mpango uliopitishwa unaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huu utakuwa na manufaa makubwa ikiwa ni pamoja na

kupunguza gharama za uagizaji wa magari, zana, mitambo na vipuri na kukuza uwezo wa nchi katika utafiti na wa teknolojia za magari na mitambo jambo ambalo ni muhimu sana kwa Taifa lolote kuweza kujitegemea katika sekta hii.

Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametoa uzito lakini naomba ninukuu kauli yake katika hili ambapo amekuwa akisema kwamba; "yajayo yanafurahisha." Kwa hiyo naomba tu tujipe muda tufanye huu utekelezaji na hayo yajayo yanayofurahisha mtayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu umuhimu wa utekelezaji wa miradi ya kilimo cha kimkakati hususan huko Chita na shamba la Mgeta, Mkoani Morogoro na msisitizo umewekwa katika kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Miradi hii ni muhimu sana kwa Taifa na kwa maono mapana kama ambavyo ilivyoelezwa unazo faida nyingi ikiwa ni pamoja na kuipunguzia Serikali gharama za kuwalisha vijana, kuchangia katika usalama wa chakula na moja ambalo halikusemwa na pia mradi huu miradi hii inatarajiwa kuchangia katika upatikanaji wa mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo jana alivyokuwa akitoa hotuba yake alisisitiza pia kwamba umuhimu wa mbegu ni kitu muhimu sana ili kuhakikisha kwamba unachangia katika upatikanaji wa chakula wa Taifa lakini na usalama wa chakula wa Taifa letu. Kwa hiyo, hili pia miradi hii itachangia katika hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huu Serikali imeendelea kutenga fedha toka vyanzo vya ndani, lakini pia tunatafuta mikopo kwa ajili ya kuendeleza miradi hii na Mheshimiwa Waziri wa Fedha anatusaidia katika hilo. Kama nilivyosema utekelezaji wa miradi hii ya kimkakati utaliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kujitosheleza kwa chakula na hatimaye kuimarisha usalama wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi limejitokeza kwa kiasi kikubwa katika mjadala; napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako tukufu kuwa Wizara imetoa kipaumbele kikubwa katika utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania na wananchi na nina imani sote ni mashahidi tumeiona kazi kubwa inayoendelea. Hadi sasa utekelezaji wa mpango huo wa miaka mitatu unaendelea kwa ufanisi wa hali ya juu. Kazi hii ni sehemu ya timu za Wizara nane ambayo timu hii iliundwa na Mheshimiwa Rais lakini inasimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kama alivyoeleza asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango huo umejumuisha migogoro 87 na mpaka sasa migogoro 58, maeneo 58 yamekwishapimwa na kuwekewa mipaka kwa sababu suala la mipaka limesisitizwa sana na maeneo 17 yamefanyiwa uthamini na kati ya yaliyofanyiwa uthamini maeneo tisa yameshalipiwa fidia na asubuhi niliyataja sita, lakini tisa ni kwa ujumla wake tangu tumeanza kutekeleza. *(Makofi)*

Kwa hiyo yaliyosalia yanaendelea ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyoongelewa leo hapa na Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Saada Mansour na Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda na Mheshimiwa Hawa Mchafu yote haya yamejumuishwa katika mpango huu katika yale ambayo yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hawa Mchafu amenitaka nimpe taarifa ya *task force* hatua iliyofikiwa nimuombe tu kumuhakikishia Mheshimiwa Mchafu kwamba kazi hii tayari ripoti imeshawasilishwa nipatie tu muda niende niipitie ripoti hii na tutawasiliana tuone jinsi tutakavyo kamilisha zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo napenda kuwashukuru viongozi wote na wananchi katika maeneo mbalimbali kwa ushirikiano mkubwa uliowezesha Wizara kutatua changamoto hizo. Aidha, niwapongeze maafisa na watumishi wa Wizara wengine wametajwa humu kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za dhati za kutatua migogoro hii ambazo ni shirikishi nawaomba sana wananchi watambue umuhimu wa maeneo tunayohitaji kama Jeshi la Kujenga Taifa na pale ambalo tunahitaji kuchukua maeneo haya basi tushirikiane tuweze kupata maeneo haya, lakini pale ambapo maeneo yamekwishachukuliwa tuwaombe sana wasirudi kwenye maeneo haya. Kwa kufanya hivyo ni hatari kwao lakini pia ni kuzusha migogoro mipya. Kwa hiyo tushirikiane wote tuweze kwa kutoa elimu hii ili wote tuweze kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limejitokeza ni uboreshaji na kuongeza makazi ya wanajeshi; hili ni suala muhimu sana na tunalipa uzito unaotakiwa naomba tu kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Wizara inaendelea na utekelezaji wa mpango wa nyumba 10,000 kwa wanajeshi na hadi sasa nyumba 6,064 zimeshajengwa katika mikoa mbalimbali. Mpango uliopo ni kukamilisha hizo takribani 4000 zilizobaki na kuongeza zaidi pamoja na kwamba katika mwaka huu hatukuweza kutenga fedha, lakini bado tunaendelea kutafuta rasilimali ili kuhakikisha kwamba tunaongeza nyumba kwa ajili ya makazi ya wanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa niaba ya watumishi wote kabla kulikuwa na hoja zingine chache ziizoletwa ambazo nyingine amenisaidia kuzijibu Naibu Waziri namshukuru sana kwa hilo, lakini nilipenda kuongelea suala la kuajiri vijana, alitoa hoja kwamba kuna vijana walifanya shughuli mbalimbali, lakini hawakuweza kuchukuliwa.

Nipende tu kuwafahamisha kwamba naimesemwa vizuri sana nafikiri na Mheshimiwa mmoja kwamba sababu kubwa ya kuwachukua vijana kwenda JKT ni kuwajengea stadi na hivyo ndivyo tunafanya na imeongezwa kwamba tuwajengee ufundi, hata hilo linafanyika. Kwa hiyo wanapokwenda JKT kinachotarajiwa pale ni kwamba wanajengewa stadi na baada ya pale waweze kwenda kujitegemea.

Kwa hiyo si rahisi kuweza kuwachukua vijana wote wanaokwenda JKT waende kuajiriwa kwa sababu kwanza hilo siyo lengo, lengo ni kuwapatia stadi lakini ushauri mzuri kabisa tumeupokea wa Mheshimiwa Asia Halamga na pia huu ulitolewa na Mheshimiwa Haji Amour kwamba pamoja na hayo tuweze kujaribu kuunganisha nguvu kama Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda kuona kwamba baada ya hapo tunawafanyia nini.

Nipende tu kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hili tayari tunalifanyia kazi, tayari nimekwishaongea na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na jana wakati akiwasilisha hoja yake moja ya eneo tuliloona tunaweza kulifanyia kazi mara moja ni kwenye upungufu wa sekta ya mafuta. Alieleza hapa kuna ukwasi mkubwa sana, kwa hiyo, tunataka tuone kwamba tunaweza kujumuisha nguvu zetu namna gani na kuwatumia hawa vijana wakaweza kushiriki katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia mazungumzo yanaendelea tuone kwamba na Wizara ya Viwanda tunaweza kushirikiana nao namna gani. Ushauri tumeuchukua lakini nipende kukuhakikishia kwamba tayari tunaufanyia kazi hata kabla ya hapo sisi tumekuwa tukijiuliza kwamba tukishawapa hizi taaluma basi waende kufanya nini, tuwawezeshe vipi, tunashukuru kwamba mmeongeza sauti katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira; upandaji wa miti tunashukuru kwa pongezi hizo lakini ushauri kwamba tuongeze pia tumeuchukua, tutaufanyiakazi na ushauri wa kutoa elimu katika kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji usio na tija, naomba tu niseme kwamba uwekezaji unaofanywa na Jeshi umekuwa na tija kubwa sana rasilimali tunazozipata kutoka Serikalini ni kidogo na nikiwapa takwimu ni kwa kiasi gani uwekezaji huu umeweza hata kusaidia Jeshi la Ulinzi na Wananchi wa Tanzania kutekeleza majukumu yao ya msingi mtashangaa. Kwa hiyo, lakini kama yapo uwekezaji ambao unafikirika

hauna madhara basi tutauangalia tuhakikishe kwamba madhara ya namna hiyo tunajikinga nayo lakini uwekezaji huu ni muhimu na umekuwa na tija sana.

Mheshimiwa Spika, mengine yalijibiwa; barabara limejibiwa lakini pia nipende tu kuwahakikishia kwamba barabara za doria na ulinzi ni kitu muhimu sana na hiki tayari nimekwishafanya mazungumzo na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na si barabara hiyo moja tu iliyoelezwa, ziko barabara nyingi na tayari baadhi zimeshaanza kufanyiwa kazi lakini baadhi tunaangalia jinsi gani ya kuziingiza katika mipango ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upandishaji vyeo wanawake; wanawake wanafanyakazi kama wanaume na hakuna ubaguzi katika upandishaji vyeo, vyeo vinapandishwa bila kujali jinsia kinachotakiwa katika Jeshi tu ni weledi, kwa hiyo, wanawake wanaendelezwa na wanapandishwa vyeo na wapo katika sehemu mbalimbali.

Kuhusu malimbikizo ya likizo hili limekwishafanyiwa kazi katika hotuba nimeeleza kwamba pamoja na mambo mengine Serikali imetoa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunalipa madeni yote na hili limeshafanyiwa kazi kama wapo waliobaki basi hao wataendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, michezo ni muhimu tumesikia na tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa niaba ya watumishi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake kupokea shukrani na pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa ya kulinda mipaka yetu. Wengi mmetoa shukrani nazipokea kwa niaba ya Wizara na kudumisha amani na mmetoa maeneo mengi yanayofanyiwa kazi nzuri ikiwa ni pamoja na katika sekta ya afya, katika sekta ya elimu, lakini pia mmeeleza katika jinsi Jeshi lilivyosimama kuhakikisha kwamba nchi yetu imebaki salama wakati tumepata msiba wa Mheshimiwa wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na maeneo mengi. Kwa hiyo tunapongeza na

pia kutoa mfano kwamba kwa kazi nzuri tumeweza kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 65 katika ujenzi wa Kikombo, mifano ilikuwa mingi lakini napenda kushukuru na kuhakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa kazi zote zinazofanywa na Jeshi la Ulinzi na Wananchi wa Tanzania zinafanywa kwa weledi, umahiri na uzalendo wa hali ya juu na hii ndiyo misingi ya utendaji wa Jeshi letu na kazi nzuri zitaendelezwa daima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri muda umeshaisha, lakini nakuongeza dakika tatu umalizie na Waheshimiwa Wabunge naongeza nusu saa tumalizie shughuli iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na kazi nzuri hizi zitaendelezwa kufanywa daima tu.

Mheshimiwa Spika, tumepokea pongezi ahsante baada ya ufafanuzi huu na kabla sijahitimisha hoja yangu naomba niwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii, waliofatilia hotuba na mijadala na naamini tutaendelea kushirikiana katika kudumisha ulinzi na amani na kuwaletea watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu katika kudumisha amani na kuwaletea wananchi maendeleo zinapaswa kuungwa mkono na sisi sote kama ambavyo mmeeleza ninyi wenyewe mmeshuhudia kwamba anafanyakazi kubwa kama Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inamshukuru kwa dhati kwa namna ambavyo amekuwa akisimamia ulinzi na usalama na kuwa mstari wa mbele katika kutatua changamoto zinazoikabili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake tangu aingie madarakani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa pia mstari wa mbele kuidumisha diplomasia ya ulinzi na ameendelea kuiletea heshima nchi yetu kama Amiri Jeshi Mkuu mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie lugha hii ingawaje siyo rasmi kwamba ameupiga mwingi kwa kutusimamia kitaifa lakini pia kutupaisha kimataifa. Tuendelee kumuunga mkono Rais wetu mpendwa na napenda kusema kuwa wanawake wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na watanzania wote kuwa chini ya uongozi mahiri wa Amiri Jeshi Mkuu Mama Samia Suluhu Hassan, Wizara ya Ulinzi na Taasisi zake zipo imara kuhakikisha kuwa nchi ipo imara na salama muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha naomba nitoe wito kwenu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kuwa ulinzi wa Taifa letu ni jukumu la kila Mtanzania, ni jukumu la kila mmoja wetu na kila mmoja wetu anao wajibu wa kulitekeleza jukumu hilo. Wanajeshi wetu wanafanya kazi kubwa sana usiku na mchana kwa weledi, uhodari na uzalendo wa hali ya juu nawapongeza sana kwa moyo huo wa kujituma na kwa kazi kubwa wanayoifanya niwaombe sasa tuwaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu!

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu!

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kitabu namba mbili, Matumizi ya Kawaida tunaanza ukurasa wa 389.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*.......Sh. 19,715,900,200

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Amandus Chinguile anahitaji ufafanuzi wa jambo mahsusi la kisera.

Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nilikuwa naomba ufafanuzi wa maelezo ya kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya migogoro hii ambayo kila kona sasa maeneo yale ambayo yamezungukwa na jeshi kuna migogoro hii ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anahitimisha hapa amesema upo utaratibu unaandaliwa na ipo timu maalum ambayo inapitia migogoro hii. Na hii inaweza ikatoa mahusiano mabaya baina ya majeshi yetu na wananchi wetu ambao wanakaa karibu na maeneo haya ya jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii kushika shilingi ila naomba ufafanuzi na maelezo ya kutosha juu ya jambo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuomba ufafanuzi napata shida kidogo kwa maana nitarudia yale yale ambayo nimekwisha yasema kwamba hili suala la utatuzi wa migogoro ni suala ambalo tumelipa uzito sana kama Wizara, lakini kama pia Serikali, na tayari maeneo yote hata uliyoyataja tumeshafika, tumeshafanya mazungumzo na wananchi kinachotakiwa sasa ni kukamilisha hatua kwa hapo tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tunalifanyia kazi na kama atahitaji maelezo ya zaidi nipo tayari kukutana naye na kumpatia ufafanuzi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kifungu kinaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 298,990,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*............Sh. 868,360,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 281,577,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*................................................Sh. 254,400,000
Kifungu 1006 – *Legal Service Division*.................Sh. 203,757,200
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*....................................Sh. 193,760,200
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit*..........................Sh. 394,200,000

Kifungu 2001 – *Industries, Construction and Agriculture Division*....................Sh. 398,124,000
Kifungu 2002 – *Military Research and Development Division*..............Sh. 908,021,400
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*.....Sh. 350,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 38 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Ngome**

Kifungu 1001 – *National Defence Headquarter (NDHQ)*......Sh.2,033,986,954,050
Kifungu 1006 – *Defence Forces Headquarter Command*................................Sh.2,395,375,200
Kifungu 1007 – *Land Forces Command*..........Sh. 3,681,543,000
Kifungu 1008 – *Air Defence Command*..........Sh. 3,416,107,050
Kifungu 1009 – *Navy Command*.......................Sh. 1,925,232,600
Kifungu 1010 – *Military Hospitals*.......................Sh. 2,318,291,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - JKT**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*....Sh. 411,863,641,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 38 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Ngome**

Kifungu 1001 – *National Defence Headquarter (NDHQ)*............Sh.56,367,636,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - JKT**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*....Sh. 13,965,535,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*.......Sh. 500,000,000
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit*.......................Sh. 2,000,000,000
Kifungu 2001 – *Industries, Construction and Agriculture Division*..............Sh. 16,658,277,700
Kifungu 2002 – *Military Research and Development Division*......Sh. 118,841,722,300
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*...........Sh. 22,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 Kanuni ya 123(3) (a) na (b) naomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO;** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa nitawahoji waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa akisaidiwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa wasilisho lake ama kwa hotuba yake ambayo imepokelewa na Wabunge na imepitishwa bila mabadiliko yoyote kwa hiyo nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri uliyoifanya, lakini pia tunakupongeza kwa ushirikiano mzuri unaoutoa kwa kamati kwa sababu taarifa iliyotolewa na Kamati hapa imeashiria kwamba mna ushirikiano wa karibu na upande wa Serikali mnasikiliza

mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo tunakupongeza sana pia kwa hilo. *(Makofi)*

Pia tunakupongeza wewe pamoja na watendaji wa Wizara yako na viongozi wote ambao wamepata nafasi ya kuja hapa leo na wamepata nafasi ya kutambulishwa wakiongozwa na Katibu Mkuu, lakini pia Jenerali wa Majeshi yetu tunamshukuru pia kwa kazi nzuri na viongozi wote wanaohusika kila mtu kwa ngazi yake na pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushirikiana na Jeshi hatujapata malalamiko kwasababu wenzetu wa Jeshi wamezoea *salute* na mambo fulani hivi ndio maana mmeona wamependeza hapa kwa hiyo kidogo Kamati ikiwa haiendi sawasawa na wenyewe wanapata changamoto. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana Kamati kwa ushirikiano mnaoutoa kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru pia wale ambao sio wajumbe wa Kamati hii lakini wamepata nafasi ya kuchangia hapa Bungeni wametoa maelezo kuhusu maeneo ya watu wanaowawakilisha na changamoto walizonazo na Mheshimiwa Waziri amesema hapa yote wameyachukua. Kwa hiyo niwapongeze pia kwa kuwasemea wananchi wenu katika maeneo mbalimbali na kwa ujumla mawazo mliyoyatoa kuhusu bajeti hii ili Taifa letu liendelee kuwa salama.

Kwa kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nitangaze rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri na watendaji wako tunawatakiwa kila la heri katika utekelezaji wa yale ambayo

mmeyaahidi kuyafanya katika mwaka huu wa fedha na kama mlivyowasikia Wabunge wana matumaini makubwa kwa fedha hizo ambazo zimeongezeka katika bajeti hii ya mwaka 2022/2023 tunaamini mambo yatakuwa mazuri zaidi kuliko yake ambayo Wabunge walikuwa wakiyapongeza hapa na tunaamini bajeti ijayo basi pongezi pengine zitakuwa zimeongezeka zaidi kuliko hata haya ambayo machache wameyaeleza changamoto za maeneo mbalimbali. Tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine ambao waliingia mchana na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi; wageni wawili wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi mmojawapo wa hawa wageni ni mshona suti wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi sijui ni yupi kati ya hawa mshona suti wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi hapa anaitwa Clementina Felix Korongo, kwa hiyo mkimuona Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi amependeza basi mnaweza mkachukua namba ya simu ili na ninyi mkashonewe huko, ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimepata malalamiko yenu kuhusu baridi humu ndani, tumepata malalamiko yenu, tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Lakini nifafanue tu kidogo kwamba tutajitahidi isiwe baridi sana kama hivi, lakini baridi hii ni ya muhimu kwasababu tupo wengi humu ndani na jengo letu limefungwa, hakuna sehemu ambayo ipo wazi kwa ajili ya kuingiza hewa. Kwa hiyo baridi hii ni ya muhimu sana hasa ukizingatia kwa ile afya yetu ya akili. *(Kicheko)*

Kwa hiyo tutalifanyia kazi Waheshimiwa Wabunge, lakini baridi ni muhimu pia kwetu si kwa kiasi hiki lakini baridi ni ya muhimu kwa sababu tupo wengi humu ndani na ni muhimu kutunza afya zetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nimepata taarifa kutoka kwa wananchi sehemu mbalimbali wakizungumzia kuhusu kuzimwa kwa magari wengine wamefurahi lakini wengine

wanasikitika kwamba madereva bado wanaacha magari, sasa wanatuma namba za magari. *(Kicheko)*

Kwa hiyo magari yale yanayoachwa sasa yakiendelea kuwaka wakati tumeshasema yazimwe yanatumwa, kwa hiyo naamini mabadiliko yataendelea katika wiki moja hii. Halafu huko baadaye tutaanza kutaja hapa namba za magari ambayo yanaendelea kuunguruma wakati hayupo dereva wala *boss* ndani ya gari.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.15 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 20 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*